# Nipashe

Jumanne Machi 26, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579875

www.ippmedia.com

ter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Vigogo CCM kortini kwa tuhuma rushwa mil. 5/-

UKURASA 2




UKURASA 13

# Maswali magumu JPM mapato Taifa

• **Ashangaa** ubovu miundombinu, ahoji ziliko fedha za waliokosa mechi, waliocheza Afcon 1980 wakumbukwa...*Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### SERIKALI YASHANGAA AJIRA WAGENI HOTELI ZA KITALII

SERIKALI imesema kuna haja ya kufanya tathmini ya mfumo wa elimu unaotumika nchini, kufuatia nafasi za juu katika hoteli nyingi za kitalii nchini kushikwa na raia...

UKURASA WA 5

### HARUFU YA UFISADI YASHTUA WABUNGE

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imebaini ubadhirifu wa zaidi ya shilingi bilioni 1.4 kutokana na kutumika kinyume cha taratibu...


## Madalali wayanawa mahekalu ya Lugumi

UKURASA 3



Rais John Magufuli akimsikiliza mchezaji wa zamani wa Taifa Stars, Peter Tino, ambaye alifunga goli moja lililoipeleka Tanzania kwa mara ya kwanza kufuzu fainali za michuano ya AFCON mwaka 1980, iliyofanyika nchini Nigeria, alipokutana na wachezaji wa Taifa Stars, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. Rais pia alimzawadia mchezaji huyo shilingi milioni tano. **PICHA: IKULU**



UK.2

## Mdhamini Lissu atamani kujitoa


**MICHEZO** **MAGUFULI: VITA AFCON IMEANZA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Maswali magumu ya JPM mapato Uwanja wa Taifa

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amehoji maswali magumu kuhusu uhalisia wa ukusanyaji na matumizi ya mapato ya Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Vilevile, amehoji kuhusu ukarabati wa uwanja huo, usalama wa mashabiki na mfumo wa ukataji tiketi, akitolea mfano mechi ya juzi ambayo Tanzania ilishinda 3-0 dhidi ya Uganda, kukiwa na idadi kubwa ya mashabiki nje ya uwanja huo wakiwa na tiketi, lakini hawakuruhusiwa kuingia kutokana na uwanja kufurika.

Akizungumza Ikulu jijini Dar es Salaam jana na wanamichezo walioipa sifa Tanzania hivi karibuni, wakiwamo wachezaji wa Taifa Stars na bondia Hassan Mwakinyo, Rais Magufuli alisema kuna maswali magumu ambayo Watanzania wanajiuliza kuhusu mchezo wa mpira wa miguu na wangependa kupata majibu.

"Nimeona (Leodgar) Tenga, Waziri (Harrison) Mwakyembe, Rais wa TFF wanani-chomekea chomekea kuhusu mashindano makubwa yanayotarajia kufanyika nchini, na mimi naona mwelekeo wao ni uleule wa kuomba omba pesa," Rais Magufuli alisema na kuongeza:

"Ingawa mimi sijauliza wala sikutaka kuuliza kwamba jana (juzi) mlikata tiketi nyingi, na uwezo wa uwanja ni watu 63,000, na zaidi ya nusu ya watu walikuwa nje, zimekusanywa kiasi gani? Sijauliza na wala siulizi. Na hizo zingine zimeenda kwenye akaunti gani? Siulizi."

Rais Magufuli alibainisha kuwa mambo mengi hayako vizuri kwenye Uwanja wa Taifa licha ya wizara kupewa mgao wa mapato kwa kila mechi inayochezwa katika uwanja huo kwa ajili ya ukarabati na usimamizi.

"Ukarabati hauko vizuri, asilimia zinazokatwa kwa ajili ya ukarabati wa uwanja zinatumika kufanya nini? Je, wizara inafanya nini? Je, viongozi wa wizara huwa hawaendi uwanjani kuona? Kama uwezo wa uwanja ni kuchukua watazamaji 63,000, na kama watu wengi walikata tiketi, je, tiketi za Tanzania hazina 'limit' (ukomo)?" Rais Magufuli alihoji.

"Je, suala la ulinzi limeangaliwaje na wizara? Je, kama watu 200,000 wangeingia ndani? Je, kama wangedondoka, watu wangapi wangefariki? Je, wizara, vyombo vya ulinzi wanalionaje suala hili?

"Je, fedha tunazoanza kupokea kutoka FIFA (Shirikisho la Soka la Kimataifa) zinatumika vizuri? Makusanyo yetu tunayoyapata tunawasaidiaje wachezaji? Wananufaikaje na jasho lao?" Rais Magufuli alihoji zaidi.

Alisema hayo ni maswali muhimu ambayo serikali, wizara na taasisi mbalimbali za michezo wanapaswa kuyatolea majibu, akisisitiza kuwa kama tunahitaji kujenga taifa lenye heshima, ni lazima maswali hayo yapatiwe majibu.

Kabla ya kujengwa kwa Uwanja wa Soccer City, Afrika Kusini mwaka 2010, Uwanja wa Taifa ndiyo uliokuwa uwanja mkubwa zaidi barani Afrika. Uwanja huo ambao ni miongoni mwa viwanja vichache vya soka nchini vinavyomilikiwa na serikali, ukiwa na uwezo wa kuketisha watazamaji 57,558.

Ushawishi wa marais wastaafu Benjemin Mkapa na Dk. Jakaya Kikwete kwa mataifa ya nje, ndiyo ulioifanya Serikali ya China ikubali kushirikiana na Serikali ya Tanzania kujenga Uwanja wa Taifa. Uwanja huo ulijengwa 2007 kwa gharama ya Sh. bilioni 56 (Serikali ya Tanzania ilichangia Sh. bilioni 25).

Rais Magufuli alisema Watanzania wanapenda michezo na wanaumia pindi timu yao inapofungwa, hivyo akaitaka Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kuhakikisha ushindi wa juzi unaendelezwa katika mechi zinazofuatwa.

"Kwanini kina (Peter) Tino na Tenga walituingiza kwenye mashindano haya (Fainali za Mataifa ya Afrika - Afcon) mwaka 1980 na baada ya hapo hatujaingia tena? 'Why' (kwanini)?

"Kwanini tukienda kwenye mashindano ya kukimbia hatuchukui nafasi na kufanya

INAENDELEA UK 8



Mchuuzi wa mifagio akisaka wateja katika eneo la Msasani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Vigogo watatu CCM Dar kortini kwa rushwa

**Waandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imewafikisha mahakamani viongozi watatu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa.

Washtakiwa hao walifikishwa jana katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, wakishtakiwa kwa madai ya kuomba na kupokea rushwa kwa ajili ya kutoa eneo la kupanga katika kiwanja kinachomilikiwa na CCM.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo na kusomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mfawidhi, Martha Mpaze.

Mwendesha Mashtaka wa Takukuru Ilala, Veronica Chimwenda, akisaidiwa na Sophia Gura, mbele ya Hakimu Mpaze, aliwataja washtakiwa hao kuwa ni Jenifer Lemunge ambaye ni Katibu wa CCM tawi la Amana, Katibu Kata wa CCM Ilala, Devotha Bantulaki na Frank Joseph, ambaye ni Katibu wa hamasa wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam.

Akisoma hati ya mashtaka yanayowakabili washtakiwa hao, Mwendesha Mashtaka Chimwenda alidai kuwa viongozi hao kwa pamoja katika maeneo tofauti ya Wilaya ya Ilala waliomba rushwa ya Sh. milioni tano na kupokea Sh. milioni tatu kwa mmoja wa wafanyabiashara kwa ajili ya kupanga katika moja ya kiwanja cha CCM kata ya Ilala tawi la Amana.

Mwendesha Mashtaka huyo alidai kuwa washtakiwa hao walikamatwa Machi 22, mwaka huu na kufunguliwa mashtaka kwa makosa ya kuomba na kupokea rushwa maeneo ya Klabu ya Wazee, Amana.

Baada ya kusikiliza mashtaka ya kesi hiyo, hakimu anayesikiliza kesi hiyo alisema dhamana kwa washtakiwa hao iko wazi na kila mmoja anapaswa kuwa na bondi ya Sh. milioni tano.

Washtakiwa hao walikana mashtaka hayo na wako nje kwa dhamana.

**Imeandikwa na Romana Mallya na Mary Geofrey**

# Mdhamini Lissu atamani kujitoa

**Na Hellen Mwango**

MDHAMINI Robart Katunda wa Mbunge wa Singida Mashariki kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amedai mahakamani anatamani kujitoa kwa sababu hana mawasiliano wala taarifa za mbunge huyo.

Kadhalika amedai kwamba Lissu hana ushirikiano naye kama mdhamini wake katika kesi ya uchochezi inayomkabili na wenzake watatu.

Madai hayo aliyatoa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Patrick Mwita, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa.

"Sina la kusema mshtakiwa hana ushirikiano, hatuna taarifa zake kama wadhamini, ningetamani nijitoe udhamini dhidi ya Lissu," alidai mdhamini Katunda.

Hakimu alisema mdhamini hawezi kujitoa wakati mshtakiwa hayupo mahakamani.

Mwita alidai kuwa maneno ya mdhamini yana upa mashaka upande wa Jamhuri.

"Tunaomba atuletee mshtakiwa wetu kwanza ndipo atangaze kujitoa," alidai Mwita.

Mdhamini wa pili, Ibrahim Ahmed, alidai kuwa hajafanikiwa kupata namba za simu za Lissu anazotumia huko nchini Ubelgiji na kwamba amekwenda kutoa taarifa na kuijulisha mahakama anaendelea kufuatilia.

Hakimu Simba alisema amesikiliza hoja za Jamhuri na zile za wadhamini, kumbukumbu za mahakama yake zipo kimya na inataka kujua taarifa za mshtakiwa huyo.

"Kesi imekwama, tunataka kuendelea kupata taarifa za mshtakiwa huyo, mdhamini huwezi kujitoa mpaka umlete mshtakiwa mahakamani," alisema Hakimu Simba.

Alisema dhamana ya washtakiwa wengine inaendelea na kesi itatajwa Aprili 25, mwaka huu.

Mbali na Lissu washtakiwa wengine ni, Wahariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na Mchapishaji wa Kampuni ya Jamana, Ismail Mehbooh.

Kwa pamoja washtakiwa hao, wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume na Sheria ya Magazeti ya mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016, jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari kisemacho,

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA



Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob (kushoto), akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Speshoz Tanzania, Jeffrey Jessey wakati wakikagua moja ya cherehani kumi zilizotolewa msaada na meya huyo kwa ajili ya vikundi viwili vya kinamama wa manispaa yake jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi, Cecilia Martin. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Madalali wayanawa mahekalu ya Lugumi

**Na Romana Mallya**

MCHAKATO wa kuuza mahekalu ya mfanyabiashara maarufu nchini, Said Lugumi, warejeshwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) baada ya kampuni ya udalali ya Yono iliyopewa zabuni hiyo kushindwa kuziuza.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Yono, Scholastica Kevela, akizungumza na Nipashe jana, alisema kuwa suala hilo wamelirejesha TRA ili wafanye mchakato wa kutafuta zabuni.

"Suala la uuzaji wa nyumba za Lugumi tumelirejesha TRA ambao wanafanya mchakato wa kutafuta zabuni, ni vizuri ukawauliza wao ili kujua nini kinaendelea," Kevela alisema.

Gazeti hili lilipomtafuta Mkurugenzi wa Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi TRA, Richard Kayombo, alikiri kuwa mchakato huo umerudi kwao.

"Ni kweli mchakato wa uuzaji wa nyumba za Lugumi umerudi kwetu kuhusu nini kinaendelea, kwa sababu nyumba zipo serikalini yaani zipo mikononi mwetu tutaamua tutakapokuwa tayari lini ziuzwe," alisema.

Kayombo alisema wanaweza kuamua kuziuza kidogo kidogo ama zote kwa pamoja.

"Siyo lazima tuziuze zote kwa wakati mmoja, tunaweza kuziuza kidogo kidogo, ila lini tutafanya hivyo...tutakapokuwa tayari," Kayombo alisema.

Nyumba hizo zilianza kunadiwa Septemba 9, mwaka juzi ambapo kampuni ya Yono ilifanikiwa kuuza nyumba moja ya Upanga kwa Sh. milioni 700 ambayo hata hivyo, Serikali haikuridhika na bei hiyo na kuamua kufanya tathmini upya ili iuzwe tena.

Novemba 9, mnada mwingine ulifanyika ndipo Dk. Louis Shika maarufu '900 itapendeza', alijipatia umaarufu baada ya kushinda zabuni ya kununua nyumba hizo kwa Sh. bilioni 3.3 na kushindwa kuzilipia kama masharti ya mnada yalivyotaka.

Nyumba zinazopigwa mnada ni tatu ambazo kati ya hizo, moja ni hiyo ya Upanga na mbili zilizopo Mbweni jijini Dar es Salaam.

Siku ya kwanza ya mnada huo uliofanyia Novemba 9, Mkurugenzi wa Kampuni ya Yono, Kevela, alianza kunadi nyumba hizo kama ilivyo kawaida ya mnada na Dk. Shika akiwa miongoni mwa wateja wanaowania kuzinunua.

Wakati wateja wengine wakipanda bei ya kununua nyumba hizo, Dk. Shika naye alikuwa akipanda bei na kuwaacha wanunuzi wenzake kwa mbali, hali iliyowafanya wafanyakazi wa Yono kumpepea na kumshangilia.

Mnada ulipokuwa ukiendelea, mnunuzi mmoja alitaja Sh. milioni 700 na kupanda hadi milioni 750, Dk. Shika alitaja (800), mwingine alipotaja milioni 810, Dk. Shika

INAENDELEA UK 8

# Serikali yashtukia ajira wageni hoteli za kitalii

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema kuna haja ya kufanya tathmini ya mfumo wa elimu unaotumika nchini, kufuatia nafasi za juu katika hoteli nyingi za kitalii nchini kushikwa na raia wa kigeni na wazawa wakibaki kushika nafasi za chini.

Uamuzi huo unakuja baada ya ukaguzi wa hoteli hizo ilizozibinafsisha kwa wawekezaji kufanyika na kubainika kuwa nafasi zote za maamuzi zinaongozwa na wafanyakazi wa kigeni hususan za nafasi za umeneja.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema hayo baada ya kufanya ukaguzi katika hoteli tano za kitalii na mbili kati ya hizo zilizopo ndani ya hifadhi nchini.

Katika hoteli hizo imebainika kuwa zote zinaongozwa na mameneja wa kigeni ambao hawawezi kuzungumza lugha ya Kiswahili.

Kanyasu alisema kama taifa kuna haja ya kujiuliza kuwa hatuna wataalamu wa kushika nafasi hizo au mfumo wa elimu ni mbovu.

Hata hivyo, Kanyasu alisema mfumo wetu wa elimu sio mbovu kiasi hicho kushindwa kuandaa mameneja katika hoteli hizo.

Alisema kwa sasa kuna wasomi wengi wa masomo hayo, lakini wapo mtaani wakiwa hawana kazi.

"Tatizo langu si kwa sababu nafasi hizo zimeshikwa na wageni ila, je, kwa nini kila hoteli meneja wake ni wa kigeni?" Alihoji Kanyasu.

Alisema mtindo wa hizo hoteli wa kutumia mameneja wa kigeni ni mkakati maalum ulioratibiwa wa kuficha taarifa muhimu hususan taarifa za kodi.

Alieleza kuwa utaratibu huo unawadumaza wazawa na kujikuta hawajui

INAENDELEA UK 8

# Mimba, utoro vyakatisha ndoto wasichana 4,090

**Na Rose Jacob, MWANZA**

ZAIDI ya wanafunzi wa kike 4,000 wameshindwa kumaliza elimu ya msingi na sekondari kutokana na vifo, utoro, ujauzito na magonjwa ya kudumu kwa kipindi cha miaka minne iliyopita mkoani Mwanza.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) Mwanza, halmashauri za Buchosa wilayani Sengerema na Misungwi zinaongoza kwa kuwa vinara kwa tatizo hilo katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Michael Rigola, katika taarifa yake kwenye kikao hicho, alisema mbali na vifo vya wanafunzi 99 vilivyotokea kwa kipindi hicho, magonjwa ya kudumu, utoro na mimba kwa wasichana wa shule za msingi na sekondari ni sababu kubwa zilizofanya kuwapo kwa idadi hiyo kubwa.

Alisema wasichana 2,646 wameshindwa kumaliza shule za msingi katika Halmashauri za Buchosa iliyoko wilayani Sengerema inayoongoza kwa wasichana wengi kutomaliza shule, ikifuatiwa na Ilemela, Kwimba, Magu, Misungwi, Mwanza Jiji, Sengerema na Ukerewe. Ligora alisema kwa shule za msingi, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi inaongoza kwa kuwa na wasichana 586 ambao kati yao watoro 517, waliopata ujauzito 15, magonjwa ya kudumu 28 na vifo 26 sawa na Buchosa yenye watoro 513, ujauzito 12, magonjwa ya kudumu 42 na vifo 19.

Alisema Magu ina wanafunzi 440 watoro wakiwa 400, waliopata ujauzito 19, magonjwa ya kudumu 19 na vifo sita, huku Jiji la Mwanza ikiwa na wasichana 425, kati yao watoro wakiwa 421, mimba tatu na kifo kimoja.

Halmashauri ya Ilemela, kwa mujibu wa Ligora, ilikuwa na wasichana 325, watoro wakiwa 305, mimba saba, vifo 12, huku mmoja akishindwa kumaliza kutokana na ugonjwa wa kudumu. Sengerema inafuatia kwa kuwa wasichana 250 wakiwamo watoro 181, mimba 31, magonjwa ya kudumu 21 na vifo 17.

Ukerewe inashika namba ya saba kwa kuwa na wasichana 19 walioacha shule ambao kati yao 14 hawakumaliza kutokana na vifo na mimba za utotoni tano ikifuatiwa na Kwimba yenye wasichana 15 na vifo vinne.




NAS DAR AIRCO YASIFIA MIPANGO YA TANZANIA KATIKA SEKTA YA AJIRA

NAS DAR AIRCO inatambua juhudi za Serikali ya Tanzania katika kuendeleza kuimarisha ujuzi na utaalamu kwa wazawa walioajiriwa.

NAS ina furaha kuchangia katika mipango hii kwa:-

- Kuajiri watanzania zaidi ya asilimia 99 ya waajiriwa wake wote
- Kuhamisha utaalamu na teknolojia zake za kimataifa kwa wafanyakazi wake wazawa na katika shughuli zake
- Kushukuru na kusaidia jamii (CSR programu), kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kutoa udhamini kwa wanafunzi wa elimu ya juu, masomo ya kiufundi, pamoja na utoaji wa nafasi za kazi kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo
- Kutoa nafasi za kujishikiza kwa muda kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa vijana wa Kitanzania wenye ari ya utoaji huduma kwenye usafiri wa anga na kuwapa ajira ya kudumu wale watakaofanya vizuri zaidi

Kwa mwaka 2018, NAS DAR AIRCO ilihudumia ndege **7,000** pamoja na mizigo ya abiria **467,000** na mizigo mingine yote yenye jumla ya tani **700** na zaidi. Abiria **515,000** kutoka katika viwanja vya ndege Dar es Salaam, Kilimanjaro na Dodoma. Kampuni inatoa huduma kwa **Air Tanzania, Fly Dubai, Ethiopian Airlines, RwandaAir** na **Air France - KLM** kuanzia hivi karibuni. NAS DAR AIRCO imewekeza zaidi ya dola za Kimarekani **$10,000,000** hapa Tanzania tokea mwaka 2016.

nas | airco

www.nas.aero

115137202

## FATMA KARUME:

# Nilikwazika kutopewa nafasi Siku ya Sheria (2)

**Na Enock Charles**

KATIKA sehemu ya kwanza ya mahojiano haya jana, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Fatma Karume, alieleza alivyokwazika kutokana na kutopewa nafasi ya kuzungumza katika maadhimisho ya Siku ya Sheria mwaka huu.

Fatma pia alizungumzia tukio la kushambuliwa kwa rais wa zamani wa TLS na Mwanasheria Mkuu wa Chadema, Tundu Lissu.

Katika sehemu ya pili, mtaalamu huyo wa sheria anazungumzia mustakabali wa sheria nchini na picha ya maisha yake. Endelea...

***SWALI: Agizo la Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi la wanasiasa wanaoendelea kufanya vikao vya ndani kuchunguzwa ili kuwabaini wanaotukana limeonekana kuibua hisia tofauti. Agizo hilo kisheria TLS mnalitazamaje?***

***FATMA:*** Kuna kitu kwenye Katiba kinaitwa uhuru wa kujumuika. Pia kuna uhuru wa mawazo, kuna haki ya faragha na kushirikiana.

Sasa, Kangi Lugola (Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi) anataka mpaka kwenye kushirikiana apeleke polisi, siasa ni ushirika, sasa yeye uhuru wote huo tuliokuwa nao anataka aukandamize kwa kupeleka polisi.

Utafikiri vyama vya siasa vikikutana, vinataka kumzungumza na Rais tu. Kwa hiyo, haki yao ya kuwa na faragha, ya uhuru wa kujumuika inachukuliwa wanatafuta sababu ya 'ku-spy on this people' (kupeleleza watu).

***SWALI: Kwa wasiomfahamu Fatma Karume, ni mtu wa aina gani hasa?***

***FATMA:*** 'I am still finding myself, Ha ha haah! Every day I am still finding myself' (bado najitafakari nilikosimamia). Unajua hayo yote kuitwa mwanaharakati au mpigania haki za binadamu, yanakuja ukiwa na upendo, compassionate (rehema au huruma), una shukrani.

Unashukuru kile unachojaaliwa na upo tayari kujitolea na una 'spirit' (ari) ya kujitolea kusaidia wenzako, 'so' (kwa hiyo), ukiwa na vyote hivyo, huna budi, utakuwa mwanaharakati. Utapambania haki za wenzako, lakini muhimu ukiniuliza kwamba mimi nataka niwe mtu wa aina gani, 'my aim is for peace'.

'Peace in my heart and I know this peace I have to help people to be compassionate, without that, huwezi kuwa na peaceful heart. Kwa hiyo, bado najaribu kuwa hivyo.

***SWALI: Bibi yako aliitwa Fatma Karume. Je, hii ndiyo siri ya wewe kuitwa Fatma Karume?***

***FATMA"*** Mimi nilikuwa mtoto wa kwanza, tena mtoto wa kwanza wa kike na pia bibi yangu mzaa mama anaitwa Fatma na bibi yangu mzaa baba anaitwa Fatma. Kwa hiyo, 'in English I got a lot about this' kwa sababu huwezi kuwa mtoto wa kwanza wa kike halafu pande zote mbili bibi anaitwa Fatma.

Mimi ilikuwa lazima niitwe Fatma tu kwa pande zote. Nilikuwa mtoto wa kwanza na bibi zangu hao kina Fatma.

***SWALI. Wewe ni Rais wa TLS, kiongozi wa IMMMA Advocate na pia mama wa familia, unaugawaje muda wako kuzitumikia pande zote hizo?***

***FATMA:*** 'I could manage' kuna muda nakuwa na familia natengeneza vikapu, ha ha ha! Natengeneza blankets si vya kuuza lakini, ha ha ha!

Unajua nilianza kutengeneza vikapu vya nyumbani kwangu mwenyewe 'and then' nikawaita watoto wa kike wawili nikawafundisha kutengeneza, nikawalipa halafu nikaanza pia kutengeneza blankets.

'I am always looking for anything to do' (mara zote natafuta cha kufanya) na huwa na 'na-enjoy' (nafurahia) kufanya hivyo na sipendi kukaa bila ya kufanya kitu, siwezi nikae nikatazama TV tu.

***SWALI: Umekuwa wakili kwa muda mrefu na sasa kiongozi wa juu wa TLS. Bila shaka umepata uzoefu mkubwa katika uongozi. Je, una mpango wa kugombea Urais wa Tanzania au Zanzibar?***

***FATMA:*** 'There is a price to pay' (kuna gharama za kulipa) kwa mtu kuwa maarufu, watu wanapenda umaarufu, lakini hawajui 'costs' (gharama) zake.

Siamini kwamba unaweza kuwa kiongozi kwa sababu kwamba baba yako alikuwa kiongozi. Urais ni kitu lazima 'uwa-convince' (uwashawishi) watu na umaarufu wa baba yako haufai kitu.

'So I don't think (kwa hiyo sifikiri) pia kuwa umaarufu peke yake unatosha kumfanya mtu kuwa rais. Uongozi ni kitu 'very complicated' (kigumu sana), umaarufu hautoshi. Sina mpango wa kugombea urais na mimi si mwanachama wa chama chochote cha siasa.

***SWALI: Gharama zipi unaingia kwa kuwa maarufu?***

***FATMA:*** 'Lack of privace' (kupungua kwa ufaragha), 'imagine' (fikiria) unakwenda mahali kila mtu anakujua, watu hawajui, lakini wao wanakujua. 'Sometimes' (wakati mwingine) unataka kwenda mahali 'just to do your business, it's a burden' (kwa shughuli zako, inakuwa mzigo).




***SWALI: Huoni kwamba umaarufu unakusaidia kuwakilisha hisia za watu mbalimbali?***

***FATMA:*** 'I am an opinion leader not because of famous but because what I think also most of the Tanzanian think. I am reflecting others and I am not different from other Tanzanians. (Ninaongoza mitazamo si kwa sababu ya umaarufu, lakini kwa sababu ninachokiwaza ndicho Watanzania wengi mawazo yao yako hapo. Ninawaakisi wengine na siko tofauti na Watanzania).

There are people looking at me and say 'ha mtoto wa Karume' but she is thinking in the way we are also thinking and I think it's because people know that I am not CCM, not Chadema, not ACT Wazalendo or any other political party. (Kuna watu wananitazama na kunikebehi 'ha mtoto wa Karume' lakini anafikiri katika namna ambayo nasi tunafikiri. Na ninadhani, ni kwa sababu tu mimi si mwanaCCM, Chadema, ACT Wazalendo au chama kingine chochote cha kisiasa).

Ukiwa huru, unakuwa 'confident' (unajiamini) kwa kuwa huna 'political affiliation' (hujajiegemeza kokote kisiasa). 'So I have no political ambitions' (sina utashi wa kisiasa), sitaki ubunge, sitaki uwaziri, sitaki cheo chochote cha kisiasa 'but I will say what I think is right' (lakini nitasema kile ambacho naona ni sahihi) na hiyo 'ina-create trust' (inajenga uaminifu) kwa wananchi.



## HABARI KITAIFA

# Harufu ya ufisadi yashtua wabunge

**Restuta Damian, BUKOBA**

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imebaini ubadhirifu wa zaidi ya shilingi bilioni 1.4 kutokana na kutumika kinyume cha taratibu na sheria ya fedha katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, hivyo kutoa maagizo matano.

Kamati hiyo ilitoa maagizo hayo baada ya kutembelea na kukagua miradi mitatu ambayo wajumbe waliitilia shaka utekelezaji wake. Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilikuwa imeitilia shaka na kubainisha upungufu mkubwa katika taarifa yake.

Kamati iligundua kuwa asilimia 90 ya miradi iliyotekelezwa mwaka wa fedha 2015/16, 2016/17 na 2017/18, ilitekelezwa chini ya kiwango ukiwamo udhaifu mkubwa wa kamati ya fedha ya halmashauri hiyo. Wajumbe pia walibaini udhaifu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo na kutokana na sababu hizo mbili, kamati hiyo chini ya mwenyekiti wake, Vedasto Ngombale Mwilu, iliagiza mambo kadhaa.

Iliagiza kufuatiliwa kwa mradi wa ujenzi wa madarasa na ukarabati wa miundombinu ya Shule ya Sekondari Rwazi, huku jukumu hilo likielekezwa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera.

Kadhalika ofisi hiyo iliagizwa kuhakikisha ujenzi na ukarabati unakamilika kabla ya Mei 30, 2019 na taarifa ya utekelezaji wa mradi huo ifike ofisi ya CAG na LAAC Juni Mosi, mwaka huu.

Katika agizo lake la pili LAAC iliielekeza Ofisi ya CAG kufanya ukaguzi maalum kwenye halmashauri hiyo. Ukaguzi huo pia utahusisha mwaka wa fedha 2015/16, 2016/17 na 2017/18 na taarifa hiyo ikikamilika iwasilishwe mapema iwezekanavyo kwa mwenyekiti wa kamati hiyo.

Wakati CAG akiendelea na ukaguzi Ofisa Masuhuli na Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba wanatakiwa kuchukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wote waliohusika na ubadhirifu wa fedha za serikali katika miradi hiyo, likiwa ni agizo la tatu.

Agizo la nne, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikishirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba, Limbe Moris, washirikiane kubaini mkandarasi aliyepewa zabuni ya kutekeleza miradi minne, ambaye hajulikani na hajitokezi kudai madai ya fedha zake za utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, ofisi hizo mbili zimeelekezwa zimpate mkandarasi huyo kupitia vyombo kadhaa kama Brela au vyombo vya ulinzi na usalama.

Agizo lingine ni kuhusu nafasi za wakuu wa idara wanaokaimu, ambapo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-(TAMISEMI) na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wahakikishe nafasi zote zinazokaimiwa, wanaokaimu wawe na sifa na kama hawana sifa, wapelekwe wakuu wa idara katika nafasi hizo.

Kamati pia ilitembelea mradi wa barabara ya kilometa tano za lami ngumu uliofadhiliwa na Benki ya Dunia wenye thamani ya shilingi bilioni 7. Zabuni ya mradi huo alipewa mkandarasi NCL wa jijini Dar es Salaam na ulitakiwa kuanza Juni 19, 2018 na kukamilika Aprili 18, 2019. Hata hivyo, baada ya mkandarasi kuanza kazi aliutelekeza kabla haujakamilika na Halmashauri ya Manispaa hiyo ilikuwa imemlipa shilingi bilioni 1.4, hivyo magari yake kumakatwa.

Miradi mingine miwili iliyotembelewa na kamati ni wa ujenzi na ukarabati wa Shule ya Sekondari Rwazi na barabara ya lami nyepesi ya Kashai aliyopewa mkandarasi Nikara wa jijini Dar es Salaam. Hata hivyo, miradi hiyo haikukamilika na imebainika kuwa na upungufu mwingi, huku wataalamu wa Halmashauri ya Manispaa wakisema mkandarasi huyo ameshindwa kupatikana.

# Vituo vya ufugaji mbioni

**Na Idda Mushi, MPWAPWA**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala wake wa Vyuo vya Mifugo nchini (LITA), kwa mara ya kwanza wanatarajia kuanzisha vituo atamizi kwa ajili ya ufugaji katika kampasi zake nane nchini, ili kuwawezesha wanaosoma katika vyuo hivyo kujifunza kivitendo kufuga kisasa, kibiashara na kwa faida na kujiandaa kujiajiri baada ya kuhitimu.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa LITA, Dk. Kejeri Gillah, alisema hayo wakati akizungumza na wakuu wa vyuo hivyo na watendaji mbalimbali wa wakala huo waliokutana katika kampasi ya Mpwapwa mkoani Dodoma kwenye mkutano wa Baraza Kuu la Wafanyakazi.

Dk. Gillah alisema tayari Sh. milioni 150, zimetengwa kwa ajili ya kuanzia uanzishwaji wa vituo hivyo na wadau mbalimbali wa maendeleo wameonyesha nia kusaidia mpango huo unaokusudia kuleta tija kuwa ya utoaji wa mafunzo katika vyuo hivyo na kuwawezesha vijana kujiajiri.

Aidha, alisema wakala huo unakusudia kutumia Sh. bilioni 4.5 kwa ajili ya kuboresha huduma mbalimbali wanazotoa katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 ikiwamo kuboresha mafunzo wanayotoa, shughuli za uzalishaji mali pamoja na mafunzo na utafiti.

Aidha, alisema wakala huo kwa mara ya kwanza unakusudia kuanza kutoa gawio la asilimia 15 ya mapato yake ghafi kwa serikali kwa awamu, sawa na zaidi ya Sh. milioni 344 kama alivyoagiza Rais Dk. John Magufuli akitaka wakala na taasisi za serikali kutoa gawio la mapato yake ili kutekeleza matakwa ya serikali.

Alihimiza wafanyakazi wa wakala huo kufanya kazi kwa bidii, maarifa, uadilifu na uaminifu ili kufanikisha malengo mbalimbali waliyojiwekea ya kuboresha utoaji wa huduma.

Akizungumzia matarajio ya uanzishwaji wa vituo atamizi, Mkuu wa Kampasi ya LITA ya chuo cha Mifugo Mpwapwa, Moses Mlahagwa, alisema wazo la uanzishwaji huo lilianzia ngazi za chini baada ya kuona mahitaji, na kushukuru menejimenti ya LITA kufanyia kazi mawazo hayo na rais kuridhia utekelezaji wake.

Akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu katika wizara hiyo, Zakariyya Kyera, alipongeza hatua ya wakala huo kwa mara ya kwanza kukusudia kutenga asilimia 15 ya mapato yake ghafi ili kutoa gawio kwa serikali.

"Lengo la serikali kuanzisha wakala huu ni kupunguza utegemezi serikalini, thaminini na kuheshimu kazi zenu na muwe wabunifu kufikia mafanikio, muundo wa LITA umekamilika, tunaendelea na jitihada za kujaza nafasi zilizo wazi ili kukidhi mahitaji ya serikali," alisisitiza.


## BONITE BOTTLERS LIMITED

### Advertisements of Employment

**1. Area Sales Supervisor**

**Qualification:**

- Applicant should be a holder of Bachelor of Commerce in Marketing / Business Administration or any other related field from recognized Institution.

**Key Skills & Abilities:**

- Ability to manage and monitor staff performance to ensure the preset targets are met
- Ability to actively pursue opportunities to improve Route to Market and leveraging best practices.
- Ability to drive horizontal expansion through outlet creation incentive programs
- Ability to identify Commercial and Market development improvement initiatives to drive incremental volume, and profit share.
- Ability to track performance against objectives regularly and initiate corrective measures.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated, flexible person and a good team player

- **Experience** : Any experience in related field will be added advantage.
- **Location** : Arusha & Kilimanjaro

**2. Salesman**

**Qualification:**

- Applicant should be a holder of form IV/VI with Diploma in Sales and Marketing / Business Administration or any related field from recognized Institution.

**Key skills & Abilities:**

- Skills and knowledge of customer care and customer services.
- Ability to forecast sales/load to be taken for each day to the location assigned.
- Able to work independently with minimum supervision.
- Self motivated, flexible person and a good team player.
- Ability to seek out and develop new business and maximize all possible opportunities to increase Sales

- **Experience : Any experience in the same field will be added advantage**
- **Location : Arusha & Kilimanjaro**

**Mode of Application:**
All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to undersigned address, reach him not later than 28/03/2019.

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI.**
**E- mail hr@bbl.co.tz**

215135602



Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

## Call for Proposals from Consultants

### Transforming Tanzania's Charcoal Sector Project

With Financial Support from the Swiss Agency for Development and Cooperation, the Tanzania Forest Conservation Group in partnership with the Tanzanian Community Forest Conservation Network (MJUMITA), and the Tanzania Traditional Energy and Development Organisation (TaTEDO) are implementing the project 'Transforming Tanzania's Charcoal Sector'.The project goal is a pro-poor and climate resilient transformation of the economics and governance of charcoal and other forest product value chains. TFCG is seeking consultants for the following three assignments:

**1. Development of a sustainability plan and gender strategy for the Transforming Tanzania's Charcoal Sector project.**

The objectives of the consultancy are: to develop a project sustainability plan, including a clear exit strategy for the project; and to conduct a gender analysis of the sustainable charcoal and timber production models.

**2. Communicating the impact of the TTCS project through case studies and photographs.**

The objectives of the consultancy are: to communicate the impact of the TTCS project on people's lives in the project villages through a series of compelling accounts of individuals' engagement with the project's interventions; and to provide a portfolio of high-quality photographs of project-related activities and landscapes.

**3. Agricultural component evaluation and partnership development.**

The objectives of the consultancy are: to evaluate the impact of the TTCS training programme for farmers on climate-smart, small-scale agriculture, agroforestry and value addition; and to facilitate the development of a strategic, formalised partnership between TFCG and an NGO whose core business is capacity building for small-scale farmers.

**Details on how to apply and the terms of reference for each consultancy are available at: http://www.tfcg.org/tenders.html**

215137002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BUSARA

**TUPONGEZE PANAPO PONGEZEKA**

**KUMPONGEZA MTU NI KUMPA SIFA KWA KAZI NJEMA ALIYOIFANYA. KIMSINGI MTU HAPONGEZWI KWA KUTENDA MABAYA BALI HULAANIWA. HATA HIVYO TUSIWE WACHOYO WA KUPONGEZA PALE PANAPOSTAHILI KUPONGEZA. KUPONGEZA NI KUTOA MOTISHA NA MWELEKEO WA DIRA NJEMA.** NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI

# Mamlaka udhibiti wa vyakula zikaze kamba

**TAARIFA** za kukamatwa kwa nyama mbovu ambayo haifai kwa matumizi ya binadamu ni tishio kwa usalama wa wananchi.

Aidha, taarifa hizo zinaibua shaka kuhusiana na suala zima la usalama wa vyakula pamoja na vitoweo kwa afya za wananchi.

Tunayazungumzia haya kutokana na kuripotiwa habari kwamba serikali imeteketeza shehena ya nyama mbovu za ng'ombe na nguruwe zenye viambata vya sumu zisizofaa kwa matumizi ya binadamu na zilizokwisha muda wa matumizi tani nane zilizoingizwa nchini kwa njia za panya na kuhatarisha afya za wananchi.

Pia nyama hizo zimekamatwa zikiuzwa katika maduka makubwa (Supermarkets) mbalimbali, licha ya kutofaa kwa matumizi ya binadamu pia zimeingia nchini bila vibali, kulipiwa ushuru wa serikali na wala kuhakikiwa ubora wake, huku nyingine zikiwa hazina nembo wala taarifa yoyote katika vifungashio.

Akizungumza wakati akishuhudia uteketezaji wa nyama hizo Njiro jijini Arusha, mwishoni mwa wiki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema kukamatwa kwa bidhaa hizo ni sehemu ya matokeo ya operesheni Nzagamba iliyowezesha kukamatwa na kuteketezwa kilo 26,295 za nyama mbovu na maziwa zilizokuwa zimeingia nchini kinyume cha sheria.

Msisitizo wetu kuhusiana na shaka ya usalama wa vyakula vinavyoliwa na watu wengi nchini unatokana na tabia ya wafanyabiashara ya vyakula kupenda kupata faida kuliko kujali afya za watu. Tamaa yao inawafanya watangulize faida kutokana na kufahamu kuwa vyakula ni bidhaa muhimu ambayo hakuna mtu anayeweza kuepuka kuinunua, vinginevyo hawezi kuishi.

Umuhimu wa chakula ndiyo sababu ambayo inapaswa kuzifanya mamlaka zetu za udhibiti wa vyakula kuwa makini katika kusimamia biashara ya vyakula kuanzia ununuzi, usafirishaji wake, upishi na matumizi.

Kwa upande wa vyama ambayo mara kadhaa imekuwa ikigundulika kutokuwa salama, tunaona kwamba kuna haja ya mamlaka hizo zikiwamo TFDA, TBS pamoja na maofisa wa afya na mifugo kukaza kamba wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yao, vinginevyo wakifanya kinyume chake, afya za wananchi wengi zitaathirika.

Mwanya ambao wafanyabiashara ya nyama wamekuwa wakiutumia kuuza bidhaa hizo mbovu ni walaji wengi kupenda kitoweo cha gharama ndogo, ambayo ni rahisi kuimudu.

Kuna hatua kadhaa ambazo zinaweza kuchukuliwa kukabiliana na hali hiyo, lakini hatua muhimu na ya msingi ni udhibiti mkali ambao hautaonea haya wala huruma yeyote ambaye ataenda kinyume cha sheria na taratibu za uuzaji wa nyama.

Ni jukumu la kila mwananchi kuzingatia kanuni za afya ambazo zinaeleza na kusisitiza ulaji wa vyakula ambavyo vinethibitishwa ubora wake na mamlaka za serikali, hivyo kama ni nyama lazima iwe imefanyiwa ukaguzi na kuidhinishwa na wataalamu wa afya. Bila hivyo, kuna athari nyingi, yakiwamo magonjwa sugu ambayo pia yanaweza kusababisha vifo.


Pamoja na kuongeza udhibiti, ipo pia haja ya kuangaliwa kwa sheria zetu ili kuzipa makali zaidi kwa ajili ya kuwabana na kuwashughulikia watu wote wanaouza nyama isiyofaa kwa matumizi ya binadamu.

Chini ya sheria mpya adhabu ya faini kubwa inaweza kutumika pamoja na kifungo ili liwe fundisho kwa wote ambao wanachezea maisha ya binadamu kwa kuuza nyama zisizofaa.

Tunaamini serikali itasimamia kauli yake kupitia Mpina kwa wafanyabiashara kutambua kuwa iko macho wakati wote na imejipanga kudhibiti uhalifu huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



# Mwarobaini wa ajali barabarani huu hapa

Na Sabato Kasika

**TANGU** pikipiki maarufu kama bodaboda kuanza kutumika kama vyombo vya usafiri mwaka 2008, kumekuwapo ajali nyingi zinazopoteza maisha, pia kusababisha ulemavu wa kudumu kwa baadhi ya Watanzania.

Zipo sababu zinazotajwa kuwa chanzo cha ajali hizo, ikiwamo kukosa umakini barabarani, kutozingatiwa kwa misingi ya usalama barabarani kutokana na baadhi ya madereva kukosa mafunzo ya msingi ya uendeshaji vyombo vya moto.

Sababu nyingine ninayoiona, ni dharau waliyo nayo baadhi ya waendesha 'bodaboda', ambayo inawezekana ndio inayosababisha wasitii sheria za usalama barabarani na kuendesha wanavyotaka.

Mfano mdogo ni kwamba, hawatakiwi kupakia abiria zaidi ya mmoja, pia wanaelekezwa kuvaa kofia ngumu (helmet). Lakini, baadhi yao hawazingatii hilo na wanaendelea kubeba abiria hadi watatu kwa mkupuo.

Mtindo wa ubebaji huo umepewa jina la mishikaki, lakini wamekuwa wakisema kwamba unasaidia kuwafanya wapate pesa nyingi, kuliko kupakia abiria mmoja.

Nawashauri ndugu zangu, jambo la msingi wanalopaswa kulifanya, ni kutii sheria bila shuruti, kwani zimewekwa kwa usalama wao na abiria.

Pia, wasilazimishe kwenda kinyume. Kila dereva ana wajibu wa kuheshimu matumizi sahihi ya barabara.

Novemba mwaka jana, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, alipokuwa bungeni, alisema tangu usafiri wa bodaboda na bajaj kuanza kutumika kama vyombo vya usafiri mwaka 2008, hadi kufikia Septemba 2018 vilisababisha jumla ya ajali 38,237

Mhandisi Masauni anasema katika ajali hizo jumla ya watu 8,237 walipoteza maisha kutokana na ajali za bodaboda, huku wengine 37,521wakiwa wamepoteza viungo vyao hali inayowapa ulemavu wa kudumu.

Serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha madereva wanazingatia sheria za usalama barabarani, ikiwa ni pamoja na kuwapa semina na kuwahimiza kwenda vyuoni kusomea kazi hiyo, ili waifanye kwa weledi.

Mamlakla hiyo ya dola, imekuwa pia ikibuni mbinu za kukabiliana na vyanzo mbalimbali vya ajali hizo, ikiwamo kupiga marufuku ufungaji pombe kali katika viroba na kuuzwa bei nafuu, kwa vile vinachangia kuwapo kwa ajili za 'bodaboda'.

Ingawa serikali imepiga marufuku, wauzaji na wanywaji wakiwamo madereva wa 'bodaboda', wamebuni mbinu nyingine ya kuwafanya waendelee kupata pombe hiyo kwa bei nafuu.

Mbinu hiyo ni kuuza pombe hiyo kali katika vipimo vidogo vinavyouzwa kuanzia Sh.300, hali inayoweza kukwamisha juhudi zinazofanywa na serikali za kupunguza ajali zinazotokana na ulevi.

Dereva anapokuwa anaendesha chombo cha moto akiwa amelewa, ni wazi kwamba hawezi kuwa makini barabara na anaweza kuendesha mwendo ambao ni hatari kwake na kwa abiria wake.

Hivyo ikiwezekana, ufike wakati sasa pikipiki zipunguzwe, zisiwe mwendo mkali unaoweza kumfanya dereva ashindwe kuumudu awapo barabarani.

Januari mwaka huu, Jeshi la Polisi lilitoa ripoti kuimarika utekelezaji wa sheria na kampeni za kudhibiti uhalifu, kumesaidia kupunguza ajali za barabarani kwa asilimia 33.8 mwaka jana.

Taarifa hiyo ya jeshi inasesma, katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2018, kulitokea matukio 3,978 ya ajali za barabarani, ikilinganisha na matukio 6,022 yaliyotokea mwaka ulitangulia wa 2017.

Msemaji wa jeshi hilo, Ahmed Msangi, anasema hiyo ina maana kwamba ajali zimepungua kwa asilimia 33.8 au upungufu wa ajali 2,034 na anawataka wananchi na watumiaji wa vyombo vya moto vya usafiri kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuwahakikishia usalama wao.

Kimsingi, ajali zinaongeza huzuni katika jamii na kupunguza mengi, nguvukazi ya taifa na kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi. Hivyo ni muhimu kila Mtanzania akazingatia sheria anapokuwa barabarani, ili kuepuka ajali hizo.

Ninasema hivyo kwasababu ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya ajali za barabarani ya mwaka 2017 inaonyesha kuwa watu milioni 1.25 hufariki kwa ajali kila mwaka huku wengine milioni 20 hadi milioni 50 wakibaki na majeraha na ulemavu wa kudumu wa aina mbalimbali.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, nusu ya wanaokufa kwa ajali za barabarani zinazotokea duniani kote ni watembea kwa miguu, madereva wa 'bodaboda' wa magari na kuathiri asilimia tatu ya pato la ndani la taifa kila mwaka.

## TANGAZO




**SHIRIKA LA UMEME (TANESCO) TANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

## HALI YA UPATIKANAJI WA UMEME KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM NA ZANZIBAR

**Machi 25, 2019**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linawataarifu Wateja wake wa Mkoa wa Dar es salaam na Zanzibar kuwa matengenezo kinga ya mashine namba 3 ya Kituo cha Ubungo II yanaendelea pamoja na uwekaji wa transfoma kubwa la MVA 300 kwenye Kituo cha kupoza umeme cha Ubungo ili kukiongezea uwezo na kwenda sambamba na ukuaji wa mahitaji ya jiji la Dar es Salaam.

Aidha, Kampuni ya Songas inaendelea na matengenezo kinga katika mashine yake namba 3 yanayotarajiwa kukamilika Aprili 09, 2019.

Kutokana na matengenezo hayo Mikoa ya TANESCO ya Dar es Salaam ambayo ni Kinondoni Kaskazini, Kinondoni Kusini, Temeke na Ilala pamoja na Zanzibar zitakuwa na upungufu wa umeme na hivyo kuathiri maeneo hayo kwa nyakati tofauti.

Tunatarajia matengenezo haya yanayokwenda kwa awamu yatakamilika ifikapo mwezi Juni 2019.

TANESCO itaendelea kutoa taarifa ya Maendeleo ya kazi ya matengenezo ya kituo cha Ubungo yenye lengo la kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa Dar es Salaam na Zanzibar kwa siku zijazo.

**Kituo cha miito ya simu 2194400 na 0768 985100**
**Tovuti: www.tanesco.co.tz,**
**Mitandao ya kijamii**
**Twitter, www.twitter.com/tanescoyetu,**
**Facebook https://www.facebook.com/tanescoyetultd/**

**IMETOLEWA NA:**

**OFISI YA UHUSIANO**
**TANESCO MAKAO MAKUU**

215137902

# Serikali yashtukia ajira wageni

INATOKA UK 3

chochote kuhusu uendeshaji wa hoteli hizo.

Alisema mwanzo ilidaiwa kuwa nafasi hizo haziwezi kushikwa na wazawa kwa vile hawajui kuongea vizuri Kiingereza, lakini kwa sasa wapo wanaojua kuzungumza na kuandika Kiingereza vizuri hata kuwazidi baadhi ya hao mameneja wa kigeni.

Aidha, alisema nafasi hizo za juu zinazoshikwa na wageni sio za kitaalamu kiasi cha kufanya zikishikwa na wazawa utendaji utasimama. Alisema wazawa wamekuwa wakifanya kazi za chini kwa malipo kiduchu ikilinganishwa na wageni.

Katika hatua nyingine, Kanyasu alishauri wamiliki wa hoteli hizo kupunguza bei kipindi cha msimu wa watalii wachache ili kuwawezesha watalii wa ndani kumudu gharama hizo badala ya kuzifunga hoteli hizo katika msimu huo.

Pia, alishauri wamiliki wa hoteli kutofautisha bei za malipo ya hoteli kwa watalii wa ndani na watalii wa nje ili kukuza utalii wa ndani.

Kwa upande wake, Meneja wa Lobo, Asram Anuary, alisema suala hilo la kushusha bei kwa watalii wa ndani kipindi cha watalii wachache wa kutoka nje ni wazo zuri, hivyo watashauriana na menejimenti ili waweze kuona uwezekano huo.



Wanafunzi wakipita pembezoni mwa Barabara ya Kigogo, jijini Dar es Salaam jana, huku wakiwa wamebeba mbao kwa ajili ya matumizi shuleni. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**


THE EMBASSY OF THE UNITED STATES OF AMERICA

Sources Sought Notice

The United States Agency for International Development (USAID)/Tanzania seeks a local partner to implement the Local Institutions Leading Development (LILED) activity. The purpose of the activity is to strengthen performance management in the public sector. Grants and grant management assistance will be provided to Local Government Authorities (LGAs) and the Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MoHCDEC).

This call is exclusively for local Tanzanian partners, defined as organizations which: • are incorporated or legally organized under the laws of, and have its principal place of business in Tanzania; • are at least 75% beneficially owned by individuals who are citizens or lawfully admitted residents of Tanzania; • have at least 75% of its staff (senior, mid-level, support) being citizens or lawfully admitted residents of Tanzania; and • if it has a Board of Directors, has at least 51% of the members of its Board who are citizens or lawfully admitted permanent residents of Tanzania.

Grant management entails soliciting, screening, and selecting grantees against published criteria, and managing the resulting grants. It also involves ensuring that the grantee has the necessary organizational capacity (i.e. systems, policies, practices) to implement the grant in accordance with best practices, and that the grantee is technically, financially, and administratively equipped to achieve the stated objectives of the grant. The LILED Recipient(s) will account for funds given to 50-150 LGAs each year and for funds provided to the MoHCDEC for performance-based financing of health facilities. As recipients of sub-grants, LGAs and the MoHCDGEC will implement these sub-grants using GOT systems and in accordance with GOT policies and procedures.

To respond to this notice, submit a document not to exceed 5 pages (inclusive of annexes) that describes:

1. Your organization's experience in providing capacity building support to government entities engaged in health activities.
2. Your organization's experience with performance-based financing.
3. Your organization's experience in managing donor funded grants.

Email your document to **usaidtzco@usaid.gov** with subject **"LILED - Sources Sought Notice"** which should be received not later than **Tuesday, April 02, 2019.**

215137702


## Madalali wayanawa mahekalu ya Lugumi

INATOKA UK3

ndipo alipotaja neno ambalo lilibeba umaarufu wake '900 itapendeza'.

Picha kadhaa za kwenye mitandao zikionyesha wafanyakazi hao wakimpepea kwa vitambaa na vitu vya aina mbalimbali, Dk. Shika wakiamini kuwa yeye ndiye mteja aliyeshinda wenzake na kutwaa nyumba hizo.

Lakini alipotakiwa kutoa asilimia 25 ya malipo ya awali kama masharti ya mnada yanavyotaka, hakuwa na fedha hizo huku akidai kuwa ziko nje ya nchi, ndipo alipokamatwa na Jeshi la Polisi.

"Tatizo ni kutoelewana, nyumba zinauzwa na wametaka asilimia 25 zilipwe hapo hapo na mimi fedha zangu zipo nje, hapo ndipo tuliposhindwana," alisema Dk. Shika.

Aidha, kutokana na kitendo hicho ambacho kilikwenda kinyume cha taratibu za mnada, Jeshi la Polisi lilimkamata, kumuhoji na kumweka maabusu kwa siku sita na baadaye alitimiza masharti ya dhamana ya kujidhamini mwenyewe.

Baada ya mnada huo kuvunjika siku hiyo, ulifanyika mwingine wa tatu Novemba 24, lakini licha ya wanunuzi kujitokeza, hawakuweza kufikia kiwango kilichopangwa.

## Mdhamini Lissu

INATOKA UK 2

'Machafuko yaja Zanzibar.'

Katika shtaka la pili wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016, walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar.

Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13, 2016, katika jengo la Jamana lililopo Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

## Maswali magumu ya JPM mapato

INATOKA UK 2

vizuri kama kina (Filbert) Bayi? Why (kwanini)? Kwanini timu zetu za ngumi zilipokuwa zinakwenda nje zilikuwa zinahusika katika kashfa za dawa za kulevya? Why (kwanini)?" Rais Magufuli alihoji.

**ATOA ZAWADI**

Kwa kushinda 3-0 dhidi ya Uganda juzi na kufuzu kushiriki fainali za Afcon mwaka huu, Rais Magufuli aliwapa zawadi ya viwanja katika Jiji la Dodoma wachezaji wa Taifa Stars na bondia Mwakinyo aliyeshinda pambano lake jijini Nairobi hivi karibuni.

"Nimeamua kuwapa zawadi ndogo kwa niaba ya Watanzania, na zawadi yenyewe ni viwanja katika Mkoa wa Dodoma. Wachezaji wote wa Taifa Stars, bondia Hassan pamoja na mwalimu wako, Tino na Tenga," Rais Magufuli alisema na kuongeza:

"Kama tuliweza kuwapa mabalozi viwanja, kwanini tushindwe kuwapa mabalozi wetu hawa walioliletea sifa taifa letu? Waziri Mkuu usimamie upatikanaji wa viwanja vyao, tena ikiwezekana viwe sehemu moja, utamwelekeza Mkurugenzi wa Jiji awasiliane na Katibu Mkuu Ikulu kusimamia suala hili."

Rais Magufuli aliahidi serikali itatoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kusaidia maandalizi ya Timu ya Taifa ya Vijana wenye umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys).

"Najua kuna fedha zimetolewa na CAF (Shirikisho la Soka la Afrika), lakini sisi kama serikali tutatoa shilingi bilioni moja zikasaidie katika maandalizi," Rais Magufuli alisema huku akieleza kuchukizwa na kipigo cha bao 1-0 ambacho Taifa Stars ilikipata ugenini dhidi ya Lesotho Novemba 18, mwaka jana.

"Baada ya matokeo yale, niliahidi kutoita timu yoyote Ikulu, baada ya kutandikwa kule Lesotho na mlikula milioni zangu 50, mchezo ule uliniboa sana, kwa sababu niliuangalia wakati mnacheza, wachezaji wengine wazuri hawakupangwa kwenye nafasi zao, nikawa najiuliza huyu aliyepanga timu alipanga kwa makusudi au kulikuwa na nini?

"Tangu siku hiyo sijawahi kumpigia Mwakyembe hadi leo. Amekuwa akiandika 'message' sijamjibu, kuna siku aliwahi kuniandikia inasema 'tuanzishe mashindano tuite Magufuli Cup kama Kagame cup', sikumjibu.

"Sijawahi kuzungumza na Naibu Waziri tangu siku hiyo, iliniuma sana kwa sababu inaumiza sana kwa nchi kama Tanzania yenye idadi ya watu milioni 55 inafungwa na timu yenye idadi ya watu milioni mbili," Rais Magufuli alisema.

Rais Magufuli pia alitoa zawadi ya shilingi milioni tano kwa Tino kutambua mchango wake kwa Taifa Stars ya mwaka 1980 iliyofuzu kwa mara ya kwanza kuingia fainali za Afcon.

Tino ndiye aliyefunga goli lililoiwezesha Tanzania kuingia fainali hizo na tangu mwaka huo haikuwahi kufanikiwa tena kuingia hatua hiyo mpaka juzi ikiwa ni miaka 39 imepita.

HABARI KITAIFA

# Sababu za mabaraza ya ardhi kushindwa majukumu yake hizi

**Na Boniface Gideon, TANGA**

KUKOSEKANA elimu kwa wajumbe wengi waliopo kwenye mabaraza ya ardhi na nyumba ngazi ya kata kumeelezwa kuchangia kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa na kusababisha migogoro kwa wananchi na manung'uniko.

Hayo yalisemwa juzi na Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga, Doris Wilson, wakati wa warsha ya kuwajengea uelewa viongozi wa ngazi mbalimbali juu ya ufahamu wa sheria na kufuata taratibu na kutoa maamuzi sahihi ili kutatua migogoro ulioandaliwa na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) Mkoa wa Tanga.

Alisema elimu hiyo itakuwa chachu kwa wajumbe hao kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwenye mabaraza hayo, lengo kubwa likiwa ni kuhakikisha wanatenda haki kwa wananchi ambao wanakabiliwa na migogoro mbalimbali kwenye maeneo yao.

"Changamoto kubwa ya mabaraza ya kata ni elimu, wajumbe wengi hawajapata elimu kuhusu mabaraza hayo, muundo, namna ya utendaji, akidi katika kuendesha na utaratibu wa kuendesha mashauri, hivyo tunaamini kupitia elimu hii inaweza kuleta mabadiliko makubwa kwenye utekelezaji wa shughuli zenu," alisema mwenyekiti huyo.

"Lakini pia tunaishukuru TAWLA kwa kuwa wanapotoa mafunzo ya namna hii wanawapa wajumbe uelewa kuhusu namna ya kuendesha mashauri hayo, kwa kufanya hivyo haki kwa wananchi inaweza kutendeka na kuondoa manung'uniko," alisema.

Aidha, alisema mikakati waliyonayo hivi sasa ni kuhakikisha wanatoa elimu kwa mabaraza ya ngazi ya kata ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi mkubwa katika kutoa haki wanapopelekewa malalamiko kutoka kwa wananchi.

Awali akizungumza wakati wa mafunzo hayo Mratibu wa TAWLA Mkoa wa Tanga, Latifa Ayoub, alisema lengo la warsha hiyo ni kutoa elimu kwa ngazi mbalimbali kwa viongozi wa mabaraza, wenyeviti na wajumbe ili waweze kujua sheria na kufuata taratibu na kutoa maamuzi sahihi wakati wakitatua migogoro.

Alisema warsha hiyo imehusisha wajumbe, makatibu na wenyeviti wa mabaraza ya ardhi kutoka kwenye kata za Magila na Kilulu kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufahamu sheria za ardhi na kutoa maamuzi sahihi kwa wananchi.

Hata hivyo alisema watajaribu kuangalia jinsi gani ya kushirikiana kupunguza changamoto hizo yakiwamo mashauri mengi yaliopo kwenye baraza hilo, hali itakayowezesha kuondosha migogoro kwa wananchi.



Watoto wakitimua mbio kuvuka barabara katika eneo la Malambamawili, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## SAHIHISHO

Katika toleo letu la jana ukurasa huu tuliripoti habari yenye kichwa cha habari "Meneja Tanroads kortini tuhuma kupokea rushwa" usahihi ni kwamba aliyefikishwa kortini ni mtumishi wa mizani na sio meneja kama ilivyodaiwa mahakamani. Pole kwa usumbufu wowote uliojitokeza kwa wahusika.

**Mhariri**

# Bilioni 2.4/- kuwapa majisafi wananchi vijijini

**Na Jumbe Ismailly, IRAMBA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida, inatarajia kutumia zaidi ya shilingi bilioni 2.4 kuchimba visima katika vijiji kumi na kukamilisha miundombinu ya visima hivyo, ili wananchi wanufaike na huduma ya majisafi na salama.

Mhandisi wa Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Athumani Mkalimoto, aliyasema hayo alipokuwa akijibu swali la Diwani wa Mtoa, Samuel Tyuma, aliyetaka kufahamu serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi huduma ya majisafi na salama kwenye vijiji kumi ambavyo fedha zimeshapatikana.

Mhandisi huyo alivitaja visima vilivyochimbwa kwa mwaka 2018/2019 ni Tintigulu, Kitusha, Kisana, Masagi, Kyalosangi, Mgundu, Ulemo, Kizega, Wembere na Ngalangala na kwamba kati ya visima hivyo Kitusha na Kisana maji hayakupatikana.

Kwa mujibu wa Mkalimoto, bajeti ya kwanza ni ya uchimbaji visima na utekelezaji wake upo chini ya wakala wa serikali na baada ya hapo wameweka mpango wa bajeti mwaka 2019/2020 ndipo utekelezaji wake utakapokamilika.

Katika swali lake la msingi, Diwani Tyuma alitaka kufahamu sababu zilizochangia kisima kilichochimbwa katika Kijiji cha Masagi tangu Novemba, mwaka jana, lakini hakijaanza kutoa huduma kwa wananchi wa kijiji hicho.

# Wabunge waipa 5 TARI kwa utafiti

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imeipongeza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kwa kufanya utafiti wenye tija na unaolenga kumbadilisha mkulima wa kawaida ili aweze kupiga hatua kimaendeleo katika kilimo na maisha yake.

Kamati hiyo imesema kuwa ili kuwezesha wakulima na wafanyabiashara wa Tanzania kuchangamkia fursa ya kilimo cha muhogo, kwa kuwa Mei, 2018, ulisainiwa mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China kuruhusu bidhaa za muhogo mkavu kutoka Tanzania kuingia katika soko la China.

Akizungumza mbele ya watumishi wa kituo cha utafiti TARI kilichopo Kibaha mkoani Pwani, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, alikipongeza kituo hicho kilicho chini ya Wizara ya Kilimo, huku akizitaka taasisi zote za utafiti nchini kutangaza kazi wanazozifanya.

"Kamati inazitaka taasisi zote za utafiti wa kilimo nchini kuhakikisha inatangaza kwenye vyombo vya habari na kwingineko utafiti wao wote ili kulinda kazi kubwa na nzuri wanazozifanya maana kukaa kimya kunafifisha juhudi za kazi zao," alisisitiza.

Dk. Ishengoma alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa ya kilimo hususani kilimo cha muhogo ambacho kimeonyesha kuwa na tija kubwa, pia ameviitaka vituo vya utafiti wa kilimo viwawezeshe wakulima kupata mbegu bora na mbinu za kisasa ili waongeze uzalishaji na kukidhi mahitaji ya soko hilo.

Katika hatua nyingine, mwenyekiti huyo aliihakikishia Wizara ya kilimo kuwa itapitisha bajeti yote inayohusisha masuala ya utafiti ili kuongeza tija na ufanisi katika kazi ya utafiti.

Alisema sio jambo jepesi kuendeleza kilimo pasi na kuwa na utafiti bora, hivyo kamati inatambua umuhimu wa utafiti nchini na kwa maana hiyo imeridhia kushirikiana na taasisi hizo za utafiti ili kuwanufaisha wakulima.

Kwa upande wake Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alikiri sekta ya kilimo haiwezi kuendelea bila kufanya utafiti kuanzia ngazi ya awali ya kilimo kwa kufanyika utafiti wa udongo, mbegu, mbolea na viuatilifu.

Alisema Wizara ya kilimo ina mpango wa kupeleka maazimio ya kuwa na sheria ya kulinda utafiti mbalimbali unaogunduliwa nchini. Kadhalika, Waziri Hasunga, aliungana na kamati hiyo kuitaka TARI kutangaza kazi zake inazozigundua ili zifahamike kuliko kuzifungia ofisini. Vilevile amewataka watafiti katika vituo vyote vya utafiti kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa umoja, kutokuwa wabinafsi na kushirikishana kazi zao kwa kuwa kufanya kazi kwa ubinafsi kunarudisha nyuma juhudi za maendeleo ya kilimo.

# Madawati yaokoa 65 kuanza masomo

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI 65 wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari ya Kata ya Kibinda Chalinze mkoani Pwani, wanatarajia kujiunga na masomo baada ya kukaa nyumbani kwa zaidi ya miezi mitatu kutokana na ukosefu wa madawati.

Kutokana na uhaba huo, Benki ya NMB imejitosa kutatua tatizo hilo na kutoa msaada wa madawati na viti vyenye thamani ya Sh. 5,000,000.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa hivyo shuleni hapo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi Benki ya NMB, Omaru Mtiga, alisema kuwa benki hiyo imetoa msaada wa madawati 60 na viti 30 ikiwa sehemu ya kurejesha faida kwa jamii.

Mtiga alisema wametoa msaada huo kufuatia kupokea maombi ya kusaidia kuchangia vifaa hivyo ili wanafunzi hao waweze kujiunga na wenzao baada ya kukaa nyumbani kwa zaidi ya miezi mitatu kwa madawati na viti.

"Benki ya NMB ina utaratibu wake wa kurejesha faida kwa jamii na tukio hili la kutoa msaada wa madawati 60 na viti 30 kwa Shule ya Sekondari Kibinda ni sehemu ya kurejesha faida kwa jamii kwa kuwa tumekuwa tukichangia katika sekta ya elimu, afya na majanga yanayojitokeza nchini," alisema Mtiga.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kibinda, Halmashauri ya Chalinze Mkoa wa Pwani, Jevelson Kamugisha, alisema kuwa shule hiyo katika mwaka wa masomo 2019, ilipangiwa wanafunzi 125 wa kujiunga na Sekondari ya Kata Kibinda.

Kamugisha alisema kuwa ni wanafunzi 60 pekee waliofanikiwa kujiunga na kidato cha kwanza na wengine 65 walilazimika kukaa nyumbani kutokana na kukosa madawati na viti.

"Ni jambo la kuishukuru NMB kwa kusikia kilio chetu na jana wametukabidhi madawati 60 na viti 30 ambavyo kwa sasa wanafunzi walioshindwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaanza masomo kesho," alisema Kamugisha.

Alisema kuwa baada ya kupokea taarifa kutoka benki ya NMB tawi la Turiani kuwa mchakato wa maombi ya kupatiwa madawati na viti umekubaliwa, uongozi wa shule ulianza taratibu za kuwaandikia barua za wito wazazi na walezi ili kuwapeleka shule watoto Machi 24, kwa ajili ya kujiunga na masomo.

**"Ni jambo la kuishukuru NMB kwa kusikia kilio chetu na jana wametukabidhi madawati 60 na viti 30 ambavyo kwa sasa wanafunzi walioshindwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaanza masomo kesho," alisema Kamugisha.**

# Kigoma kupata umeme wa uhakika mwakani

**Na Mwandishi Wetu**

MKOA wa Kigoma utaanza kupata umeme wa gridi kuanzia mwezi Aprili mwakani, hali itakayoufanya mkoa huo kupata umeme wa uhakika na serikali kuokoa fedha zinazotumika kununua mafuta ya kuendeshea mitambo ya umeme.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati wa ziara yake ya kukagua usambazaji umeme vijijini katika Wilaya ya Kakonko na Kibondo mkoani Kigoma na kuwasha umeme katika Kijiji cha Kewe na Rugunga.

"Serikali imeshaanza taratibu za ujenzi kutoka Desemba mwaka jana na njia hiyo ya umeme ya msongo wa KV 132 itajengwa kutokea Tabora kupitia Urambo, kwenda Nguruka mpaka Kidawe wilayani Kigoma," alisema Dk. Kalemani.

Alisema mradi huo wa ujenzi wa njia ya umeme ambao utagharimu Sh. bilioni 84 utahusisha pia ujenzi wa vituo vitatu vya kupoza umeme.

Kuhusu hali ya usambazaji umeme mkoani Kigoma, Dk. Kalemani, alisema jumla ya vijiji 149 vitapelekewa umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme wa awamu ya tatu mzunguko wa kwanza.

Alisema ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo wa usambazaji umeme mkoani Kigoma, serikali imeweka makandarasi wawili wanaosambaza umeme vijijini ambao ni Urban & Rural na CCCE-Intern. Aidha, alimwagiza mkandarasi wa umeme katika Wilaya ya Kibondo na Kakonko (Urban & Rural) kuhakikisha anamaliza kazi ya usambazaji umeme katika vijiji vya wilaya hizo ifikapo mwezi Juni, mwaka huu.

Kwa nyakati tofauti, wananchi katika vijiji vya Kewe na Rugunga, waliishukuru serikali kwa kuwapelekea nishati ya umeme kwa Sh. 27,000 tu ambayo pia imefika katika Taasisi za Umma kama zahanati na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.



Ofisa Mauzo wa Benki ya NBC, Dunstan Lipawaga (kushoto), akimkabidhi kadi ya ATM aina ya Visa mkazi wa Mtwara, Ismail Sama, baada ya kufungua akaunti ya Fasta wakati wa kampeni ya Shika Ndinga katika Uwanja wa Shule ya Msingi Majengo mkoani humo juzi. NBC inadhamini kampeni hiyo kwa malengo ya kusogeza huduma za kibenki karibu na wateja wao, wateja wanafungua akaunti ya Fasta na kupata kadi ya ATM ya Visa hapo hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali watakiwa kuuza bidhaa nje ya nchi

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewataka wazalishaji wenye bidhaa zilizokidhi matakwa ya viwango na kukabidhiwa leseni za kutumia alama ya ubora, kuhakikisha wanatumia fursa hiyo kupanua masoko yao ikiwa ni pamoja na kuuza bidhaa zao nje ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TBS, Prof. Makenya Maboko, kwenye maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika (ARSO), yaliyofanyika Makao Makuu ya Shirika hilo Ubungo, jijini Dar es Salaam.

Maadhimisho hayo yaliyoenda na utoaji leseni za kutumia alama za ubora kwa wazalishaji ambao bidhaa zao zimekidhi matakwa ya viwango.

Prof. Maboko alisema alama ya ubora ni muhimu sana katika biashara kwa kuwa inampa mzalishaji uhakika kuhusu ubora na usalama wa bidhaa yake, hivyo kumjengea imani kwa walaji.

"Lakini pia alama ya ubora humsaidia mzalishaji kupanua masoko ya bidhaa zake nje ya nchi na ni wazi basi hatua hii ni ya kujivunia sana kama mzalishaji na kama taifa kupanuka kwa masoko ya kikanda na kimataifa kutasaidia kuongeza fedha za kigeni, hivyo kusaidia kukuza uchumi," alisema.

Alifafanua kuwa hali hiyo itasaidia kufikiwa kwa azima ya taifa ya kujenga uchumi wa kati unaotegemea uzalishaji wa viwandani ifikapo mwaka 2025.

Aliwataka wazalishaji waliopatiwa leseni hizo kuzingatia masharti yake na kuwa waadilifu katika uzalishaji wao, ili kuhakikisha wanaendelea kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango wakati wote.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuinua uchumi wa taifa na wazalishaji binafsi wakati wote.

Kuhusu jitihada zinazofanywa na Rais John Magufuli katika kupambana na rushwa nchini, Prof. Maboko alisema wadau wa viwango ni fursa muhimu ya kuhakikisha wanatoa mchango wao kwa kueneza uelewa na weledi unaotumika katika kuandaa viwango.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, alisema maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika ni muhimu kwa kuwa wanapata fursa ya kuwakumbusha wazalishaji, watoa huduma na wananchi wote kuhusu umuhimu wa kuzingatia viwango vya ubora katika maisha yao ya kila siku.

Kwa mujibu wa Dk. Ngenya, kaulimbiu ya maadhimisho hayo ya saba ya Siku ya Viwango Afrika ni; "Nafasi ya viwango katika kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa kwa mabadiliko endelevu ya Afrika."

Alisema kwa Tanzania serikali imejipambanua katika suala la vita dhidi ya rushwa, hivyo na wao katika tasnia ya viwango wanayo fursa ya kuonyesha njia katika kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa.

# Serikali yaahidi kutatua changamoto huduma ya shufaa

**Na Mwandishi wetu,** ARUSHA

SERIKALI imesema itaanza kutatua changamoto zinazoikabili huduma ya shufaa nchini zikiwamo za uhaba wa dawa na kupanda kwa bei zake kuanzia mwaka ujao wa fedha.

Huduma shufaa ni mbinu ya kuboresha maisha ya mgonjwa anayekabiliwa na maradhi yanayotishia uhai ili umauti umkute kwa heshima anayostahili binadamu mwingine yoyote.

Akizungumza jijini hapa, Mkemia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi, alisema tangu huduma hiyo ianze kupatikana Tanzania takribani miongo miwili iliyopita, huduma hiyo imekuwa ikipatikana katika vituo vichache vya afya vinavyomilikiwa na sekta binafsi hususan vya madhehebu ya dini.

Wadau wa huduma shufaa kutoka Tanzania na Uganda walikutana jijini Arusha hivi karibuni katika kikao kazi cha siku mbili ambacho, pamoja na mambo mengine, kilijadili umuhimu wa kusambaza huduma hiyo katika mfumo mzima wa afya nchini Tanzania.

Idara ya Afya ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) iliandaa kikao kazi hicho kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Washiriki walikuwa wafamasia kutoka hospitali za rufani za mikoa, waratibu wa miradi 24 ya huduma shufaa, wakiwamo madktari na manesi na maofisa kutoka wizara mama nchini Tanzania na Uganda.

Msasi alikihakikishia kikao kazi hicho kuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) itatoa vibali kwa hospitali zote za rufani za mikoa nchini ili kuanzia mwakani zitoe huduma shufaa.

Alisema serikali itajenga uwezo wa vituo vitano vya kanda vya kubadilisha dawa ya morphine kutoka unga kuwa kimiminika ifikapo mwakani ili kupunguza adha ya maofisa wa vituo vinavyotoa huduma shufaa na wagonjwa kusafiri umbali mrefu kufuata dawa hiyo muhimu.

Alitoa mfano wa ofisa wa kituo cha huduma shufaa wa wilayani Kyela, Mkoa wa Mbeya, ambaye hutumia Sh. 500,000 kufuata dawa ya morphine kimiminika jijini Dar es Salaam.

Morphine ni dawa ya kulevya inayotumika kisayansi kupunguza maumivu makali kwa wagonjwa wa maradhi yanayotishia uhai ili waweze kuendelea na maisha yao ya kila siku.

Tanzania na Uganda zimeridhia azimio la Umoja wa Mataifa lijulikanalo Single Convention on Narcotic Drugs la 1961 linalopiga vita usafirishaji na matumizi mabaya ya dawa za kulevya duniani.

# Wenye viwanda waomba bidhaa za nje ziongezwe kodi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAMILIKI wa viwanda jijini Arusha wameiomba serikali kuondoa msamaha wa kodi na kuongeza tozo katika bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, kwa ajili ya kuvilinda viwanda vya ndani na bidhaa zinazozalishwa nchini.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu kwa niaba ya wamiliki wa viwanda jijini Arusha, Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Lodhia Group, Sailesh Pandit, alisema kuna haja kwa serikali kubadilisha sheria za ulipaji kwa kufuta misamaha ya tozo na kuongeza kodi kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Alishauri kwa bidhaa za chuma zinazoingizwa kutoka nje ya nchi wanatakiwa kulipa kodi ya serikali kwa asilimia 35 na viwanda vya ndani vipunguziwe kodi ili kuongeza ari ya uzalishaji kwa wingi ambapo itasaidia kuthaminisha bidhaa za ndani na viwanda vyake.

"Wamiliki wa viwanda vya chuma wanahali ngumu kutokana na baadhi ya sheria za nchi zilizopo katika ukanda wa SADC, bidhaa zinazotoka ndani ya nchi husika hazipewi kipaumbele kama zinazotoka nje ya nchi hizo, hivyo tunaiomba serikali yetu kukaa chini na wamiliki wa viwanda ili kufahamu changamoto zinazowakabili ikiwamo ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchi kukosa soko.

"Wafanyabiashara wanaogopa kuwekeza kutokana na bidhaa za ndani kulipiwa kodi kubwa kuliko zinazotoka nje ya nchi, pamoja na bidhaa hizo kutokuthaminiwa katika soko la ndani," alisema.


Aliongeza viwanda vilivyopo hapa nchini, vinatosheleza mahitaji ya wananchi, lakini bidhaa kutoka nje ya nchi zinaingizwa kwa asilimia 70, hivyo, inasababisha viwanda vya ndani kukosa mwelekeo wa kibiashara.

Akitolea mfano katika kiwanda chake cha chuma, awali alikuwa akizalisha tani 100 ya bidhaa kwa siku, lakini baada ya kuyumba kwa soko la ndani uzalishaji umeshuka hadi kufikia 30.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema dhamira ya serikali kufikia uchumi wa kati na wa viwanda inawezekana kwa asilimia 100, endapo serikali itatoa fursa na vipaumbele kwa viwanda na bidhaa zinazozalishwa hapa nchi.

"Kwa upande wangu nimeunga mkongo mpango wa serikali wa kufikia uchumi wa kati na viwanda, ukiangalia katika viwanda vyangu nimeajiri wafanyakazi zaidi ya 1,400, pia kwa mwaka nalipa kodi ya serikali zaidi ya Sh. milioni 30, huu ni mwanzo mzuri na kama wafanyabiashara wengine wakiendelea na moyo huo, kwa kweli tutafikia malengo ya nchi.

"Njia pekee ya kulinda bidhaa za ndani na soko lake ni serikali kufanya mabadiliko ya kodi kwa kupunguza kwenye bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kuondoa msamaha wa tozo zote kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi, ukiangalia hapa nchini tuna viwanda vya chuma zaidi ya 14, ambavyo vikitumika vizuri vinaweza kuitangaza nchi kimataifa," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula, akifungua semina ya siku mbili ya wadau wa madini iliyoandaliwa na Tume ya Madini na kufanyika Mji Mdogo wa Mirerani jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanafunzi 269 wabainika uoni hafifu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANAFUNZI 269 kutoka shule za msingi Moivaro na Arusha zilizoko mjini hapa wana matatizo ya uoni hafifu.

Hayo yamebainishwa na wataalamu wa masuala ya utambuzi wa uoni hafifu kwa watoto kutoka nchini Norway kwa kushirikiana na Chuo cha Elimu Maalum Patandi walipokuwa wakifanya zoezi la upimaji mwishoni mwa wiki.


Akizungumzia juu ya mradi huo, Mwalimu Lucas Kivuyo, alisema kumekuwapo na mabadiliko makubwa baada ya kufanya uchunguzi kwa wanafunzi wa shule hizo mbili na kubainika kuwapo kwa changamoto hiyo ya uoni hafifu kwa wanafunzi hao.

Naye Mkufunzi na Mwalimu wa Chuo cha Elimu Maalumu Patandi, Stamford Chalamaganza, alisema changamoto iliyopo ni uwepo wa wanafunzi hao kutofanya vizuri darasani kutokana na uwepo wa uoni hafifu jambo ambalo alitaka Wizara ya Elimu kuwatambua zaidi walimu na kuongeza wigo katika kuwafikia wanafunzi nchi nzima.

"Endapo walimu hao watafikiwa na elimu, kutasaidia kuwabaini wanafunzi hao wenye tatizo hilo kwa kuwa idadi kubwa ya walimu hawana taaluma ya kuwabaini wanafunzi wenye changamoto hiyo darasani," alisema.

Naye Ofisa Elimu Mkuu anayeshughulikia Idara ya Elimu Kitengo cha Elimu Maalum kutoka Ofisi ya Rais (Tamisemi), Julius Migeha, alisema bado kuna tatizo kubwa la uwepo wa wanafunzi wenye tatizo la uoni hafifu, hivyo kulingana na taratibu zilizopo katika Idara ya Elimu mikakati iliyopo ni walimu wapatiwe elimu zaidi ili waweze kuwasaidia wanafunzi.

Hata hivyo kutokana na ushirikiano uliopo kati ya Chuo Kikuu cha nchini Norway na Chuo cha Ualimu Patandi Elimu Maalumu, wamekuwa wakitoa jitihada katika kuwabaini wanafunzi wenye changamoto hiyo, ambapo Profesa Gunvor Wilhemsen kutoka Norway alisema shauku yao ni kufikia shule zote za msingi ili kuondoa matatizo kwa wanafunzi na kuwawezesha kusoma vizuri bila changamoto za uoni hafifu.





# Wananchi wanyonge sasa wasaidiwa masuala kisheria

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WATOA huduma ya msaada wa kisheria katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro wamesema wananchi wanyonge zaidi ya asilimia 40 wamesaidiwa katika kutekeleza mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Msaidizi wa kisheria wa Kijiji cha Wiri kilichopo Kata ya Gararagua, Hamza Munisi, alisema kutokana na matukio mengi yaliyowahi kujitokeza ya watu kudhulumiwa haki zao, hasa wanawake wanaponyang'anywa mali wanapofiwa na waume zao, wanasheria hao wamekuwa mkombozi mkubwa wa kuwasaidia na hatimaye kurudishiwa haki zao.

"Umuhimu wetu katika Wilaya ya Siha, ulianza kuonekana na kuungwa mkono na viongozi wa mbalimbali katika serikali, pale tulipomwokoa mwanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari Magadini, aliyekuwa amefaulu kujiunga na kidato cha tano sekondari ya Oshara ambaye aliozeshwa na wazazi wake baada ya matokeo ya mitihani kutangazwa. Leo mwanafunzi yule yuko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam," alisema Hamza.

Zaidi alisisitiza: "Kuna mwitikio mzuri na hali ilivyo hasa huko vijiji ni kwamba wananchi wengi wasio na uwezo wanakimbilia kwa wasaidizi wa kisheria kupata tafsiri kuhusu malalamiko yao kama yanapaswa kwenda polisi au mahakamani."

Alisema pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na wasaidizi hao wa kisheria, mwitikio wa wananchi kutumia wasaidizi wa kisheria wanapopata matatizo unatia matumaini, ingawa bado kuna watu wanaowadharau kwa kuwaona kama watu wasiokuwa na kazi ya maana.

"Kiukweli tunafarijika sasa maana viongozi wa serikali ngazi ya vijiji na kata na hata wilaya, Mkuu wa Wilaya yetu Mheshimiwa Onesmo Buswelu, hivi sasa wanatupa ushirikiano na tunafanya nao mikutano ya pamoja na tumeshatengeneza mpango wetu tumeupa jina la 'chain' na tunakwenda wote wakati mwingine kutatua matatizo ya wananchi," alieleza.

Mmoja wa wakazi wa Kata ya Gararagua, Winfida Mashauri, ambaye ni miongoni mwa wanufaika wa msaada wa wasaidizi hao wa kisheria, alisema baadhi ya wananchi wanaokabiliwa na matatizo hushindwa kujitokeza kwa kuona aibu au kuogopa kuonekana wabaya kwenye jamii pale mtu aliyetenda kosa anapohukumiwa kwenda jela.

Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma wa Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 na Kanuni zake za Mwaka 2018, ushauri wa msaada wa kisheria maana yake ni ushauri na msaada unaotolewa kwa mtu asiye na uwezo katika mashauri ya jinai na madai kuhusu sheria husika, taratibu za kisheria na uandaaji wa nyaraka za kisheria.

Kazi ya kuwanoa wasaidizi hao wa kisheria katika Mkoa wa Kilimanjaro, imekuwa ikitekelezwa na Shirika la Kwieco kwa ufadhili wa Shirika la Legal Service Facility (LSF).

Wakati wasaidizi wa kisheria wakianza kufurahia mwitikio wa huduma hiyo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alipotembelea Mkoa wa Kilimanjaro kuona shughuli hizo alisema serikali inaona ukatili wa kijinsia ni tatizo kubwa na ambalo ndio malaria mpya, ukimwi mpya na ujambazi mpya katika taifa.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa (kushoto), akifafanua jambo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Mizani kinachojengwa Dakawa mkoani Morogoro, wakati kamati hiyo ilipokagua mzani huo. **PICHA: WUUM**

# Mwekezaji atangaza neema kwa wakulima

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

KAMPUNI ya Ideal Health Care and Chemicals E.A (IHC) ya Moshi inayojiandaa kuwekeza kwenye kiwanda cha kutengeneza sukari mbadala inayotokana na mazao mapya ya mimea ya stevia, rebaudiana, utupa na chia seed, imetangaza neema kwa wakulima wanaotaka kufanya kilimo cha mkataba.

Akizungumza jana na viongozi wa dini, wanasiasa, wafanyabiashara na wataalamu wa sekta ya afya Mkoa wa Kilimanjaro, Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Dk. John Kabugi, alisema kilimo hicho cha mkataba wataingia makubaliano na wakulima watakaojitokeza kuchangamkia fursa hiyo.

"Wanahitajika wakulima wa mazao hayo na mazao mengine kama mchicha. Tumeanza kwa kuwahamasisha wakulima kuchangamkia fursa ya kilimo cha mazao mapya ya biashara ambayo yanahitajiwa na kampuni hiyo kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema.

Zao la stevia reubaudiana ni zao linalotokea kwenye nchi za Paraguay, Brazil na Amerika ya Kusini ambalo majani yake yanatumika kutengeneza sukari ambayo ni rafiki kwa watu wenye ugonjwa wa kisukari.

Taarifa ya kampuni hiyo ya IHC, inaeleza zaidi kuwa zao la stevia ni zao linalotumika katika mataifa ya kigeni kwa ajili ya tiba kwa watu wenye shinikizo la damu (BP), kisukari na matatizo ya mifupa.

"Tunatarajia kwamba zao hili litakuwa linaingiza kipato cha Dola za Marekani milioni 10 hadi milioni tano kwa wakulima kwenye kipindi cha miaka mitano ya kwanza kwa Mkoa wa Kilimanjaro. Na zao la tephrosia vogelii (Utupa) au 'Fish Poison' ni zao ambalo linatumika shambani kuua wadudu, panya na fuko na ukiotesha viumbe hao hawatakaribia katika shamba lako na itakuwa faida kubwa kwa mkulima," alieleza Dk. Kabugi.

Katika andiko lake kwa wakulima, Dk. Kabugi ameeleza kuwa zao hilo la tephrosia vogelii (utupa) au 'fish poison' kama wanavyoliita, utafiti umefanyika na zao hilo limeonekana kuwa salama kwa binadamu.

Kuhusu zao la chia seed au salvia hispanica, Mkurugenzi huyo amedai ni lishe nzuri ya ubongo na kurudisha kumbukumbu ambalo pia hutumika kurudisha kinga ya mwili na lina madini yanayojenga mifupa na protini kwa wingi.

Zao hilo ambalo asili yake ni Mexico na America ya Kaskazini ni miongoni mwa mazao yatakayolimwa kwa kilimo cha mkataba kitakachofungwa kati ya Kampuni ya IHC na mkulima.

## Watanzania wanaotembelea Kinapa waongezeka

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

KIWANGO cha Watanzania wanaotembelea Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (Kinapa) kimeongezeka, huku wanaochochea hamasa hiyo wakitajwa kuwa ni wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Kinapa, Betrita Loiboki, amesema idadi ya watalii wa ndani wanaotembelea hifadhi hiyo na kupanda mlima huo mrefu kuliko yote barani Afrika, imeongezeka kutokana na wananchi walio wengi kuanza kuhamasika kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo.

"Mwitikio huu wa watalii wa ndani ni changamoto sasa kwetu kuwahudumia lakini pia inaongeza kiwango chetu cha uchangiaji wa pato la taifa na ajira kwa Watanzania. Kada hii ya wanafunzi inatupa hamasa zaidi na tunafurahi wanakuja Watanzania, kuliko kuachia watalii kutoka nje ya nchi ambao ndio wengi wamekuwa wakitembelea vivutio hivyo ikilinganishwa na idadi ya Watanzania," alisema.

Mhifadhi huyo alisema ni vyema halmashauri za wilaya zikaangalia uwezekano wa kuwezesha wanafunzi kutembelea hifadhi ya Mlima Kilimanjaro kujifunza kwa vitendo kama ilivyo Halmashauri ya Wilaya ya Siha ambayo tayari imeanza utaratibu huo.

Kwa upande wake, Mhifadhi wa Ikolojia wa Hifadhi hiyo ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, Imani Kikoti, akizungumzia vivutio vinavyovuta hamasa hiyo, alisema ni eneo lililohifadhi bioanuai kubwa za aina mbalimbali za mazingira na viumbe.

Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ina bioanuai za aina 2,500 za mimea, aina 140 za wanyama na aina za ndege 177.

"Vivutio vya urithi wa dunia ambavyo tunatakiwa kuvilinda kwa hali na mali ni kama mimea adimu na isiyopatikana sehemu nyingine duniani, barafu ya kudumu karibu na Ikweta (300km), maporomoko ya maji kama Lauwo na Kinukamori Water Falls. Pia tunahifadhi kwa sababu kuna kasoko kuu ya mlima (crater) na uwanda wa juu wa Shira," alieleza Kikoti.

Baadhi ya walimu Uleki Massawe na wanafunzi akiwamo Brighton Shoo ambao wamepata fursa ya kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia lango la Londrosi lililopo Wilaya ya Siha na kujionea aina mbalimbali ya vivutio, uoto wa asili na miamba wamesema mafunzo ya vitendo ni muhimu kwa wanafunzi kwani hali ambayo itawawezesha kufanya vizuri katika masomo yao.

Kwa kawaida, safari ya kupanda Mlima Kilimanjaro humpitisha mpandaji katika kanda za hali ya hewa tofauti kuanzia ile ya nchi za Tropiki hadi Arktiki. Kilele cha Kibo chenye urefu wa mita 5,895, ndicho kivutio kikubwa kwa wageni kutokana na kufunikwa na theluji.

Katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, kuna njia sita za kupanda hadi kileleni na njia iliyo rahisi na iliyo maarufu zaidi ni ile ya kuanzia lango la Marangu ambako ndiyo makao makuu ya hifadhi.

Nipashe

# TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Jumanne Machi 26, 2019

Ukurasa 17



## Mzizi wa ubaguzi ulikojichimbia

Ukurasa 18




## JE, WAJUA?

Hoteli ya kwanza katika anga za juu




Ukurasa 19

## Kampuni za simu nchini tunakesha mfumo malipo uhamie elektroniki



# Shule maalum ya kompyuta kwa kinadada ‘waliochemsha’

Ukurasa 16

ELIMU KUTOKA POLISI

# Kwanini uripoti Polisi simu yako inapopotea?



Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Ahmed Msangi

MWANANCHI mwenzangu, kwanza nianze na kukupa pole kwa majukumu ya kila siku pamoja na hongera kubwa kwa kujishughulisha kama Mtanzania mwenye kuhitaji maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla.

Dunia yetu imeingia katika maendeleo ya teknolojia ya intaneti na mitandao. Kutokuwa na ufahamu wa mitandao, ni kukosa kitu muhimu katika maisha, kwa maana tunakoelekea kila kitu kitahusisha mitandao, isipokuwa mambo machache sana.

Ebu jiulize swali, kama umewahi kutoka nyumbani ukasahau simu yako ya mkononi je, siku hiyo utafanya kazi vizuri? Jibu liko wazi, hakuna aliyeko salama katika zama hizi, kwamba anaweza kukwepa teknolojia, la hasha ni ngumu sana.

Tujifunze kwanini ni muhimu sana kupata elimu hii ya makosa yanayohusiana na mitandao.

Kwanza, kila mmoja ajue kwamba katika matumizi ya mitandao (hapa nina maana ya Intaneti) lazima utajikuta ni mwathiria wa matumizi ya mitandao ya kijamii, mfano Whatsapp, Facebook, Tweeter, Instagram, snapchart, blogs, Websites, Forums.

Katika matumizi hayo, kila mmoja wetu huenda akajikuta mtenda makosa ya kimtandao kwa namna moja ama nyingine.

Ukiipitia Sheria ya Makosa ya Kimtandao, 'The Cyber Crime Act 2015' utajua kabisa kwamba hakuna ambaye hataonekana hatendi kosa lolote la kimtandao katika jamii, japo watu huzidiana ukubwa wa makosa yenyewe.

Hivyo, ni wazi kwamba, kila mmoja wetu ni mwathirika wa watumizi ya Intaneti na anahitaji elimu hii.

Asilimia kubwa ya watu duniani kote, ni watumiaji simu za mkononi maarufu kama 'smartphone.' Simu hizi zimegawanyika katika mifumo mbalimbali, kutegemeana na mfumo uliowekwa ndani ya simu yenyewe, kama vile: Android, Windows, Rim, IOS, Droids.

Asilimia kubwa sana ya watu duniani hutumia simu zenye mfumo wa Android, ambao ndio mwandishi wa makala amejikita zaidi katika kuelimisha kuhusiana na simu za aina hiyo.

**KWANINI URIPOTI POLISI**

Zipo sababu nyingi za kiusalama, zinazoweza kuwa hatari kwa mwanachi aliyepoteza simu, asipochukua hatua zinaweza kumkuta, iwapo simu hiyo itafika mikononi mwa watu wabaya, yaani wahalifu wa kimitandao.

Kutokana na kwamba upelelezi wa makosa ya kimtandao huwa mgumu na unahitaji sana utaalamu wa hali ya juu, ni muhimu kutoa taarifa mapema sana. Nitataja sababu mbili muhimu sana za kuzingatiwa, kutokana na mada hii ni ndefu sana kitaalamu.

**MFUMO DHAIFU WA ULINZI**

Simu za Android, ambazo mmiliki wake ni kampuni ya Google, haina ulinzi wa kutosha kuweza kumzuia mtu asiyekuwa mhusika kuingia kwenye mfumo na kufanya anachotaka.

Hapa nina maana hata kama umeweka ulinzi kama vile: 'Pina, Password, Fingerprint au Patten' zipo njia kadhaa za kuondoa ulinzi wako, iwapo anayefanya hivyo ana lengo la kutenda uhalifu. Uzoefu unaonyesha, watu wengi waliopoteza simu wanalalamikia kusambazwa kwa picha zao za siri katika mitandao mbalimbali ya kijamii, pamoja na kuibiwa fedha kwenye huduma za mitandao ya kifedha zilizopo.

Katika eneo hili, pia ni hatari kwa mtu aliyepoteza simu, kwani anapokosa ulinzi wa simu hiyo, mhalifu anaweza kupata nafasi ya kuingia katika mitandao ya kijamii, blogs, You tube channels, Gallary za simu na kufanya mambo mbalimbali mabaya.

Pia, mwenye nia mbaya huyo anaweza kutapeli watu kutumia akaunti ya mhusika na mambo mengine mengi mabaya, ambayo ni uhalifu kama uhalifu mwingine.

**WADUKUZI KIMTANDAO**

Wapo watu wanaitwa wadukuzi. Hawa ni watu ambao wanatumia mfumo wa kudhoofisha kifaa chenye mfumo na kuweza kupenya na kufanya wanachotaka ndani ya kifaa husika.

Kitaalamu ni wanatumia Hacking Mods Applications ambazo zinauwezo wa kufanya chochote atakachohitaji kwenye kifaa husika.

Mfano upo kwamba, ni uwezo wa kurudisha vitu ulivyowahi kufuta kama picha, video na ujumbe wowote, ambazo zipo zina uwezo wa kutuma taarifa za muhanga kuanzia sauti, ujumbe wa maneno wa kawaida na hata taarifa zote utakazopokea na kutuma kwa njia ya mitandao ya kijamii na barua pepe. Hii ni hatari sana na ni kosa kisheria hata za Kimataifa.

**UNAWEZAJE KUWA MUHANGA?**

Kumbuka mambo yaliyotajwa hapo juu yanapotokea kwenye simu uliyoipoteza kunaweza kupelekea makosa ya kimtandao ambayo, pia ni jinai. Mtuhumiwa namba moja atakuwa ni yule aliyepoteza simu kwa uzembe ambaye hakuripoti upotevu wa simu yake katika kituo cha Polisi.

Hivyo, sheria iko wazi utawajibishwa kwakutumia kifaa chako (simu) kwa kufanyia uhalifu wa kimtandao. Mfano ukipoteza simu au kuibiwa, haujatoa taarifa, mtu aliyeokota akasambaza picha chafu, akatapeli watu, na kutuma ujumbe wa matusi.

Yote hayo ni makosa kisheria na polisi watafanya kazi yao ya kuchunguza na kumkamata mmiliki wa simu, hivyo utajikuta kwenye matatizo pasipo kutenda kosa, hivyo kuripoti kituoni mara tu unapoibiwa au kupoteza simu ya mkononi, ni suala la msingi kwa watumiaji wote wa simu za mkononi, ili usije jikuta unatuhumiwa uhalifu pasipo kutenda kosa.

*•Imetolewa na kitengo cha Uhusiano, Polisi Makao Makuu, Dar es Salaam. barua pepe habari.phq@tpf.go.tz au habariphq@gmail.com*

---



TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Upotoshwaji maneno ya Kiswahili ulivyo

SHAKA (hali ya kuwa na wasiwasi juu ya jambo) yangu ni jinsi Kiswahili kinavyoborongwa (haribu kazi kwa kasi; atili, bananga) na waandishi wa magazeti yetu ya Kiswahili.

Matokeo yake sasa, hata kuandika sentensi zenye mtiririko unaoeleweka zatushinda waandishi. Kwa muktadha huu, 'maana' ni dhana inayowakilishwa na neno; ufafanuzi wa kitu au jambo.

Kinyume chake ni upotoshaji, yaani kitendo cha kufanya mtu mwingine afanye jambo lisilokuwa sahihi.

Ingawa yapo baadhi ya maneno yenye maana zaidi ya moja, sioni sababu ya kupotosha maana halisi ya maneno, ilhali yapo maneno sahihi, lakini hatuyatumii. Badala yake twatumia maneno yaliyo tofauti na maudhui (wazo kuu linaloelezwa katika maandishi au katika kusema) ya kazi zetu.

'Mwisho' ni ukomo wa jambo; kikomo, hitimisho; hali ya kumalizika, tamati. Kwa hiyo isemwapo 'mwisho wa siku,' maana yake ni mwisho wa siku husika.

Soma sentensi ifuatayo: "Akizungumza na … jana, Katibu Mkuu wa Klabu ya…., alisema walikuwa wamemtengea dau …na alikubali kwenda kusaini mkataba, lakini mwisho wa siku wakasikia amechukuliwa…."

"Mwisho wa siku hutumiwa na watu wengi kiasi cha kuonekana ni maneno sahihi kumbe sivyo. Badala ya kuandika 'mwisho wa siku' ingeandikwa 'mwishowe' au 'hatimaye.

"…alifunga bao lake la tisa msimu huu, wakati…ikipata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya… katika pambano lililopigwa Uwanja wa Taifa ambapo msemaji wake…. Aliamua…. kuwatawanya mashabiki wa Yanga waliokuwa wakimzonga mara baada ya pambano hilo kali."

"Simba yazidi kutetema Bara" ni kichwa cha habari kwenye gazeti mashuhuri la michezo nchini. Je, ni kweli kuwa Simba ilitetema? Maana ya 'tetema' ni kitendo cha kutikisika, harakaharaka; tetemeka. Ingeeleweka kama ingeandikwa "Simba yatetemesha Ligi Kuu."

Waandishi tunavyoharibu maneno: "Mara baada ya kuanza kwa Ligi Kuu Bara kikosi cha… (timu) hakikuwa kikipewa nafasi kubwa ya kutamba kutokana na kuwa na wachezaji wengi wa kawaida, huku mafundi wakiwa ni wachache mno." Sentensi ya maneno 31 yaliyoandikwa shelabela (hali ya kukosa mpango maalumu)!

Ingeandikwa: "Ligi Kuu ya Bara ilipoanza,…haikupewa nafasi kubwa ya kufanya vizuri kwani wachezaji wengi walikuwa wa kawaida wakati mahiri wakiwa wachache." (Maneno 22). 'Mahiri' ni -enye uhodari wa jambo fulani.

Sentensi ya mwisho ya habari hiyo haikumalizika; kwa hiyo haikueleweka! "Mabingwa watetezi wa ligi hiyo,… wanashika nafasi ya tatu baada ya kujikusanyia pointi 27 kutokana na…" (Mwandishi alikomea hapo bila kueleza ni kutoka na nini.)

Haraka haraka haina baraka! Wanaodurusu (wanaopitia maandiko ili kusahihisha) hawakuwa makini katika kazi yao.

"Kikosi changu ni kizuri na tunatambua tunaenda kucheza na timu nzuri lakini mara nyingi huwa kikosi cha ushindi katika timu yoyote hakibadilikagi," alisema Aussems, ambaye alichukua mikoba ya kukinoa kikosi cha…

'Haibadilikagi' si Kiswahili sanifu (-enye kufuata vigezo vilivyokubalika.) 'Mikoba' ni wingi wa 'mkoba' na maana yake ni chombo cha kusukwa au kushonwa cha kutilia vitu; mkoba wa ukili. Pia, ni mfuko wa mganga wa kuwekea zana zake za kazi. Ina maana kocha wa Simba alikabidhiwa mikoba ya uchawi!?

Ingeandikwa: "Kikosi changu ni kizuri na tunakwenda kupambana na timu nzuri. Hata hivyo, mara nyingi kikosi cha ushindi hakibadiliki," alisema

Sentensi zinakorogwa sana na kumfanya msomaji arudie kuisoma, ili aelewe kilichoandikwa.

**Methali: Pauliwapo nyoka hapaachi ndombezi.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**Simu: (+255) 0784 334 096**

ELIMU

NA YASMINE PROTACE,
MKURANGA

# ELIMU KICHINA INAVYOZIDI KUMEA SHULE SEKONDARI

- Mkurugenzi Wizara: Kuna shule 17 serikalini
- St. Mathew: Sisi tumo, shule yetu 75% sayansi



Wanafunzi wa Shule ya St Mathew, wakionyesha kazi zao katika mahafali shuleni kwao. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

KUWAPO uwekezaji mkubwa kiuchumi kwa taifa kupitia uzalishaji wa bidhaa na huduma, ajira na kodi kunaamua hatima ya wengi kwa mengi.

Katika kuchangamkia fursa za ajira kutokana na uwekezaji, mataifa yamewekeza na mengine yako mbioni kuwekeza, hivyo jamii ina wajibu kujipanga kupokea uwekezaji huo, ili wanufaike nao. Ni kwa vipi? Moja ya njia kuu ni ajira.

Hapo ndipo inapokuja suala la elimu na vipengele vyake, kwani ni mtaji muhimu wa kuajiriwa.Walioelimika ni wa kwanza kunufaika na wasioelimika wanaangukia katika makundi ya chini kama vile vibarua.

Pia, ndipo inapoamsha jukumu la walimu kuwafundisha wanafunzi kwa mbinu za nadharia na vitendo, ili kuwajegea ubunifu na kuweka kando ukaririshaji.

### MKURUGENZI ELIMU

Akiwa katika katika mahafali ya Kidato cha Sita katika Shule ya Sekondari St.Mathew's, iliyopo Mkuranga, hivi karibuni, Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Sekondari katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Benjamin Oganga, analisisitiza hilo.

Anasema walimu wanapaswa kufundisha kwa vitendo, ili kuwafanya vijana wao kuwa wabunifu na wajuzi wenye mafanikio.

Oganga, aliyekuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo, analaumu ufundishaji wa kukaririsha unachangia wanafunzi kutokuwa wabunifu.

"Kuna baadhi ya walimu wamekuwa wakiwafundisha wanafunzi masomo kwa kuwakaririsha na hali hiyo inachangia mtoto kutokuwa mbunifu," anasema.

Oganga anaipongeza St .Mathew kwa kuwafundisha wanafunzi kwa vitendo, ili baadaye wajitambue na kuwa wabunifu.

Anarejea ziara yake katika Maonyesho ya Vijana Wanaohitimu Kidato cha Sita katika masomo yao, aligundua wanafunzi wamejifunza kwa vitendo kutokana na maneno waliyoeleza, vikiwamo vifaa walivyotumia katika maonyesho hayo walifafanua matumizi yake.

Akizungumzia hali ya elimu nchini, anasema kuanzishwa kwa elimu bure kumetoa mwamko mkubwa kwa wazazi wasiokuwa na uwezo, sasa wanaowaandikisha watoto wao shuleni.

### LUGHA ZA KIGENI

Mkurugenzi Msaidizi anasema nchini kuna shule 17 za sekondari zinazofundisha lugha ya Kichina, taifa ambalo sasa liko juu katika uhusiano wa biashara nchini na dunia kwa jumla.

> "Kuna baadhi ya walimu wamekuwa wakiwafundisha wanafunzi masomo kwa kuwakaririsha na hali hiyo inachangia mtoto kutokuwa mbunifu.

Katika kulitekeleza hilo, Oganga anasema kuna walimu waliotoka China kutoa mafunzo nchini na wanawanoa wenzao wa nchini, ili Wachina watakapoondoka, walimu wa nchini waendeleze jahazi.

Mbali na Kichina, anataja Kifaransa na Kiarabu, kuwa kinafundishwa katika lengo la kuwawezesha Watanzania wajue lugha tofauti

### UHUSIANO WA SHULE

Akizungumzia ushirikiano wa shule binafsi na za serikali, anasema wanatambua mchango mkubwa uliofanywa na shule binafsi katika kuwapatia elimu Watanzania

Oganga, anasema shule binafsi zipo nyingi na zimekuwa zikitoa huduma ya elimu kwa Watanzania wengi wanaokosa nafasi katika shule za serikali.

Anasema ushirikiano upo na wamekuwa wakiwapa vitabu, pia kunapokuwapo semina, wanazialika shule binafsi, lakini wamiliki kuombwa kuwawezesha walimu nauli ili waweze kufika na kushiriki.

Anasema kuna shule binafsi ambazo hawezi kuzitaja, lakini zimekuwa zikipatiwa walimu kutoka shule za serikali kuwasaidia kufundisha.

Pia, anaipongeza St. Mathew's kwa kuwa na michepuo ya masomo yote, huku ikihamasisha wanafunzi kusoma michepuo ya sayansi.

Benjamin Majoho, ni Ofisa Elimu wa Sekondari Wilaya ya Mkuranga, anasema wilaya hiyo ina shule tatu za kidato cha tano na sita.

Majoho anasema St.Mathew's imekuwa mkombozi katika wilaya hiyo, kutokana na kiwango chake bora cha ufaulu katika mitihani ya taifa kila mwaka.

### UONGOZI WA SHULE

Mmiliki wa shule hiyo yenye miaka 21, Peter Mutembei, anaipongeza serikali kwa kuiruhusu kutoa kibali cha uanzishwaji shule binafsi.

Anataja siri ya ufanisi kitaaluma kwa shule yake inafanya vizuri kila mwaka kutokana na nidhamu walizowajengea wanafunzi wao.

"Bila ya nidhamu mwanafunzi hawezi kuwa na maadili," anasema Mutembee na kuongeza kuwa, katika hatua ya kuifuata Tazania ya Viwanda, asilimia 75 ya wanafunzi shuleni kwake wanasoma sayansi.

Pia, anataja motisha kwa walimu na wanafunzi kama vile zawadi za fedha tasilimu, punguzo la ada kwa walimu wenye watoto shuleni na wanaofanya vizuri, kumechangia wanafunzi kufanya vizuri.

Mutembei, anasema kutokana na kujikita katika huduma za elimu, ana shule tatu wilayani Mkuranga, zingine ni Victory na Ujenzi.

Mmiliki huyo anaelekeza ombi kwa serikali, izikumbuke shule binafsi zinazofanya vizuri na kuweka mbali dhana ya kutilia shaka matokeo ya shule binafsi, isipokuwa penye uhakika.

### MKUU WA SHULE

Mkuu wa Shule hiyo, Christopher Segeleyi, anataja siri ya mafanikio ni nguvu ya pamoja iliyopo kati ya walimu na wanafunzi, akitaja mfano wa kielelezo kwamba mwaka jana, wanafunzi darasa la saba 30 walipata daraja A.

TEKNOLOJIA

NA SALOME KITOMARI

# Shule maalum ya kompyuta kwa kinadada 'waliochemsha'

## • Wageuzwa wasuka programu, tovuti • Balozi Marekani azikubali kazi zao

NI dhana iliyozoeleka kwamba wanaume au wavulana, kwa vijana wadogo, kawaida yao wanajifunza masomo yanayohusiana na teknolojia, huku wasichana au wanawake wakielekea kwenye masomo ambayo yanaaminika siyo magumu.

Asasi ya elimu ya Apps and Girls, ambayo ni mahususi kwa kinamama, imekuja na mtazamo inayoutafsiri kuwa ni kuvunja mwiko, kwa kuwa na programu ya kuwafundisha wanawake masomo ya tekonolojia.

Hapo mitaala yao inazama zaidi katika elimu ya kompyuta, wakizama zaidi katika maeneo yanayolikana kitaalamu kama 'applications' na tovuti wanazoziuza kwa wateja inayowapa kipato.

Kupitia kaulimbiu yao 'Tech is Female' (Teknolojia ni wanawake), anasema wasichana hao kwa nyakati tofauti wametengeneza tovuti wanazoziuza kwa wateja na inawapatia fedha za kuendesha familia.



Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson (kulia), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari (kushoto), wakipata ufafanuzi wa wataalamu wa teknohama. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Apps and Girls, Caroline Ekyariisma. **PICHA ZOTE: JOHN BADI.**

### MKURUGENZI APPS

Mkurugenzi Mtendaji wa Apps and Girls, Caroline Ekyariisma, anasema mchakato wa kuwapata wasichana hao, ulifanyika nchi nzima na kati yao wahitaji 30 ndio waliofuzu mafunzo yao yakiwa ni kuwafundisha teknolojia, hadi hatua ya kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Anasema lengo la taasisi hiyo, ni kuwawezesha wanawake na wasichana masuala ya teknolojia au Habari na Mawasiano (Tehama), ili wabadili maisha yao kwa kutumia teknolojia bila ya kuangalia umri na kipato chao.

### NJE YA CHUO

"Tunaunda klabu kwenye shule za msingi na sekondari ambazo kila wiki wanafundishwa masuala ya teknolojia, kama kutengeneza tovuti na vifaa vinavyosaidia watu kuboresha maisha yao," anasema.

Aidha, Apps and Girls inawasaidia wasichana waliokosa fursa ya kuendelea na elimu kutokana na sababu mbalimbali kama kupata mimba, ambao hufundishwa mafunzo ya teknolojia ya ngazi ya juu kwa miezi sita.

"Tunataka wafikie uwezo wa kuchukua hii elimu, kuiunganisha na ujasiriamali na kubuni vitu ambavyo vitawawezesha kupata fedha hata kabla ya kupata kazi," anasema.

Aidha, anasema kampuni ya simu ya Tigo, ilianza kukisaidia kituo hicho kwa muda mrefu, kwa kuwapatia fedha za kuwaendeleza wasichana kwenye teknolojia na hivi sasa wameshawafikia wasichana wengi wanaojiajiri kupitia tekonolojia hiyo.

> "Tunaunda klabu kwenye shule za msingi na sekondari ambazo kila wiki wanafundishwa masuala ya teknolojia.

Caroline anasema, hivi sasa wameshajipanga kufikia zaidi shule 51 nchini, pia mabinti walioacha shule kwa sababu mbalimbali zaidi ya 3,000

Anasema, wasichana wengi wana uhitaji wa elimu hiyo, lakini uwezo wa taasisi hiyo ni mdogo na kwamba wapo wanaobuni vitu wakiwa wadogo, lakini wazazi wao hawana uwezo wa kuendeleza vipaji hivyo.

Kwa mujibu wa Caroline, wasichana wanatarajiwa kutengeneza tovuti hizo kwa ajili ya maonyesho ya wajasiriamali wasichana yatakayofanyika Novemba, mwaka huu.

Anafafanua: "Tunawafundisha na baada ya muda wanaajiriwa na wengine walioko shuleni wameendelea na masomo yao, pia wameweza kushiriki mashindano ya ubunifu na wengine wamepata nafasi ya kusoma nje ya nchi."



Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson, akibadilishana mawazo na wasichana waliotengeneza tovuti na 'applications' wanazoziuza.

### MATUNDA YA SHULE

Caroline anataja moja ya matunda ya kazi za mabinti hao yatokanayo na kazi zao, ni kuchangia ongezeko la wataalamu wa kompyuta wa jinsia yao, katika sehemu nyingi.

"Watoto wetu siyo kwamba wanafundishwa kutengeneza Apps na kubaki nazo, bali wanasaidia watoto wengine, wanakuwa 'mentors' (wakufunzi wasimamizi) wa wengine, ili kuwapa ujuzi wa utengenezaji wa huduma mbalimbali kwa ajili ya kuziuza," anasema.

"Hawa mabinti wakipata familia zao, wataendelea kwa kuwa ni kitu kipo ndani yao na wataendelea kusaidia wengine na mwishowe kusambaza ujuzi, ambao husaidia kuwa na wasichana wengi waliojifunza teknolojia na kuitumia kama biashara," anaongeza mkurugenzi huyo.

### WALIVYOPATIKANA

Akielezea jinsi mabinti hao walivyopatikana, Mkurugenzi anasema walitangaza kwenye mitandao ya kijamii na wapo walioomba na kwenye taasisi zinazohusiana na wasichana na watoto na wakawapendekeza watoto tofauti.

"Tulipata maombi zaidi ya 190, lakini tulikuwa tunataka wasichana 36 ambao tuliwafanyia usahili kujua wanapenda nini na kwanini wanapenda kujiunga na sababu zilizowafanywa wasiendelee na masomo," anasema.

"Tumefanya hivyo, kwa kuwa tulitaka tupate mwenye utayari wa kuendelea na ana nia ya kujifunza, lakini amekosa uwezo wa kujiendeleza. Tutaendelea hivi kila baada ya miezi sita kupata wasichana," anasema.

Anataja mbinu nyinyine, ni kuwatembelea wanafunzi shuleni wanaofundishwa na baadaye wanafika kituoni humo mara moja kwa wiki, kwa ajili ya kujifunza zaidi Tehama, ikiwamo kuunda vitu ambavyo wataviuza na kupata fedha.

> Wanawake hupendelea zaidi kuwekeza mapato yao kwa ajili ya maslahi ya familia zao mara 10 zaidi ya wanaume.

### UFADHILI

Mkurugenzi huyo anasema, wasichana hao hukutanishwa na wafadhili na wawekezaji na kisha wanawauzia mawazo yao, baadhi wanapata wafadhili wa kuyaendeleza zaidi na hivyo kufanya ujasiriamali wa teknolojia.

Anasema mafunzo hayo huwajengea uwezo kujiamini, na kuwafanya waone kuwa teknolojia siyo ya wanaume pekee bali hata wasichana wanaweza kuitumia kujipatia kipato kwa kujiajiri na kuajiri wengine.

"Tuna wasichana ambao wametoka vijijini kabisa, tuliwaleta tukawafundisha kwa muda wa miezi mitatu, tukawatuma waende mtaani kutafuta wateja.

"Walipata ambao waliwaamini na kuwapa kazi ya kutengeneza tovuti, pia tunawafundisha lugha ya Kiingereza inayowasaidia kuwasiliana kirahisi," anasema.

"Lengo letu ni kutoa mafunzo ya kutengeneza programu kwa wasichana katika shule 61 za sekondari zilizo chini ya mpango wa 'Tigo E-Schools' nchi nzima, unashirikisha makundi ya wasichana ambao hawapo shuleni, wakaopata fursa sawa ya kushiriki na kunufaika," anasema.

### BALOZI MAREKANI

Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson, amewatembelea wasichana hao na kueleza kuwa ukatili wa kijinsia unaendelea nchini kwa kisingizio cha mila na desturi.

Dk. Patterson anasema, wasichana na wanawake hukutana na vikwazo vingi vya elimu na afya, na kwamba wakati wa hedhi ndipo wasichana wanalazimika kuacha shule na kuingia katika wazo la kuolewa.

"Wanawake hupendelea zaidi kuwekeza mapato yao kwa ajili ya maslahi ya familia zao mara 10 zaidi ya wanaume; Tanzania asilimia 20 ya wanawake wenye umri wa miaka 20 hadi 24, wamemaliza elimu ya sekondari na asilimia 20 hawana elimu kabisa," anasema.

Kwa mujibu wa Balozi Patterson, changamoto kubwa inayowakabili wanawake ni kukosa nguvu, ushawishi na sauti ya kufanya maamuzi muhimu yanayohusu masilahi yao na kutenda kwa uhuru bila adhabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya simu ya Tigo, Simon Karikari, anasema kampuni hiyo inatambua mchango wa wasichana na wanawake kwenye maendeleo ili kutoa fursa sawa kwa walio wanafunzi na wasio wanafunzi katika kuwezesha kiuchumi na kidijitali na kuwa vinara ulimwenguni.

"Uwezeshaji unaofanywa na Tigo kwa wasichana na wanawake, unalenga kuwezesha utekelezaji wa miradi ya kigunduzi kwenye Tehama kwa makundi ya wasichana waliofanyiwa mchujo na ambao watapewa mafunzo maalum kabla ya kuwekwa nchini ya uangalizi maalum wakati wakifanya miradi walioyobuni wenyewe," anasema.

---

JIELIMISHE

# Mzizi wa ubaguzi ulikojichimbia



Watoto wa nchini Afrika Kusini, ambako katika zama za miaka ya 1980, weusi na weupe hawakuruhusiwa kuoana. **UN.**

"UMEFIKA wakati wa kusema sasa imetosha ubaguzi wa rangi. Chuki dhidi ya wageni na mifumo mingine yoyote ya chuki na ubaguzi haina nafasi katika karne hii," anasema Kamishina Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, Michelle Bachelet.

Katika ujumbe wake maalumu kuhusu siku ya kimataifa ya kutokomeza ubaguzi wa rangi iliyobeba kaulimbiu "kupunguza na kukabiliana na ongezeko la itikadi na misimamo mikali ya kibaguzi, Bachelet anasema:

"Lengo ni kuhakikisha hatua zinachukuliwa kudhibiti hali hiyo ambayo inachagiza ajenda za kitaifa zenye ubaguzi zinasambaa sehemu mbalimbali duniani na kuchochea ubaguzi wa rangi, chuki dhidi ya wageni na hali zingine za kutovumiliana, ambazo mara nyingi zinawalenga wahamiaji na wakimbizi, pia watu wenye asili ya Afrika".

Anasisitiza: "Utaifa na ubaguzi wa rangi havitoi suluhu yoyote ya changamoto zinazozikabili jamii hivi sasa, vinatokana na misingi ya nadharia na kusambazwa na kukuzwa na mitandao ya kijamii.

"Hatua hii imepanda mbegu za hasira na kuvuna chuki na machafuko, suala hili la utaifa ni kinyume kabisa na uzalendo, kwani linaongeza mgawanyiko, linaandaa ghasia na kuzifanya jamii kutokuwa salama."

Anahimiza kuwa watu wote wanapaswa kukemea wazi ujumbe hasa wa kisiasa unaochagiza hali hiyo, kwani anaweza kuipenda nchi yake, pia akaipenda dunia na anaweza kuheshimu taifa lake, wakati huo huo, akiheshimu tofauti zilizopo na wengine.

Mtaalam huru kuhusu mifumo ya kisasa ya ubaguzi wa rangi nchini kuhusu chuki dhidi ya wageni na kutovumiliana , Tenday Achiume, anasisitiza hilo, kwa kulaani vikali ajenda za kitaifa zinazoongeza vitendo na sera za ukandamizaji, ubaguzi na kuwatenga watu ambazo zinaathiri watu binafsi na makundi ya watu kwa misingi ya rangi zao, ukabila, nchi watokako na dini zao.

Anatolea mfano shambulio la wiki iliyopita la jijini Christchurch nchini New Zealand, iliyoya watu 50, akizitaka nchi kusimama kidete kuchukua hatua kukomesha hali hiyo kabla haijageuka na kuwa ni jambo la kawaida. **UN.**

## HABARI KWA UFUPI

JE, WAJUA?

# Hoteli ya kwanza katika anga tofauti




Hoteli ya Aurora. **PICHA: MTANDAO.**

ILINUIWA kusisimua safari za duniani: Kituo cha Aurora, ambacho ni hoteli ya kwanza duniani kwenye mzunguko wa Obiti, katika anga za juu.

Tangazo rasmi kuhusu mpango huo, lilitolewa Aprili mwaka jana huko San Jose, California Marekani.

Hoteli hiyo ya kifahari, imejengwa kwa ukubwa wa ndege kubwa ya kibinafsi, itakayoruhusu watalii kupaa maili 200 kutoka duniani na kupata fursa ya kutupia jicho mandhari ya sayari na mwanga wa Kaskazini na Kusini.

Gharama sio nyepesi; safari hiyo ya siku 12 kwenye kituo cha Aurora inayotarajiwa kufanya ziara ya kwanza ya kitalii mwaka 2022, ni ya thamani ya Dola milioni 9.5 kwa mtu mmoja. Hiyo ni sawa na Sh. bilioni 21.85.

Hata hivyo, kampuni hiyo inasema orodha ya watu wanaosubiri safari hiyo ya kitalii inakusanywa miezi saba, kabla ya safari yenyewe.

"Sehemu ya hisia tunayotaka kuwapatia watu ni kujua maisha halisi ya mwana anga za juu yalivyo," anasema Frank Bunger, mwasisi na Mkurugenzi Mtendaji wa Orion Span, kampuni inayosimamia uidhinishaji wa hoteli hiyo ya Aurora.

"Lakini, tunatarajia wageni wengi watakuwa wakichungulia nje ya madirisha na kuwaita kila wanaowajua na iwapo watachoka, kipo tunachokiita 'holodeck,' mfumo wa uhalisia unaoonyesha hali ilivyo na unaweza kufanya chochote unachotaka kufanya mfano kuelea katika anga za juu, kutembea kwenye mwezi na hata kucheza gofu", anaongeza kusema mkurugenzi huyo.

> "Sehemu ya hisia tunayotaka kuwapatia watu ni kujua maisha halisi ya mwana anga za juu yalivyo.

Mbali na kuweza kuchungulia nyota na sayari ya dunia kutoka dirishani, inatarajiwa wageni katika Aurora watajaribu kufanya mambo katika muda watakaokuwa wakiishi katika hoteli hiyo, kama kujaribu kupanda chakula kama inavyofanywa sasa na maafisa katika ISS.

Wengi katika taaluma ya sayansi wanaona kama hatua isiyoepukika katika maisha ya mwanadamu. Lakini, kuna msemo wa kale, kwamba jihadhari kabla ya hatari; kusema kwamba safari ya raia kwenda katika anga za juu ni kitu kilichoko katika kiwango cha msingi, bado haielezi hatua imepigwa kiasi gani.

Kila mmoja anakubali kwamba, utalii katika anga za juu ni jambo kubwa: Ulianza mnamo 2001 wakati raia wa Marekani Dennis Tito alipolipa shirika la anga za juu Russia Dola milioni 20 (Sh.Bilioni 46) ili kuzuru kituo cha ISS kilichopo huko. Baadhi ya mataifa tayari yameidhinisha msingi katika sekta hiyo katika siku zijazo.

Lakini, wataalamu wanasubiri kuona iwapo utalii wa raia katika anga za juu unaweza kutekelezwa kwa namna gani.

Kilichosalia kubainishwa ni usalama, na viwango vya uhandisi

## UTAFITI

### Unajua 4% ya wakazi duniani ni wahamiaji



Wahamiaji waliokamatwa, wakiwa chini ya ulinzi, mkoani Iringa. **PICHA: MTANDAO.**

SUALA la Uhamiaji ni mada inayoleta mvutano katika zama zilizopo, baina ya nchi mbalimbali, hata inazua msahngao mkubwa.

Je unajua, asilimia nne ya watu duniani wanaishi katika nchi tofauti na walipozaliwa?

"Kumekuwapo mazungumzo mengi kuhusu wimbi la uhamiaji, lakini idadi inaonyesha hadithi nyingine tofauti," mtaalamu wa idadi ya watu, Gilles Pison, anasema.

Msomi na mtafiti huyo wa masuala ya uhamiaji duniani., ana mtazamo wa majumuisho kuwa uhamiaji unaweza kutofautiana kwa kiasi kikubwa, kutokana na taarifa zinazopatikana kuhusu idadi ya watu wanaohamia.

Anatumia mfano wa kilichoitwa 'Wimbi la Uhamiaji Ulaya mwaka 2015,' lililosababishwa na ukosefu wa utulivu katika nchi za Mashariki ya Kati, kutokana na vita vya wenyewe nchini Syria.

"Pamoja na wingi wake hasusan barani Ulaya, wahamiaji walianza kuingia kwa wingi tangu mwaka 2015, kutokana na mizozo ya Mashariki ya Kati, bado mtazamo kuhusu Uhamiaji Kimataifa haujabadilika," Pison anaeleza na kuongeza:

"Umoja wa Mataifa unasema, inakadiriwa kuwa kulikuwa na wahamiaji wanaokisiwa milioni 258 mwaka 2017, sawa na asilimia 3.4. I, idadi ndogo ikilinganishwa na idadi ya watu duniani."

"Kiasi hiki kimeongezeka katika kipindi cha miongo kadhaa-miaka 30 iliyopita, mwaka 1990 ilikuwa asilimia 2.9 na mwaka 1965 ilikuwa asilimia 3 mabadiliko ni kidogo katika kipindi cha miaka 100,"anaeleza

Ulaya ina nchi tatu ambazo ziko kwenye nafasi kumi za kwanza zenye idadi kubwa ya wahamiaji:Uswisi, Uingereza na Hispania, ambayo inaingia katika orodha mpya ya lindi la Uhamiaji.

"Hispania ilikua nchi iliyokua na wahamaji mpaka mwishoni mwa miaka ya 1980, lakini sasa ina takriban aslimia 13 ya watu wake ni wahamiaji, karibu sawa na Marekani," anaeleza Pison

Lakini, vipi kwa nchi zinashuhudia watu wake wakihama? Haitashtusha kuiona India ikiongoza kwa idadi kubwa ya watu wake kuishi nje ya nchi, watu takribani milioni 16 wanaishi nje ya India-zaidi ya asilimia moja ya idadi ya watu nchini humo-ikifuatiwa na Mexico, watu milioni 12.5 wanaoishi nje ya nchi hiyo, yaani katika kila raia 10 wa Mexico, mmoja anaishi nje ya nchi hiyo.

Uhamiaji ni mada inayogusa nchi nyingi duniani na kumekuwa na hofu kuhusu suala hilo

Utafiti wa Pison pia unabainisha nchi zenye sifa ya kutoa na kupokea wahamiaji, mfano ni Uingereza, ambayo suala la uhamiaji imekua kwenye ajenda za kisiasa na zimechukua nafasi kubwa kwenye maamuzi ya nchi hiyo katika kupiga kura katika kuondoka kwenye Umoja wa Ulaya.

Uingereza ina wahamiaji milioni 8.4 lakini pia raia wa nchi hiyo milioni 4.7 wanaishi nje ya nchi hiyo.

• **Makala hii ni kwa mujibu wa mtandao.**

TEKNOLOJIA

**NA MWANDISHI WETU**

BOSI TIGO

# Kampuni za simu nchini tunakesha mfumo malipo uhamie elektroniki

- Aisifu serikali inajitahidi kuifuata dunia
- Ataja mageuzi digitali wanayoyaendesha

SEKTA ya fedha nchini hivi sasa iko katika mageuzi makubwa, kutoka matumizi ya fedha mkononi kuelekea mfumo wa kielektroniki, inayoelezwa kuwa salama na yenye tija zaidi. Hiyo, inaanzia benki ambao ndio wamiliki wakuu wa sekta hiyo, hadi asasi zingine za fedha nchini.

Katika eneo hilo la sekta nje ya benki, kuna kampuni za simu ambazo zimekamata nafasi katika sekta hizo na zinakuja kwa kasi.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya simu ya Tigo, Simon Karikari, anasema kampuni nyingi duniani zinasisitiza malipo ya kielektroniki au malipo yasiyo ya fedha taslimu.

Anarejea nchi nyingi zilizopiga hatua kubwa kibiashara, pia katika eneo hilo ziko juu, ingawaje katika sura pili, anasema Tanzania haijabaki nyuma, akikiri kuwapo hatua kubwa inayochukuliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, zikiwamo kampuni za simu zinazotoa mchango mkubwa kwenye suala hilo.

Mkurugenzi huyo anasema, hadi sasa Tanzania iko kwenye njia sahihi kuelekea uchumi usiotumia fedha taslimu na uwapo wa huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi, umesaidia hatua hiyo kupigwa.

Kwa mujibu wa Karikari, kuwapo huduma jumuishi za kifedha kumewezesha jamii zisizofikiwa na huduma kuu za kifedha, nazo hazijaachwa nyuma, mdau mkuu akiwa simu za mkononi.

Anajigamba kuwa Tigo iko katika nafasi nzuri, pia ni mdau anayeshirikiana katika mfumo wa Malipo ya Kielektroniki wa Malipo Serikalini (GePG,) ikiwa ni kampuni ya kwanza ya simu kujiunga na mfumo huo.

Pia, anasema hadi sasa wanajitahidi kuihamisha jamii kuelekea utamaduni wa malipo yasiyo ya fedha taslimu, kwa kuwaelimisha wateja faida za kutumia huduma za kifedha kwa njia ya simu za mkononi na kufanya mlipo kwa elekroniki.

"Tunaamini kuwa tunaelekea kuzuri katika jitihada za kuhahakisha watu wanajenga utamaduni wa kufanya malipo mbalimbali kwa njia ya kielektroniki na kuachana na matumizi ya pesa taslimu," anasema Karikari.

**WATEJA WA DIGITALI**

Karikari anasema, hivi sasa kampuni yake inafanya jitihada kuhakikisha maisha ya wateja wake yanakuwa ya kawaida na yanayowezesha miamala yao kuwa rahisi zaidi.

Anafafanua: "Hivi karibuni tumezindua 'Tigo Pesa App' ambayo ni mfumo wa kisasa kabisa unaorahisisha malipo mbalimbali kwa njia ya simu.

"Hii ni moja kati ya 'App' bora duniani na ambayo inafanya malipo kuwa rahisi na haraka, ikiwa na usalama wa hali ya juu, kuhakikisha fedha za mteja zinakuwa salama muda wote."

Anasema, kwa kutumia mfumo huo wa 'App' mteja anaweza kuchagua namba kutoka kwenye orodha yake aliyozihifadhi kwenye simu yake na kufanya malipo, badala ya kutafuta wasaa wa kuzinukuu pembeni.

Lingine analolieleza, ni mteja anaweza kuchukua taarifa za kielektroniki (kus-can QR codes) kwa zaidi ya watoa huduma 4,000 pamoja na baadhi ya taasisi za serikali na kisha anafanya malipo kirahisi.

Mkurugenzi Karikari anasema, maendeleo yaliyoko sasa yanaibadilisha jamii, ingawa kuna safari ndefu ya kufikia viwango vya juu vya huduma za fedha inayofikia lengo la kuwa na jamii isiyotumia fedha taslimu na kufanya malipo kwa wakati.

Anaeleza haja ya kuwa na jamii sasa inayohitaji kuwa na muda wa kutosha kubadili utamaduni wa awali na kuwafanya wateja waamini haja ya kuhamia kwenye utamaduni mpya.

Pia, anasema mbinu za malipo ya umma zilizoko sasa hazitoshi kuifanya ihamie kwenye mfumo mpya usiohusisha fedha taslimu.

Wadau wa fedha pamoja na kampuni za simu, zinasema hivi sasa zinaendelea kuongeza wigo wa malipo kwa njia ya kielektroniki, ili kufikia malengo hayo.

**UZINDUZI WA APP**

Kuhusu jitihada za kampuni yake, anajivuna kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu sasa, imewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye mfumo wa malipo ya kidigitali, ikilenga kuwapatia wateja huduma za kifedha zinazoendana na dunia ya kisasa.

"Tigo Pesa Apps campaign ni hatua mpya ya kuboresha uzoefu wa wateja wanaotumia na watakaotumia huduma ya Tigo Pesa. Pamoja na uzoefu huo mpya na wa kipekee, maboresho hayo mapya yanafanya malipo kuwa rahisi, haraka, pia salama kwa kiasi kikubwa.

"Watumiaji wake wataweza kufanya malipo kwa zaidi ya taasisi 300 za serikali kwa urahisi zaidi, kwa maana tayari zipo kwenye 'App,'' anasema Karikari.

Kuhusu usalama wa mfumo huo ambao ni sehemu ya mambo ambayo wateja wanayazingatia sasa, anajitetea uko salama na unamhitaji mteja kutumia namba yake ya siri kila anapohitaji kufanya miamala yake.

"Imetengenezwa kwa kuzingatia usalama wa fedha za mtumiaji, kwa kuhakikisha inafuata matakwa ya sheria kama ambavyo inaelekezwa na mamlaka inayosimamia na kudhibiti mawasiliano," anahitimisha.




Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo Tanzania, Simon Karikari, akizumgumza katika hafla inayohusu teknolojia ya mawasiliano ya habari, katika Shule ya Apps Gilrs, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU.**



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Wadau wanajadili:

## Hisabati limo katika kundi la masomo yanayowasumbua sana wanafunzi wengi, kufikia hatua ya kuliogopa. Nini mchango wa wazazi, katika kuwafanya watoto wao walipende na kulimudu?



**ALLY SULEIMAN (MKAZI WA DAR ES SALAAM)**

SOMO la Hisabati lina umuhimu mkubwa kutokana na nafasi yake, ukweli ni kwamba ndio kichocheo cha maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kwa hiyo, mzazi anatakiwa kuwa karibu na mtoto, pia kuwasiliana na walimu kila mara, hasa somo hili kwa ajili ya kujua tatizo la mtoto wake kama anashindwa kulimudu.

Walimu nao wanatakiwa kuwa marafiki wa wanafunzi, ili kuwaondolea hofu au woga.


Hatua hiyo itawezesha kujua wanafunzi wana matatizo gani katika somo hilo na kutafuta njia za kuwasaidia.

Serikali ilishasema inahitaji sana wanafunzi wasome Hisabati, ili waweze kuendeleza sayansi na teknolojia, ambayo itasaidia katika utekelezaji wa Sera ya Viwanda.

Kwa hiyo, sisi wazazi kila mmoja wetu anatakiwa kumhamasisha mtoto wake kupenda somo hili.

Tukifanya hivyo tutakuwa na mchango mkubwa wa kuwafanya walione kama somo la kawaida.

Wakati serikali ikichukua hatua za kuongeza walimu wa Hisabati shuleni, pia kutoa mafunzo kwa walimu wanaofundisha somo hilo, wazazi nao watimize wajibu wao siyo kuachia walimu tu.



**MICHAEL MALEMBEKA (OFISA TEKNOLOJIA SIDO, DAR ES SALAAM)**

KWANZA, ni vyema kujua chanzo cha baadhi ya wanafunzi kukwepa somo hili. Mojawapo woga wao wenyewe na kutojiamini, kutokana na kusikia maneno ya mitaani kuwa hisabati ni ngumu.

Mbaya zaidi, baadhi ya wazazi hawajawa chachu ya kuwasaidia kisaikolojia watoto wao kuhusu Hisabati.

Mzazi anatakiwa kumjenga mtoto kujiamini katika somo hilo, kumsisitiza na kumnunulia vitabu vya somo na umsaidia kujifunza afanye mazoezi kila jioni, ili aweze kulizoea na hatimaye kufaulu.

Ikumbukwe, hata wanamichezo hufanya mazoezi ili kujiandaa kwa mechi.

Ukifuatilia utagundua kwamba, kwa sasa wazazi wengi wako 'bize', hawana ukaribu na watoto wao, hawana muda wa kuwauliza watoto wao wamejifunza nini shuleni.

Ushauri wangu ni kwamba wazazi wawape watoto wao matumaini na kuwajengea ujasiri, kwani hiyo ndio siri ya kushinda magumu yote.

Ninaamini kwamba mwanafunzi akiwezeshwa anaweza. Wazazi wasiwe chanzo cha kukatisha watoto wao tamaa bali wawahimize kupenda masomo yote.



**AUGUSTINE BYALILE (MWALIMU MKUU SHULE YA MSINGI JITIHADA DAR ES SALAAM)**

WAZAZI wana mchango mkubwa katika maendeleo ya watoto wao shuleni, lakini baadhi yao mchango wao ni mdogo sana, kwani huwakatisha tamaa kwa kujitolea mifano wao wenyewe na kwa misemo yao kwamba 'Hisabati ni baba mkwe' kwa vile wao hawataki kujihusisha na somo hilo.

Wazazi wa aina hii ndio wale wanaowachagulia watoto wao masomo. Utaratibu huu haujakaa vizuri, kwani unaweza kuchangia kukwamisha maendeleo ya mtoto kielimu. Jambo la muhimu ni kwamba wasaidie kuwezesha watoto wao kumudu somo hili.

Ninajua wanafunzi wengi wamekuwa wakilikimbia, kwasababu wameshakaririshwa kuwa ni gumu na kwa sababu wanaosema ni wazazi, maana yake ni kwamba ni lazima mtoto ataamini hiyo, kwa kuwa aliyesema ni mzazi wake.

Huu ni upotoshaji wa hali ya juu, sikubaliani nao kabisa. Siyo vizuri mtu ambaye mtoto anamtegemea, halafu anakuwa wa kwanza kumpotosha.

Hakuna kisichowezekana chini ya jua, jambo la msingi ni kujiwekea malengo tu mwisho wa siku yaweze kutimia. Ila wazazi wana nafasi kubwa katika kuhakikisha wanazingatia hilo.



**LEONARD MBANGILE (MKAZI WA DAR ES SALAAM)**

MSINGI mzuri wa elimu kwa mtoto unaanzia nyumbani, kwa hiyo sisi wazazi tuna wajibu wa kuhakikisha tunajua maendeleo ya watoto wetu na kama kuna tatizo tuwasaidie siyo kuwafokea bali kuwatia moyo.

Kumfokea ni sawa na kumtoa kwenye mstari. Inawezekana mzazi hajui vizuri somo hilo, lakini ana wajibu wa kumuhimiza mtoto wake kulipenda na hata kumtafutia masomo ya ziada, ili aweze kujiendeleza na hatimaye kuijua vizuri Hisabati.

Lakini wanafunzi nao wanapaswa kuliona somo hilo kuwa ni kawaida kama yalivyo mengine, wajiamini na kufanya mazoezi mara kwa mara. Woga na kutojiamini ni sababu mojawapo inayowafanya wasijiamini, wawapo katika maandalizi ya mtihani au jaribio lolote lile la somo la Hisabati.

Wajenge fikra na imani kuwa wanaweza hata kama huwawezi kupata maswali yote, lakini ninaamini yapo watakayoyafanya vizuri. Wanafunzi wa sasa wakumbushwe haka 'ka-wimbo' kanakosema hivi: "Hesabu ni nzuri sanaeee, hesabuu ni sana nzuri eee... E mwalimu e - mwalimu tufundishe."

Njia hii ilitumika kuhamasisha wanafunzi kupenda somo hili. Sidhani kama wanafunzi wa sasa 'wana- kajua' 'kawimbo' haka, wafundishwe kwani kanaweza kuwaondolea hofu katika somo hilo.



**ISSAH NJINJO (MWALIMU, MKAZI WA RUANGWA LINDI)**

HISABATI siyo somo rahisi, kwa kuwa ni sayansi na somo lolote la sayansi ni gumu, kwa sababu linahitaji udadisi wa hali ya juu. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na bidii na maarifa, ili kuwa na uelewa mkubwa wa kujua vitu vingi ili aweze kufaulu somo hili.

Vilevile, linaweza kuwa rahisi kwa kujumlisha na kutoa, lakini ikumbukwe kuwa kuna maswali, ambayo mwanafunzi anaweza kupewa akatumia muda hata wa nusu saa kufikiria kabla ya kulifanya. Pamoja na ugumu wake, ninaomba niwatie moyo wanafunzi kwamba wazidi kuongeza bidii ili waweze kulijua vizuri, kuliko kukataa.

Wapo wanafunzi waliokaririshwa ni gumu na hawataki kuthubutu kulifanya. Huu ni mtazamo hasi unaotakiwa kuachwa.

Wazazi wawatie na wawajengee mazingira ya kupenda Hisabati tangu wakiwa madarasa ya chini. Wasisitiziwe kuwa somo hilo siyo la kushindikana na wasaidiane na walimu kuwapa msingi mzuri tangu mwanzo, watafika madarasa ya juu wakiwa tayari wana uelewa wa kutosha kwenye somo hilo, ambalo ni rahisi kama watakuwa wameandaliwa vizuri.







## CCM wamwangukia Rais Magufuli

**Na Mwandishi Wetu, MBARALI**

WANACHAMA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika Kata ya Igurusi Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamemwomba Rais Dk. John Magufuli, kuingilia kati ujenzi wa bwawa la umwagiliaji la Lwanyo ambalo limechukuwa muda mrefu bila kukamilika.

Bwawa hilo limejengwa kwa zaidi ya miaka mitano, lakini bado wananchi hawajanufaika huku likidaiwa kuwa limejengwa chini ya kiwango hali inayohatarisha maisha ya wakazi wa mji wa Igurusi endapo litabomoka.

Aidha, bwawa hilo lilitakiwa kujengwa na serikali kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa Kata za Igulusi na Utengule – Usangu kwa ajili ya umwagiliaji wa zao la mpunga.

Wakizungumza kwenye mkutano mkuu wa kata wa CCM, baadhi ya wanachama wa chama hicho walimwomba Rais Magufuli aingilie kati ili mradi huo ukamilike haraka na wananchi waanze kunufaika.

Mwenezi wa CCM Kata ya Igurusi, Pir Ibrahim, alisema bwawa hilo linajengwa kwa zaidi ya miaka mitano bila kukamilika na kwamba diwani wa kata hiyo alijitahidi kutekeleza ilani, lakini bado kuna changamoto ya bwawa la umwagiliaji la Lwanyo, ambalo likikamilika litaongeza uzalishaji wa zao la mpunga na vitunguu.

"Tumeona juhudi za viongozi wetu katika kufuatilia ubora wa bwawa hili, kama kuna ubadhirifu basi wahusika wachukuliwe hatua, mbona Rais Magufuli amesaidia maeneo mengine kuwatumbua mafisadi? Tunaomba aje na huku ili wananchi tunufaike na mradi wa bwawa hilo," alisema Ibrahim.

Diwani wa Kata ya Igurusi, Hawa Kiwele, alisema katika kata yake ametekeleza ilani kwa asilimia 90 kwa kuwasogezea sogeza huduma muhimu wananchi ikiwa ni pamoja na sekta ya afya.

Bwawa la umwagiliaji la Lwanyo linadaiwa kuwa na zaidi ya miaka mitano tangu ujenzi wake uanze bila kukamilika, huku ikidaiwa kuwa zaidi ya shilingi bilioni 3 zimeteketea na kwamba lilikuwa likisimamiwa na Wizara ya Maji kupitia Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji Mbeya.



# Naibu Waziri aagiza gereza kulima ekari 1,000 za mahindi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, ameuagiza uongozi wa Gereza la Kilimo la Songwe mkoani Mbeya kuhakikisha unatimiza lengo walilopewa na serikali la kulima ekari 1,000 za mahindi mwaka huu.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara katika gereza hilo kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa agizo hilo, ambapo alisema gereza hilo ni miongoni mwa magereza 10 nchini yaliyoteuliwa na serikali kwa ajili ya uzalishaji wa chakula.

Alisema pamoja na gereza hilo kupewa lengo hilo kwa muda mrefu, lakini utekelezaji wake bado haujafikia asilimia 100 kwa madai kuwa mpaka sasa wamelima ekari 750 pekee.

Masauni alisema lengo la serikali kutoa agizo hilo ilikuwa ni kuhakikisha magereza yanajitegemea kwa chakula na kuipunguzia serikali gharama za uendeshaji wa magereza hizo hasa kuwalisha wafungwa.

"Fanya kila linalowezekana ila mwaka huu ni lazima mmalizie hizo ekari 250 zilizobakia katika msimu huu wa kilimo, Mheshimiwa Rais aliagiza wafungwa watumike katika shughuli za uzalishaji wa chakula chao wenyewe," alisema Masauni.

Hata hivyo alisisitiza kuwa pamoja na kuwatumia wafungwa ni lazima zitumike na mbinu zingine ili kuendana na msimu wa kilimo hasa kwa miaka ijayo.

Mkuu wa Gereza hilo, Mrakibu Mwandamizi wa Magereza Peter Anathory, alisema walishindwa kufikia lengo kutokana na kuharibika mara kwa mara kwa vifaa vya kulimia hasa matrekta ambayo ni ya muda mrefu na yamechakaa.

Alisema gereza hilo lina matrekta matatu ambayo mawili ni ya zamani na moja pekee ndio jipya, hivyo ufanisi wa kazi ulikuwa mdogo na hivyo msimu ukaisha kabla hawajafikia lengo.

Alisema kwa sasa wanaendelea na maandalizi ya kukamilisha ekari 250 zilizobaki kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo ambalo liko karibu na maji.

Anathory alisema pamoja na kwamba serikali imeagiza wafungwa ndio watumike kwenye uzalishaji, lakini wao waliamua kujiongeza kwa kutumia matrekta kwa madai kuwa wangeamua kuwatumia wafungwa pekee wasingefikia hata hizo ekari 750.

"Mheshimiwa Naibu Waziri, huku kwetu Mbeya, msimu wa kilimo huisha Desemba 30 kwa hiyo tungetaka kuwatumia wafungwa pekee tusingeweza kufikia hata hizi ekari 750, lakini lengo letu ni kuhakikisha tunatimiza lengo kwa kutumia umwagiliaji," alisema Anathory.

Hata hivyo alisema baadhi ya maeneo wanayokusudia kuyatumia yalikuwa yanatumika na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Uyole ya jijini Mbeya (Tari- Uyole) na hivyo kwa sasa wameisimamisha taasisi hiyo na kwamba maeneo mengine walikuwa wamelima maharage.

Alisisitiza kuwa wanakusudia kumwagilia ekari zote 250 ambazo wameanza maandalizi ikiwamo kuwatumia wafungwa kusafisha mfereji wa maji kutoka kwenye chanzo mpaka mashambani.



Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi Benki ya NMB, Omari Mtiga, akizungumza jambo wakati wa halfa ya kukabidhi madawati 60 na viti 30 kwa Shule ya Sekondari ya Kata ya Kibinda Chalinze mkoani Pwani. Wa kwanza kulia ni Meneja wa tawi la benki ya NMB, Turiani, Aneth Matolo, Meneja wa benki ya NMB Kanda ya Mashariki, Baraka Ladislaus na Diwani wa Kata ya Kibinda, Mkufya Mfikilwa.

# Sherehe za Mei Mosi kufanyika Mbeya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

SHEREHE za maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, maarufu kwa jina la Mei Mosi, mwaka huu, zimepangwa kufanyika kitaifa mkoani Mbeya na Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dk. John Magufuli anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo juzi, wakati wa kikao cha kwanza cha maandalizi ya sherehe hizo kilichofanyika jijini Mbeya kikiwahusisha viongozi wa kitaifa wa Shirikisho la Wafanyakazi nchini (Tucta) na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa.

Chalamila alisema Rais Dk. Magufuli amekubali kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo mwaka huu, yatakayofanyika kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya, jambo ambalo alidai kuwa ni heshima kubwa kwa Mkoa wa Mbeya.

"Tunawashukuru Tucta kwa kupanga maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kufanyika kitaifa mkoani Mbeya na tayari Rais Dk. Magufuli amekubali kuwa mgeni rasmi, hii ni heshima kubwa kwa mkoa wetu," alisema Chalamila.

Chalamila alisema kuwa kutokana na uwepo wa Rais Magufuli mkoani Mbeya, siku hiyo ni muhimu sana kwa wananchi wa Mbeya kuitumia kama fursa kubwa ya kiuchumi na kujenga uhusiano mzuri kitaifa.

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (Tucta), Tumain Nyamhokya, alisema kuwa ili maadhimisho hayo yafanikiwe ni lazima viongozi wote kila mmoja ashiriki katika maandalizi.

Alisema kutokana na uwepo wa Rais kwenye maadhimisho hayo, hakutakuwapo na maadhimisho ya Mei Mosi katika kila wilaya mkoani Mbeya na badala yake wilaya zote zitaungana kwenye maadhimisho ya kitaifa yatakayofanyika jijini Mbeya.

"Maandalizi ya Mei Mosi mwaka huu mkoani Mbeya ambako ndiko yanafanyika kitaifa inabidi yawe ni ya pamoja, kama ni michango, ikusanyeni huko kwenye wilaya zenu na kuileta ili tuunganishe nguvu, kama Rais atakuwapo hapa Mbeya sitarajii kila Mkuu wa Wilaya aadhimishe kivyake wilayani kwake, bali wote mnatakiwa kujumuika na Rais kwenye maadhimisho ya kitaifa," alisema Nyamhokya.

Rais Magufuli kama atakuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Mei Mosi mkoani Mbeya mwaka huu, itakuwa ni mara yake ya kwanza kutembelea mkoa huo wa Mbeya tangu alipochaguliwa kuwa Rais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.





# Kampeni ya unywaji kistaarabu yatinga Dodoma

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imeendesha kampeni yake ya unywaji kistaarabu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani jijini hapa, huku madereva wakinufaika na vifaa vya usalama barabarani.

Kampeni hiyo maarufu kama 'Usinywe na Kuendesha chombo cha moto' imelenga kuwafikia watu 1,000 wakiwamo madereva hususan bodaboda, wanafunzi wa vyuo pamoja na umma kwa lengo la kutoa elimu juu ya unywaji kistaarabu ili kupunguza ajali zitokanazo na ulevi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo uliofanyika jijini hapa, Mkurugenzi wa Uhusiano wa SBL, John Wanyancha, alisema kampeni hiyo imelenga kutoaji elimu kwa wateja wake nchini ili kupunguza matukio yanayoepukika kama ajali zitokanazo na unywaji wa pombe kupindukia.

"SBL imejizatiti katika kuunga mkono juhudi za serikali, watu binafsi, wadau na kampuni kuhakikisha kwamba jamii hasa madereva ambao kwa kiasi kikubwa ndiyo waathirika wa ajali zitokanazo na ulevi, wanazingatia unywaji kistaarabu kwa usalama wao na abiria," alisema Wanyancha.

Kampeni hiyo inashirikisha wadau mbalimbali ikiwamo Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra), madereva bodaboda pamoja na jamii kwa ujumla ikilenga katika kupunguza ajali zitokanazo na ulevi wa kupindukia nchini. Kwa upande wake, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Dodoma, Nuru Selemani, alisema kampeni hiyo ni chachu katika kupunguza ajali, huku akiwataka madereva kuzingatia elimu iliyotolewa ili kuongeza usalama wao wawapo barabarani.

"Kulishirikisha Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, kunaonyesha ni kwa jinsi gani SBL wanatilia maanani suala zima la usalama barabarani hasa matokeo ya ulevi na uendeshaji vyombo vya moto. Uzoefu unaonyesha kwamba baadhi ya watu hujisahau na kujiingiza katika ulevi wa kupindukia bila kuzingatia usalama wao na vyombo vya moto wanavyoendesha," alisema.

RTO aliwataka madereva kutumia makoti hayo ipasavyo kila wanapokuwa katika majukumu yao ya kila siku kwa usalama wao, abiria na watumiaji wengine wa barabara. Kwa mujibu wa ripoti za Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwa mwaka 2018, jumla ya ajali 876 za bodaboda ziliripotiwa kutokea na kusababisha vifo 366 na majeruhi 694. Ripoti zinaonyesha kupungua kwa ajali hizo ambapo kwa mwaka 2017 zilikuwa 1,459 zilizosababisha vifo 728.

Ili kupambana na ajali hizo, SBL imekabidhi jumla ya makoti ya usalama barabarani (Reflectors) 80 kwa madereva bodaboda ili kuhimiza uzingatiaji wa sheria za usalama barabarani.

# Uharibifu wa miundombinu waleta hasara ya mil. 371/-

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAKALA wa Barabara mkoani Dodoma (TANROADS), umesema katika mwaka wa fedha 2018/19, umepata hasara ya Sh. milioni 371.7 kutokana na uharibifu wa miundombinu ya barabara.

Akiwasilisha jana mpango wa utekelezaji wa miradi ya barabara zilizo chini ya Tanroads katika kikao cha Bodi ya Barabara mkoani hapa, Mhandisi Leonard Chimagu, alisema wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya wizi wa alama za barabarani na uharibifu wa samani za barabara.

Alifafanua kuwa pia uegeshaji holela wa magari makubwa kandokando ya barabara unasababisha kukatika kwa kingo za barabara na kuisababishia hasara kubwa.

"Wizi wa alama za barabarani 30 hadi Januari 2019, umesababisha hasara ya Sh.milioni 10.5, wakati uharibifu wa mabega ya barabara unaotokana na uegeshaji holela umesababisha hasara ya Sh.milioni 361.2 na hadi sasa kuna maeneo hayajatengenezwa," alisema.

Hata hivyo alisema uegeshaji holela magari makubwa linachangiwa na polisi kwa kuhama hama wanapofanya ukaguzi na kusimamisha magari pembezoni mwa barabara.

Meneja huyo alisema serikali za vijiji zimeshirikishwa kwenye ulinzi wa miundombinu na samani nyingine za barabara ili kuhakikisha kuwa wezi hawapati mwanya wa kuiba au kuharibu miundombinu ya barabara.

"Tunapenda kutoa wito kwa wenzetu polisi kuainisha maeneo mawili au matatu kwa kila barabara ambayo yatatumika kufanya ukaguzi wa magari ili tuweze kuimarisha kingo maalum kwa ukaguzi," alisisitiza.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Binilith Mahenge, aliagiza kushirikishwa viongozi wa ngazi za vijiji na kata kukabiliana na wafugaji ambao wamekuwa wakipitisha mifugo na kuharibu barabara. Alisema ili barabara ziweze kudumu kuna umuhimu wa kudhibiti upitishaji mifugo na kutaka utaratibu uliokuwapo awali usimamiwe.

"Serikali za vijiji na kata zikashirikishwe suala hili na nyie Tarura na Tanroads mkasimamie hili, lakini mwashirikishe wananchi mnapoweka hizo alama za kuvusha mifugo," alisema.

Akichangia katika kikao hicho, Mbunge wa Jimbo la Mtera, Livingstone Lusinde, alisema ni vyema Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) na Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) kuhakikisha alama za uvushaji mifugo barabarani zinawekwa kwa kushirikisha wananchi.

"Maana inawezekana unaweka kibao sehemu nyingine ambayo mfugaji analazimika kutembea umbali mrefu ndio afikie kibao cha kuvusha, ni muhimu mliangalie hili mkaviweke kulingana na mazingira," alisema.




Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Dodoma, Nuru Selemani (kushoto), akijadiliana na Mkurugenzi wa Uhusiano wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), John Wanyancha (katikati), na mmoja wa maofisa wa usalama barabarani baada ya kuzindua kampeni ya unywaji kistaarabu iitwayo 'Usinywe na Kuendesha' uliofanyika mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkutano wa SADC kufanyika nchini Septemba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, Profesa Paramagamba Kabudi, ameliagiza Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo kuanza maandalizi ya mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), utakaofanyika Septemba mwaka huu nchini.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Profesa Kabudi alisema wanatakiwa kuanza maandalizi mapema ili kutowaangusha Watanzania kulingana na ukubwa wa mkutano huo.

"Naomba muanze maandalizi mapema maana Septemba siyo mbali kulingana na ukubwa wa mkutano huo," alisema.

Alisema anahitaji kuona kila kitu kinakwenda sawa baada ya kuwapa agizo hilo, huku akisisitiza kwamba hataki kuona baraza hilo linashindwa kufanya maandalizi ya mkutano huo.

Alisema kwa miaka yote serikali imekuwa ikisisitiza taasisi kujenga na kutekeleza utaratibu wa kuwashirikisha watumishi, kwa sababu ushirikishwaji wao kwenye mipango ya wizara unaongeza umiliki wa mipango iliyowekwa kwa ajili ya kusaidia kupata mawazo.

Alilitaka baraza kuwa mshiriki mkubwa katika kubuni mbinu mpya za utekelezaji na namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza na siyo kusubiri mtu mwingine aje kutatua changamoto hizo.

Alisema baraza hilo lisifanye kazi ya kupokea malalamiko tu kutoka kwa wafanyakazi, bali liwe ni chombo cha kuweka mazingira mazuri yatakayowafanya watumishi kutimiza majukumu yao vizuri na kikamilifu.

Alifafanua zaidi kuwa katika kutekeleza bajeti ijayo, lazima wakumbuke vipaumbele vya serikali na kuhimiza watumishi kujituma, kuondokana na uzembe, na vitendo vyovyote vya rushwa mahala pa kazi.

Profesa Kabudi aliagiza kuzingatia misimamo wa serikali wa kubana matumizi yasiyo ya lazima ili kuongeza tija.



# ACT-Wazalendo yavuruga vichwa viongozi wa CCM

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewaonya baadhi ya viongozi wa kisiasa wanaotumia vibaya uhuru wa kidemokrasia kuhatarisha hali ya amani ya nchi.

Viongozi wa kisiasa wa ACT-Wazalendo na CUF wametakiwa kutotumia mipasuko na migogoro ya ndani ya vyama vyao kuhatarisha hali hiyo ya amani na kwamba Wazanzibar na Watanzania hawapo tayari kuingia katika machafuko ya kisiasa kwa sababu ya maslahi binafsi ya watu wachache.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi, aliyasema hayo wakati akizungumza katika kikao cha ndani cha chama hicho kilichoambatana na hafla ya kukabidhi gari kwa uongozi wa Jimbo la Magomeni mjini Unguja lililotolewa na Mbunge wa Jimbo hilo, Jamal Kassim Ali.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema CCM haina muda wa kushughulikia sera za vyama vingine na kwamba itaendelea kusimama imara na kupaza sauti inapoona baadhi ya watu wachache wanaovunja sheria za nchi kwa makusudi bila ya kujali misingi ya utu na haki za binadamu.

Alisema kuwa mpasuko wa kisiasa ulioko baina ya viongozi wa CUF na ACT-Wazalendo baada ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Seif Sharif Hamad, kufukuzwa ndani ya chama hicho na kujiunga na ACT-Wazalendo baadhi ya wafuasi wa chama hicho wamefanya vitendo vya uvunjifu wa sheria kwa makusudi.

Dk. Mabodi alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuchukua hatua stahiki mapema, kwa kuwa dhana ya hali ya amani na utulivu wa nchi haviuzwi katika maduka kama bidhaa bali imeletwa na sera bora za CCM. Alisema nchi zilizoingia katika machafuko ya kisiasa na vita vya wenyewe kwa wenyewe zilianza taratibu, huku taasisi na mamlaka zenye dhamana ya ulinzi na usalama zikipuuza kuchukua hatua katika hali hizo na badala yake mataifa hayo yamejikuta yakiingia katika vita hivyo kwa kipindi cha muda mrefu.

Alisema kuwa CCM itaendelea kushindana kwa sera za maendeleo na kuwapelekea wananchi mahitaji muhimu ya msingi na si kujiingiza katika siasa za ubabe na uharibifu wa mali za umma.

"Wito wangu kwa viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa nchini, tuwaongoze na kuwaelekeza mambo mema wanachama wetu, kwa kuwajengea mazingira ya kuamini ushindani wa sera na badala ya siasa za ovyo na machafuko," alisema Naibu Katibu Mkuu huyo.

Aidha, alimtaka Msajili wa Vyama vya Siasa, kuchukua hatua za haraka za kuhakikisha chama kinachovunja sheria na katiba za nchi wachukuliwe hatua za kisheria.

Pia, alimtaka msajili huyo wa vyama vya siasa kufanya uhakiki wa michango ya fedha za wahanga wa mafuriko Zanzibar zilizokuwa zikichangishwa na viongozi wa CUF chini ya Seif Sharif Hamad na kutolewa ufafanuzi wa kina juu ya matumizi yake kama ziliwafikia walengwa.

Naibu Katibu Mkuu huyo alieleza kuwa wananchi wanapaswa kupuuza kauli za Seif Sharif Hamad za kudai kuwa migogoro ya vyama vyao inachochewa na serikali jambo ambalo si kweli bali anaendeleza ulaghai na siasa za fitina.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Magomeni, Jamal Kassim Ali, alisema gari hiyo aliyoitoa imegharimu Sh. milioni 29.5 ni miongoni mwa sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM kwa kuwaondoshea kero za usafiri wananchi wa jimbo hilo.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu ametatua kero za ukosefu wa majisafi na salama kwa kuchimba visiwa tisa ambavyo vinatoa huduma ya majisafi na salama katika maeneo ya shehia zote za jimbo hilo.

Mbunge huyo aliongeza kuwa kwa kushirikiana na Mwakilishi wa Jimbo hilo wameanzisha kituo cha mafunzo ya amali kinachotoa mafunzo ya ujasiriamali na ufundi kwa vijana wa jimbo hilo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitizama mihogo inavyopita kwenye mashine baada ya kuzindua kiwanda cha unga wa muhogo cha Kampuni ya Cassava Starch of Tanzania Corporation mkoani Lindi wikiendi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bidhaa za China, Dubai zateketezwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAKALA wa Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA) umeteketeza samaki tani 106 aina ya peduu walioingizwa Zanzibar kutoka China na maziwa tani 23 kutoka Dubai baada ya kubaini vimeharibika na kukosa sifa kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

Samaki hao waliokuwa kwenye makontena manne waliingizwa na kampuni ya Drive Shark na kontena moja la maziwa kutoka Dubai lililetwa na mfanyabiashara Yunus Hashim.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kuangamiza bidhaa hizo katika kijiji cha Kibele, Ofisa Uhusiano wa ZFDA, Abdulmatin Yassin, alisema samaki hao waliharibika baada ya kukosa barafu wa uhakika kwenye makontena.

Alisema kukosekana kwa umeme kwenye makontena yalipofika bandarini Zanzibar kulisababisha kupungua barafu iliyogandisha samaki na kuanza kuharibika.

Abdulmatin alisema samaki wanapoingizwa nchini huwa wameganda na hutakiwa waendelee kubakia katika barafu wakati wote, lakini wakati makontena yakisubiri taratibu za uingizaji palitokea kasoro na kusababisha samaki kuharibika.

Alisema kwa upande wa bidhaa ya maziwa, yaliharibika baada ya baadhi ya maboksi kupasuka wakati yakisafirishwa kutoka Dubai kuja Zanzibar.

Mkuu wa Kitengo cha Uchunguzi wa Athari Zitokanazo na Chakula wa Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar, Aisha Suleiman, alisema samaki aina ya peduu wanaoingia nchini kutoka nje ni salama kwa matumizi ya binadamu lakini umakini unahitaji wakati wa kuwasafirisha na wanapofika bandarini.

Aliwataka wananchi wanaponunua samaki wanaoingizwa nchini kuwa waangalifu na wahakikishe wameganda kwenye barafu na wasiwaweka muda mrefu kabla ya kuwapika ama waendelee kuwaweka katika barafu.

Aidha, aliwashauri wafanyabiashara kufuata taratibu zote za kuingiza bidhaa nchini na kutafuta bidhaa zenye ubora uliowekwa na Bodi ya Chakula na Dawa Zanzibar ili kujiepusha na gharama zisizokuwa za lazima.

Kwa upande wake mkuu huyo wa kitengo cha uchunguzi wa athari zitokanazo na chakula wa ZFDA amewahakikishia wafanyabiashara kwamba bodi hiyo haina nia ya kuwakandamiza kutokana na kazi nzuri wanayofanya, lakini lengo ni kulinda afya za wananchi kwa kuhakikisha wanapata bidhaa zilizo salama.

## Naibu msajili wa vyama vya siasa akemea vurugu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa imevitaka vyama vya siasa wakiwamo wanachama na mashabiki wa vyama hivyo, kufanya siasa za kistaarabu na kimaendeleo ili kudumisha amani na umoja.

Akizungumza na waandishi wa habari, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Mohamed Ali, amesema kuwa ofisi hiyo haitasita kuchukua hatua stahiki kwa chama chochote ama mwanachama atakayekiuka sheria za nchi hasa zile zinazosimamia vyama vya siasa bila ya kujali ukubwa au umaarufu wa chama.

Aliwataka wananchi na wafuasi wa vyama hivyo kutokubali kudanganywa na kiongozi au mwanachama yoyote wa chama cha siasa katika kuvunja sheria.

"Nachukua nafasi hii pia kuwaomba viongozi wa dini kuwaasa waumini wao kujizuia kutumia imani zao za dini kwa malengo ya kujinufaisha kisiasa, ili kuepusha kuliingiza taifa letu kwenye mgawanyiko na migogoro isiyo na tija," alisema.

Aidha, alieleza katika hali isiyotarajiwa baada ya tamko la msajili wa vyama vya siasa kukemea vitendo vya uvunjifu wa sheria kuna baadhi yao pamoja na wafuasi wao ambao watuhumiwa kutenda makosa hawakuonekana kujutia ama kukemea vitendo hivyo.

Alieleza kuwa baada ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF kuingia ACT- Wazalendo baadhi ya wafuasi wake walionekana kufanya vitendo vya kihalifu.

Aidha, alieleza kwamba masuala ya kutumia dini au ukabila katika harakati za kisiasa katika Tanzania halijawahi kupewa nafasi na waanzilishi wa taifa marehemu Julias Nyerere na marehemu Abeid Amani Karume.

Alieleza kuwa sheria ya vyama vya siasa inakataza chama chochote cha siasa kutumia dini kufikia malengo yake kwa kuwa marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa ya mwaka 2019 imesisitiza suala hilo kwa kukataza hata wanachama binafsi kufanya hivyo.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 25 March**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 26 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 27 March**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 28 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 29 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 30 March**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 31 March**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima — WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 25 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 26 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 27 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 28 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 29 March**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 30 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 31 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


5 EATV

NIRVANA

LEO USIKU SAA 3:00

JUMANNE
11:00 DADAZ (live)
13:30 Kali Za Wana
14:00 Dakika10 Za Maangamzi
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Nirvana
21:30 Wakilisha
22:00 Grace Na Asili Yangu
22:30 Bongo Hits



**NIRVANA** *ni kipindi cha kisasa kinachoongelea mitindo, sanaa, urembo na staili za maisha. **NIRVANA** inawalenga wale wanao ongoza kuonyesha mitindo mipya kwenye jamii na wale wanaofuatilia*

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One — WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

# Mkenya ashinda tuzo ya mwalimu bora duniani

**DUBAI, Falme za kiarabu**

MWALIMU Peter Tabishi ambaye ni mtaalamu wa masomo ya hisabati na fizikia kutoka Shule ya Sekondari katika kijiji kinachopatikana eneo la bonde la ufa nchini Kenya, ameshinda tuzo ya mwalimu bora mwaka 2019 ulimwenguni.

Tabichi, ambaye anatoka katika Shirika la kidini la Francisco, alishinda tuzo ya dunia ya mwaka 2019 ya mwalimu bora na amepewa zawadi ya Dola za Marekani milioni moja, baada ya kuwapiku washiriki wengine 10,000 waliochaguliwa kutoka nchi 179.

Peter amesifiwa kwa mafanikio yake katika shule yenye madarasa yenye watoto wengi pamoja na vitabu vichache.

Anasema ndoto yake kubwa ni kuwaona wanafunzi wake wakipenda masomo ya sayansi.

Tuzo hiyo ilitangazwa katika sherehe iliyofanyika mjini Dubai, ambapo alitambuliwa kama mwalimu aliyejitolea kufanya kazi isiyo za kawaida kwa watoto katika eneo lisiloweza kufikiwa kwa urahisi la bonde la ufa nchini Kenya.

Waandaaji wa shindano hilo wameeleza kuwa Mwalimu Tabishi amekuwa akitoa asilimia 80 ya mshahara wake wa mwezi kwa wanafunzi maskini katika shule ya kutwa ya sekondari ya wasichana na wavulana ya Keriko iliyopo katika kijiji cha Pwani Village, Jimbo la Nakuru, ambao vinginevyo wasingeweza kupata sare za shule na vitabu.

Amepokea tuzo hiyo katika sherehe iliyofanyika siku ya Jumamosi huko mjini Dubai, ambayo mwenyeji wake alikuwa nyota wa filamu kutoka Hollywood, Hugh Jackman.

"Kila siku barani Afrika tunafungua ukurasa mpya wa maisha. Tuzo hii haitambui mimi bali inawatambua vijana wa bara hili. Nipo hapa kwa sababu ya kile ambacho wanafunzi wangu wamefanikiwa katika maisha yao, la muhimu si pesa," alisema Tabishi baada ya kupokea tuzo.

Alisema tuzo hiyo inawapa wao fursa, pia inaueleza ulimwengu kwamba wanaweza kufanya kitu chochote.

Mwalimu Tabishi alisema ametwaa tuzo hiyo baada ya kuwashinda walimu wengine tisa kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu waliofanikiwa kufika fainali kuwania tuzo hiyo ya mwalimu bora.

Anaeleza kuwa anataka kuwa mfano na kusaidia na kuinua sayansi siyo kwa Kenya tu bali barani Afrika.

"Kama mwalimu ninayefanya kazi nao, nimeona matumaini ya yale ambayo wanaweza kuyafanya, udadisi wao, vipaji, uwezo wao wa kiakili na imani yao. Vijana wa Afrika hawatabakizwa nyuma na matarajio ya chini, Afrika itaweza kutoa wanasayansi, wahandisi, wajasiriamali, ambao majina yao yatakuwa miongoni mwa watu maarufu katika kila kona ya dunia. Na wasichana watakuwa sehemu kubwa ya historia hii," alisema Tabishi.

Tabishi ni Mtawa wa Shirika la Mtakatifu Francisco, la dini ya Katoliki lililoanzishwa na Mt. Francis wa Assisi katika karne ya 13.

*DW*



Mwalimu Peter Tabichi (katikati), akiwa na muigazaji wa filamu Hugh Jackman (kushoto), mrithi wa mfalme wa Dubai, mwanamfalme Sheikh Hamdan bin Mohammed Al Maktoum (kulia), baada ya kushinda tuzo ya mwalimu bora. **PICHA: ALLIANCE**

# Urusi yatuma ndege za kivita Venezuela

**MOSCOW, Urusi**

NDEGE mbili za kijeshi za Urusi juzi, zilitua katika Uwanja Mkuu wa Ndege wa Venezuela zikiwa na idadi kubwa ya wanajeshi pamoja na kiwango kikubwa cha silaha.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la Habari la Urusi la Sputnik limesema kuwa ndege hizo zilitumwa kutekeleza mkataba wa kijeshi wa kiufundi.

Mwandishi wa habari wa Venezuela, Javier Mayorca, aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter kwamba aliona wanajeshi wapatao 100 na tani 35 za vifaa vya kijeshi vikishushwa kwenye ndege.

Mayorca aliandika kuwa ndege ya kijeshi ya Urusi ya mizigo Antonov-124 na ndege ndogo aina ya Jet zilitua karibu na mji mkuu Caracas Jumamosi.

Alieleza kuwa Generali wa Urusi, Vasily Tonkoshkurov, aliwaongoza wanajeshi hao walipokuwa wakitoka ndani ya ndege.

Hali hiyo imetokea ikiwa imepita miezi mitatu baada ya nchi hizo mbili kufanya mazoezi ya pamoja ya kijeshi.

Urusi imekuwa mshirika wa muda mrefu wa Venezuela, ikiikopesha nchi hiyo iliyoko Amerika Kusini mabilioni ya dola na kusaidia sekta ya mafuta na jeshi.

Vilevile, Urusi imekuwa ikipinga hatua ya Marekani ya kuiwekea vikwazo serikali ya Rais wa Venezuela, Nicolás Maduro.

Uhusiano baina ya Moscow na Venezuela umeimarika katika miezi ya hivi karibuni, wakati uhusiano kati ya Marekani na Venezuela ukiwa mbaya zaidi.

Mwezi Desemba Urusi ilituma ndege za kijeshi aina ya Jet nchini Venezuela kama sehemu ya mazoezi ya kijeshi.

Urusi iliyalaani mataifa mengine ya kigeni kwa kumuunga mkono kiongozi wa upinzani wa Venezuela, Juan Guaidó, ambaye alijitangaza kama rais wa mpito mwezi Januari.

Rais Maduro amemshutumu Guaidó kujaribu kupanga mapinduzi dhidi yake kwa usaidizi wa Marekani.

Rais Maduro alipata ushindi kwa kura chache katika uchaguzi uliofanyika Aprili 2013 baada ya kifo cha aliyekuwa mshirika wake Rais Hugo Chávez.

Rais Maduro alichaguliwa kwa muhula wa pili Mei, 2018, katika uchaguzi ambao ulikosolewa sana na wakaguzi wa kimataifa.

Venezuela imekumbwa na mporomoko wa uchumi, huku uhaba wa chakula na mfumuko wa bei ukiongezeka.

Guaidó anamtuhumu Rais Maduro kuwa mtu asiyefaa kuwa Rais, na alipata uungaji mkono wa watu wengi nchini humo pamoja na viongozi wa Marekani na Muungano wa Ulaya.

Serikali ya Rais Maduro inaendelea kutengwa, huku nchi nyingi zikiilaumu kwa mzozo wa kiuchumi ambao umewafanya raia zaidi ya milioni tatu kuihama Venezuela.

Wakati huohuo, serikali ya Moscow imepanua ushirikiano na serikali ya Caracas katika miaka ya hivi karibuni, ikiongeza mauzo ya silaha na kuongeza zaidi mikopo kwa nchi hiyo.

*BBC*

## Waliofariki dunia kwa ebola Congo wafikia 1,000

**KINSHASA, Congo**

WIZARA ya Afya katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imesema idadi ya watu waliofariki kutokana na maradhi ya ebola nchini humo imefikia 1,000.

Waziri wa Afya, Oly Ilunga Kalenga, alisema pamoja na idadi hiyo ya vifo, mamia ya familia za Wacongo zinaendelea kuteseka na maradhi hayo hatari, huku pia idadi ya mayatima ikiongezeka.

Alisema mlipuko uliotokea hivi karibuni katika eneo la Mashariki mwa Congo umeua watu 629, lakini watu wengine 320 wamenusurika, watu 91,000 wameshapatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa huo tangu Agosti mwaka jana.

Maofisa wa Congo wamesema wafanyakazi wa mashirika ya afya wamefanya kazi katika mazingira magumu kuwahudumia waathirika katika shughuli zao Mashariki mwa Congo ambako kumetapakaa makundi yenye silaha.

*DW*

## Viongozi wa kijeshi Mali 'watumbuliwa'

**BAMAKO, Mali**

BAADA ya kutokea kwa mauaji ya zaidi ya watu 135 wa jamii ya Fulani katikati mwa nchi ya Mali, serikali ya nchi hiyo imetangaza kuvunja kundi la wanamgambo la Dan Nan Ambassagou na kuwaondoa wakuu kadhaa wa jeshi kwenye nafasi zao.

Waziri Mkuu wa Mali akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao cha Baraza la Mawaziri alisema kuwa kundi la wanamgambo la Dan Nan Ambassagou, lililoruhusiwa kumiliki silaha katikati mwa Mali limevunjwa.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mashirika kadhaa kundi hilo linaundwa na wanamgambo wanaowafanyia vitendo viovu watu wa jamii ya Fulani.

Vyanzo kadhaa kutoka nchini Mali vimeeleza kuwa kuna uwezekano wa wanamgambo hao kuhusika pia katika matukio ya Ogossagou, karibu na mji wa Bankass.

Washambuliaji waliokuwa wamevalia mavazi ya kijadi ya uwindaji wakiwa na silaha waliwaua watu zaidi ya 130 kwenye kijiji katikati mwa nchi ya Mali.

*RFI*

# Kamwele aagiza ripoti ya miradi kuandikwa upya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwele, ameiagiza ripoti ya miradi iliyoandikwa na Baraza la Uchukuzi na kuwasilishwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, iandikwe upya baada ya kamati hiyo kusema hairidhishi.

Akizungumza katika mkutano wa baraza hilo, Kamwelwe alisema amepewa taarifa na kamati hiyo kuwa ripoti hiyo ni mbaya haina ufanisi wowote kulingana na miradi hiyo.

"Naagiza ndani ya siku moja ripoti hizi ziandikwe upya, sitaki nishambuliwe na wabunge kwa sababu ya hii ripoti hakikisheni mnakesha kuiandika tena," aliagiza.

Kamwelwe alisema hakuna kilichofanyika kutokana na kamati hiyo kuiponda ripoti hiyo.

"Nataka baraza hili liwe na matokeo chanya na si kufurahia tu posho na nahitaji kuona kila anayesafiri analeta ripoti kwangu iliyoshiba," alisisitiza.

Naye, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Erick Mwakalinga, aliwataka washiriki kuwa makini na kile wanachojadili na si kubweteka.



Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Hamza Sadiki, akifungua warsha kwa waandishi wa habari ya kuwajengea uwezo juu ya uhifadhi wa vyanzo vya maji iliyofanyika Bagamoyo mkoani Pwani jana. Kulia ni Kaimu Ofisa wa Maji wa bonde hilo, Msunda Wilson. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Afungwa jela miaka 30 kwa kumpa ujauzito mwanafunzi

**Na Happy Severine,** MASWA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, imemhukumu kifungo cha miaka 30 mkazi wa Kijiji cha Igunya, Sunzu Mpangala (27), baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kumbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa sekondari.

Mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Tumaini Marwa, mwendesha mashtaka Inspekta Nassib Swedi, alidai kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo Juni 16, mwaka jana, majira ya saa 11 jioni huko katika kijiji cha Igunya Kata ya Shishiyu.

Swedi alidai kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa akimfundisha mwanafunzi huyo wakati wa likizo akiwa anasubiri ajira serikalini baada ya kuhitimu shahada ya elimu kutoka Chuo Kikuu cha UDOM.

Mwendesha mashtaka alidai kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu namba 60 A(3) cha Sheria ya Elimu Sura ya 353 kama ilivyofanyiwa marekebisho ya sheria ndongo namba 2 ya mwaka 2016.

Mtuhumiwa alipopewa nafasi ya kujitetea, alikiri kutenda kosa hilo na kuiomba mahakama ijaribu kumpunguzia adhabu kwa kuwa hana wazazi na anategemewa na familia.

Hata hivyo, Swedi alipinga hoja hiyo na kuiomba mahakama itoe adhabu kali kwa mtuhumiwa huyo ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama hizo kwa kuwa wamekuwa wakikatisha ndoto za wanafunzi.

I T V

JARIDA LA WANAWAKE: SAA 1:00 USIKU

Leo Blandina Sembu atakuwa na Rose Tesha mwanaharakati na pia Mkurugenzi wa TESHA ADD akizungumzia hasa jinsi ya kumsaidia mwanamke na watoto wenye ulemavu katika kupata haki zao na elimu jumuishi.

# Kiwanda cha kisasa kuzalisha tani 1 unga wa muhogo kwa siku

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya tani 6,000 za unga wa muhogo zinatarajiwa kuzalishwa kwa mwaka na kiwanda cha kisasa cha kuzalisha unga huo wenye kiwango cha juu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ulimaji na usindikaji muhogo ijulikanayo kama Gassava Starch of Tanzania Corporation (CSTC), Christophe Gallean, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani moja kila siku za unga huo.

"Tunafurahi kuanzisha rasmi kiwanda cha kwanza cha ubora wa hali ya juu na cha kisasa nchini Tanzania. Tunajivunia sana uwapo wa kiwanda hiki na taswira inayoipa kampuni yetu ya CSTC, Mkoa wa Lindi na Tanzania kwa ujumla. Tunashukuru sana kwa ushirikiano wa serikali chini ya uongozi wa Rais John Magufuli," Gallean alisema.

Alisema kiwanda hicho kilianzishwa miaka saba iliyopita kwa lengo la kuuza unga wa muhogo wenye ubora wa hali ya juu ndani ya nje ya nchi.

Alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kusafirisha bidhaa zake katika masoko muhimu duniani yakiwamo ya Afrika ya Mashariki na Kusini, Mashariki ya Kati, Marekani na Ulaya.

"Mfumo wa utendaji wa CSTC ni kukuza mazao yenye ubora wa hali ya juu katika mashamba makubwa yenye ufanisi na kusimamiwa na CSTC. Vilevile kusindika mazao yote katika kiwanda kilichopo eneo la karibu, mfumo huu wa utendaji unaofuatwa na CSTC wa kuzalisha mazao na kuwa na kiwanda cha usindikaji ni wa kipekee katika soko la unga wa muhogo la Afrika," alisema.

CSTC ilianza kufanya kazi mwaka 2012 nchini ikiwa na wafanyakazi zaidi ya 400 ambao kati yao asilimia 97 ni Watanzania.

"Tunaendelea kuongeza wafanyakazi, kutoa mafunzo na kuendelea kutoa fursa kwa vijana wengi za uongozi katika ngazi zote za uendeshaji kuanzia kiwandani, mashambani na katika shughuli za utawala," Gallean alisema.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MARIAM MMARIKA BUNGIRE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari **TOYOTA VITZ** yenye namba za usajili **T181 CVV** . Chassis namba **SCP100292262.** Engine namba **1SZfe 0237.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**WBM/RB/3711/2019.**

215138202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURI MDAIWA**
**MCA/6**

**Mahakama ya mwanzo: MALAMPAKA**
**Wilaya ya: MASWA**
**MADAI NAMBARI 1 YA 2019**
**MDAI : MOTO JULIUS**
**Amdai**
**Mdaiwa: ZENGO PUGUTE**
**Kwa: ZENGO PUGUTE**
**k.k M/KITI WA KITONGOJI**
**MWATIGI- BUKIGI**

Kwa kuwa mdaiwa ameleta madai yake kwamba **MDAI ANAMDAI MDAIWA TSHS. MILIONI MOJA LAKI TISA NA ELFU THEMANINI 1,980,000/= TU.**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya ALHAMIS tarehe 28.03.2019 saa 2.00 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukudhuria siku hiyo iliyotajwa hapo juu, mahakama ikitibitisha kama umepokea kuitwa shaurini katika mahakama hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa

Hati hii yatolewa na amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 15.03.2019.

215138302

**IN THE DISTRICT COURT OF NYAMAGANA**
**AT MWANZA**
**CIVIL/CRIMINAL APPEAL NO. 36 OF 2018**

**WITNESS FESTO..........................APPELLANT**
**DHIDI YA**
**ABDULMAJID MOHAMED........................RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTE THAT** the above case has been fixed for hearing/mention of the 27TH day of MARCH 2019 at 8:30 a.m. in the forenoon.

YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all documents upon which you intend to rely in support of your case.

GIVEN UNDER my hand and the SEAL of the court this 22 day of MARCH 2019.

215137802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 25/03/2019

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 27/03/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **BABATI kuelekea SAME** gari hilo lenye namba za usajili: **T827, BCN T741 CPB, T 985 ABJ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu -mita 17**
   **Upana -mita 3.0**
   **Kimo -mita 3.2**
3. Njia itakayotumika **BABATI hadi SAME kupitia ARUSHA MOSHI ROAD** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115138002

### KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**SALUMU HASSANI ONGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili **MC 751 BBJ (BAJAJ BOXER).** Chassis namba **MD2A21BZIEWD56765.** Engine namba **PFZWED10057.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**MAG/RB/11149/2018.**

115137102

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MGA/63)**

**Mahakama ya Mwanzo ya UJIJI**
**Wilaya ya KIGOMA**
**SHAURI LA MADAI NO. 14 LA MWAKA 2019**
**Mdai: RODRICK SAMWEL MADUHU**
**Amdai**
**Mdaiwa: LIGHTNESS JOSEPH MSAWIRA**
**Kwa: LIGHTNESS JOSEPH MSAWIRA WA DAR ES SALAAM**
**Kwa kuwa Mdaiwa/mdai ameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari ya Mdai)**

**MDAIWA UNADAIWA NA MDAI MADAI YA TALAKA NA MGAO WA MALI YA NDOA (MGAWANYO WA MALI) YA PAMOJA**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 07/04/2019 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 18/03/2019

115136702

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTMENT C. LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yenye namba za usajili **MC 725** BMT.Chassis namba **LBRSPJB54G9046662.** Engine namba. SL157FM116963685

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/94/2019.**

115136602

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.26 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late GERVAS ANDREA MICHAEL**
**Of Majengo within Dodoma city**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by MARIA HUSSEIN SAID**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before **15TH/04/2019.**
Dated at Dododma this ....22/03/2019

115136502

**IN THE DELIGATE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.24 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late RASHID MANG'ANA MARWA-DECEASED**
**AND**
**In the matter of the Application for letters of Administration by NEEMA GABRIEL MAJALIWA**

**GENERAL CITATION**

All person claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioners.

Objections to the grant should be filled on or before **10th /04/2019.**

The will if any of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

**Dated....21th/03/2019**

115136402

NJOO UTAN-GAZE BIDHAA YAKO

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie 0767 223 311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# KANTE akataa kutua Madrid

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa Chelsea, N'Golo Kante, amesisitiza kwamba anajiona kama ana muda mrefu zaidi wa kukaa hapo Chelsea, licha ya uvumi kuenea kwamba anahusishwa na mpango wa kuhamia Real Madrid.

Baada ya kuteuliwa tena Zinedine Zidane kama kocha mpya wa Los Blancos, jina la Kante limekuwa likihusishwa na mpango wa kuhamia kwenye dimba la Santiago Bernabeu mwishoni mwa msimu huu.

Taarifa za hivi karibuni zimeeleza kwamba mabingwa hao watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wamekuwa wakiwania kumsajili kiungo huyo, hasa baada ya kiwango cha Casemiro kushuka.

Hata hivyo, katika mahojiano na RTL, nyota huyo wa Blues hao, Kante amekanusha uvumi huo wa kujiunga na Madrid na kubainisha kwamba bado hajamaliza kazi pale Stamford Bridge.

Alisema: "Nipo hapa Chelsea na bado nina malengo ya kuendelea kukaaa hapa, kile kilichosemwa sehemu nyingine siyo muhimu.

"Hiyo sio muhimu. Nipo Chelsea hapa na nitaendelea."

Mfaransa huyo alisaini mkataba wa miaka mitano na miamba hao wa Ligi Kuu ya England Novemba mwaka jana.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia alikuwa na mwanzo mgumu wa msimu huu chini ya Maurizio Sarri.

## Liver wajiandaa kumuuza Keita

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imeripotiwa inajipanga kumuuza kiungo wake, Naby Keita (pichani chini), mwishoni mwa msimu huu, baada ya kushuka kwa kiwango.

Wekundu hao walikubali kumsajili Keita mwaka 2017, kutoka RB Leipzig, na hatimaye alijiunga hapo Anfield kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini ameshindwa kuimarisha kiwango chake.

Uwapo wa wachezaji kama Georginio Wijnaldum na Adam Lallana wamekuwa chaguo la kwanza mbele ya Keita, na hivyo kumfanya mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea kufikiria kuondoka.

Habari za kutaka kuondoka kwa Keita zimekuja baada ya taarifa kudai kwamba, kocha Jurgen Klopp amebainisha kuwa yupo tayari kuidhinisha kuondoka kwa mchezaji huyo.

Liverpool itakuwa tayari kumuachia mchezaji huyo kwa pauni milioni 10 ili aweze kufanya usajili wa wachezaji wengine.

Klabu kadhaa za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, zimetajwa kumuwania kiungo huyo.

Bayern Munich na Borussia Dortmund ndio klabu ambazo zimeingia kwenye mbio moja za kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

Baada ya kujiunga hapo Anfield kipindi cha majira ya joto, Keita alijikuta mwenyewe katika kikosi cha kwanza.

Hata hivyo, akajikuta kwenye wakati mgumu wa kushuka kwa kiwango chake na kuwa benchi.

Amecheza mechi 27 chini ya Klopp, lakini ametoa pasi ya mwisho moja tu na bado hajaweza kufunga.






## Giroud azungumzia kuondoka Chelsea

**LONDON,** England

OLIVER Giroud amefungua mlango wa uwezekano wa kuondoka katika klabu yake ya Chelsea ili aweze kupata klabu kucheza mara kwa mara.

Mshambuliaji huyo ameanza katika mechi sita tu za Ligi Kuu na kufunga bao moja chini ya kocha Maurizio Sarri msimu huu, lakini amebakia kuwa mshambuliaji chaguo la kwanza kwa kocha wa Ufaransa Didier Deschamps na alifunga kwenye ushindi wa 4-1 dhidi ya Moldova wakati wa mashindano ya kufuzu kwa Euro 2020 Ijumaa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, amefunga mabao 15 katika mechi 52 alizoichezea Chelsea tangu kujiunga nao akitokea Arsenal Januari mwaka 2018.

Lakini ujio wa Gonzalo Higuain mapema mwaka huu umemfanya Mfaransa huyo kutokuwa kwenye nafasi ya kucheza hapo Stamford Bridge.

Giroud mkataba wake na miamba hao wa London Magharibi unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua kwa miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Lyon.

Na mshambuliaji huyo ameiambia Telefoot kwamba: "Kuna uwezekano. Lakini sijapigiwa simu yoyote. Nina furaha hapa England.

"Mara zote nimekuwa na hamasa ya kucheza chini ya Rais Jean-Michel Aulas. Lyon ni klabu nzuri."

# HUDSON-ODOI

## afunguka anavyovumilia Chelsea




**LONDON,** England

WINGA wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, amesisitiza kwamba yeye si mtu wa kupaniki, licha ya uvumi kuenea kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, anataka kuondoka hapo Stamford Bridge ili kutafuta timu itakayompa nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza.

Hudson-Odoi, ambaye hivi karibuni aliichezea kwa mara ya kwanza timu ya Taifa ya England, bado hajaanza mchezo wowote kwenye Ligi Kuu.

Bayern Munich walitangaza hadharani kwamba wametenga kiasi cha pauni milioni 30 kwa ajili ya kumsajili nyota huyo Januari mwaka huu, lakini walishindwa kufikia makubaliano.

Akizungumza na Gazeti la Telegraph kabla ya mchezo wa England wa jana Jumatatu dhidi ya Montenegro, Hudson-Odoi alisisitiza kwamba bado anabakia kuwa mvumilivu wakati akitafuta klabu sahihi ya kuichezea.

Alisema: "Mara zote nina akili na mtazamo ule ule bila kujali kundi la umri iwe 18 au 21.

"Bado niko vile vile, sitabadilika nina mchezo mmoja na kikosi cha kwanza. Nitaendelea kuwa mvumilivu na kuwa mnyenyekevu na kujituma nikiwa uwanjani.

"Nina imani hiyo itanipa nafasi nzuri zaidi ya kujiamini kwa kila nitakachokuwa nikifanya.

"Mimi ni mvumilifu. Mara zote napenda kucheza soka, naupenda mchezo huu. Lakini kuna wakati unatakiwa kuwa na uvumilivu na kusubiri nafasi yako ije."

# Madrid yajipanga kumsajili Pjanic



**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, anapanga kutoa ofa ya Euro milioni 80 kwa ajili ya kiungo wa Juventus, Miralem Pjanic (pichani), ambaye ameripotiwa kwamba majaliwa yake kwenye klabu yake hayajulikani.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Bosnia, alisaini mkataba mpya na Juventus kipindi cha majira ya joto kilichopita na kumaliza uvumi kwamba anatakiwa na klabu za Chelsea na Paris Saint-Germain.



Hata hivyo, klabu yake haijaweka wazi kama ipo tayari kumuachia mchezaji huyo, ingawa yeye anataka changamoto mpya.

Kwa mujibu wa Gazeti la ilBianconero, wawakilishi wa Pjanic watakutana na Juventus mwishoni mwa msimu huu kwa ajili ya kujadiliana majaliwa ya mchezaji huyo kama ataondoka klabuni hapo.

Mshahara wake wa mwaka sasa unatarajiwa kuongezeka kutoka Euro milioni 4 hadi milioni 6.5 msimu ujao na Juventus walikuwa tayari kumlipa mshahara huo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, yeye mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kuondoka katika klabu hiyo.

Zidane anaonekana kwamba anamhitaji mchezaji huyo ili kukiimarisha kikosi chake kwa ajili msimu ujao.

## Rais Benfica akataa kumuuza Joao Felix

**LISBON,** Ureno

RAIS wa Benfica, Luis Felipe Vieira, amezionya klabu zote zinazomnyatia mchezaji wao, Joao Felix (pichani chini), kwamba, hawana mpango wa kumuuza winga huyo.

Manchester United imekuwa ikihusishwa zaidi na mpango wa kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye amekuwa akitajwa kwamba ni mmoja wa nyota wanaotarajiwa kung'ara zaidi Ulaya hapo baadaye.

Kumekuwa na uvumi kwamba 'Mashetani Wekundu' hao wameandaa ofa ya Euro milioni 120 kwa ajili ya kumsajili chipukizi huyo, huku pia Juventus, Real Madrid na Manchester City wakiwa wanamnyatia Felix.

Akizungumza na Tuttosport, Vieira amesisitiza kwamba Benfica hawana haraka ya kumuuza Felix, na hawataikubali ofa yoyote kwa ajili ya winga huyo.

Alisema: "Bilashaka Ulaya yote inazungumzia kipaji cha wachezaji wa Benfica. Sasa ni wazi kwamba mradi wetu wa kukuza wachezaji vijana unatoa matokeo chanya.

"Joao Felix ni Cristiano Ronaldo ajaye? Kuna kitu kimoja kwa uhakika kabisa: Felix ni mmoja wa wachezaji bora wanaotoka Ureno tangu Ronaldo.

"Kwa wakati huu hatuna mpango wa kumuuza na tunataka kumuongezea mkataba zaidi aendelee kuwa na sisi.

"Joao amekuwa na kiwango cha kuvutia na ni mchezaji mwenye akili. Ni mtu mzuri, anaonyesha kwamba ni mchezaji mwenye thamani kwa upande wetu na ametufanya tujisikiea fahari zaidi."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu kwenye soka la Ureno.

Katika mechi 18 alizocheza kwenye ligi, Felix amefunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho tano.



## HABARI MICHEZO

### KWA UFUPI

**KEITA KUTEMWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL inapanga kumruhusu kiungo Naby Keita, 24, kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu na itakubali kupoteza kwa nyota huyo wa kimataifa wa Guinea. **(Sun)**

**ZIDANE AMGOMEA ASENSIO**
KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amesema kiungo Mhispania Marco Asensio, 23, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool, hatauzwa na klabu hiyo. **(Mirror)**

**ANDERSEN AZIVUTA UTD, ARSENAL**
MANCHESTER United, Arsenal na Tottenham zinamfuatilia beki wa Sampdoria, Mdenmark Joachim Andersen, 22. **(CalcioMercato)**

**UNITED YAONYWA KWA MAGUIRE**
MANCHESTER United imeambiwa itapaswa kuvunja rekodi kuweza kuipata saini ya beki wa England, Harry Maguire, 26, kutoka Leicester. **(Star)**

**LIVERPOOL KUMKOSA DE LIGT**
LIVERPOOL itamkosa beki wa Ajax na Uholanzi, Matthijs de Ligt, 19, kufuatia Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, kusafiri kwenda kukamilisha dili hilo. **(Sun)**

**GODFREY AVUTIA VIGOGO EPL**
BEKI wa Norwich City, Ben Godfrey, 21, anayewindwa na Manchester United, amekuwa akifuatiliwa na wasaka vipaji wengi Ligi Kuu England. **(Sun)**

**LIVERPOOL NAYO KWA SKRINIAR**
LIVERPOOL ni klabu ya mwisho kumfuatilia beki wa Inter Milan na Slovakia, Milan Skriniar, 24. **(TeamTalk)**

**JUVE KUJIPANGA KWA VARANE**
JUVENTUS inaweza kumfuata beki wa Real Madrid, Raphael Varane, 25, baada ya Mfaransa huyo kuiambia klabu hiyo ya Hispania anataka kuondoka. **(Football Italia)**

**BALE AKARIBISHWA TENA SPURS**
GARETH Bale atakaribishwa kwa mara nyingine Tottenham kama nyota huyo ataamua kuondoka Real Madrid, amesema beki wa Spurs, Ben Davies. **(Goal)**

**BARCA YAFUNGUKA KWA CILLESSEN**
BARCELONA haifikirii kuwa kipa Mholanzi Jasper Cillessen, 29, anataka kuondoka majira haya ya joto na inaamini katika kutafuta mbadala. **(Marca)**

**ARSENAL YAMUWINDA ARIBO**
ARSENAL inapanga kumsajili kiungo wa Charlton Athletic, Joe Aribo, 22, majira haya ya joto. **(Mirror)**

**EVERTON, LEICESTER ZAMFUATA KOUTRIS**
EVERTON na Newcastle ni miongoni mwa klabu za Ligi Kuu zinazomtazama beki wa kushoto wa Olympiakos, Leonardo Koutris, 23. Leicester na West Ham pia zinamtolea jicho nyota huyo wa kimataifa wa Ugiriki. **(TeamTalk)**

**ARSENAL YAMPIGIA HESABU BARELLA**
MASHUSHU wa Arsenal wanamtazama kwa karibu kiungo wa Cagliari, Nicolo Barella, 22, aliyefunga bao lake la kwanza timu ya Taifa ya Italia dhidi ya Finland. **(Metro)**

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD AZIDI KUNOGA AKIPIGA YA 100 UBELGIJI

**Sasa amefikisha mabao 30 kimataifa wakati huu akizidi kupigiwa hesabu na Real Madrid kuelekea...**

**NICOSIA,** Cyprus

HUKU akikanusha kutokukubaliana na lolote kuhusu kujiunga na Real Madrid majira haya ya joto, kiungo mshambuliaji wa Chelsea, Eden Hazard, ameendelea kuweka rekodi zake kimataifa akiwa na Ubelgiji.

Hazard amekuwa akihusishwa na kujiunga na Real Madrid majira haya ya joto kufuatia kurejea kwa kocha Zinedine Zidane kuinoa klabu hiyo, lakini hata hivyo, Mbelgiji huyo amekana kutokuwa na mazungumzo yoyote na klabu hiyo ya Hispania wakati huu akiitumikia Ubelgiji kuelekea kufuzu Euro 2020.

Nyota huyo juzi, Jumapili alitikisa nyavu akipiga mechi yake ya 100 ya kimataifa wakati Ubelgiji ikishinda 2-0 dhidi ya Cyprus kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020.

Hazard aliuzamisha mpira kimyani katika kona ya goli dakika ya 10 baada ya kupokea pasi kutoka kwa Michy Batshuayi, ambaye aliwafinya mabeki watatu kabla ya kumpasia Hazard. Hilo likiwa bao la 30 la kimataifa kwa Hazard, na la tano dhidi ya Cyprus.

Batshuayi alifanya matokeo kuwa 2-0 dakika nane baadaye, kufuatia kuumiliki mpira kutoka kwa kaka wa Hazard, Thorgan na kuuzamisha kimyani akimzidi maarifa kipa Urko Pardo.

Ubelgiji inaongoza Kundi I ikiwa na pointi sita, tatu mbele ya Urusi, Kazakhstan, Cyprus na Scotland.

Urusi ilirejea katika makali yake ikitoka kufungwa na Ubelgiji Alhamisi na kuifunga Kazakhstan mabao 4-0 kwenye mji mpya wa Kazakh wa Nur-Sultan.

Winga wa Valencia, Denis Cheryshev alifunga mabao mawili ya kwanza ya Urusi kutokana na krosi, na kisha kumtengenezea Artyom Dzyuba kwa krosi na kufanya matokeo kuwa 3-0. kabla ya Kazakh kujifunga moja na kuwafanya wageni wao kuibuka na ushindi huo wa mabao 4-0.

HABARI MICHEZO

# OKWI: STARS WALIKUWA BORA TAIFA KUTUSHINDA

Na Faustine Feliciane

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Uganda, Emmanuel Okwi, amesema kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', kilikuwa bora zaidi yao na ndio sababu ya kuibuka na ushindi.

Juzi Stars iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Uganda na hivyo kufuzu kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 zitakazofanyika Juni mwaka huu, nchini Misri.

Akizungumza na Nipashe jana, Okwi alisema Stars walicheza vizuri na walistahili ushindi walioupata.

"Mchezo ulikuwa mgumu, tulikuwa na lengo la kushinda, lakini nafikiri Taifa Stars walikuwa bora zaidi na ushindi walioupata walistahili," alisema Okwi.

Alisema kufuzu kwa Taifa Stars kwenye fainali za Afrika ni ushindi wa Wana-afrika Mashariki kwa kuona timu nyingi za ukanda huu zimefuzu.

Mbali na Stars, timu nyingine zilizofuzu kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki ni pamoja na Uganda, Burundi na Kenya.

Stars imesonga mbele kufuatia kushika nafasi ya pili ikiwa na pointi nane, tano nyuma ya vinara wa Kundi L, Uganda, huku Lesotho ambao walikuwa wakiwania nafasi moja kuungana na Waganda hao wakishika nafasi ya tatu kufuatia kulazimishwa sare tasa na Cape Verde katika mechi yao ya juzi.

Katika mchezo wao uliochezwa muda mmoja na wa Stars, Lesotho ilikuwa ikihitaji ushindi wowote ili kufuzu hata kama Tanzania ingeshinda dhidi ya Uganda.

Mabao ya Stars juzi yalifungwa na Simon Msuva, Erasto Nyoni na Agrey Morris, huku John Bocco akitoa pasi za mwisho katika hayo mawili na moja la Nyoni lililotokana na mkwaju wa penalti, ikiwa ni juhudi binafsi za Mbwana Samatta kumnawisha beki wa Uganda ndani ya boksi.



Wachezaji wa Timu ya Taifa, 'Taifa Stars' pamoja na viongozi wengine wakiwa katika Ukumbi wa Mikutano Ikulu jijini Dar es Salaam jana, baada ya kufanikiwa kufuzu kushiriki fainali za michuano ya Mataifa ya Africa (Afcon) 2019 kwa kuifunga Timu ya Taifa ya Uganda (Cranes) mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Taifa juzi. **PICHA: IKULU**

# Stars imebebwa na mashabiki - Himid

Na Mwandishi Wetu

NAHODHA Msaidizi wa Timu ya Taifa 'Taifa Stars' Himid Mao, amesema wingi wa mashabiki kwenye mchezo wao dhidi ya Uganda, uliwapa mzuka wa kupambana hadi kuibuka na ushindi Uwanja wa Taifa juzi.

Himid aliliambia Nipashe jana kuwa, hata wachezaji ambao hawakupata nafasi ya kucheza mechi hiyo ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Misri Juni, mwaka huu, kila mmoja alikuwa na hamasa kuona wanashinda kwenye mchezo huo muhimu.

"Mimi niwashukuru sana mashabiki, wingi wao uwanjani na shangwe walizokuwa wanapiga zilitufanya kupambana kuhakikisha tunapata ushindi," alisema Himid.

Aidha, alisema walikuwa na kila sababu ya kushinda mchezo huo ili kufikia mipango yao ya kucheza fainali za Afrika, jambo ambalo wamelitekeleza kwa vitendo.

"Tunashukuru tumefanikiwa kufuzu fainali za Afrika, kila mmoja ndoto yake ilikuwa kuona tunafuzu kwa fainali hizi kwa sababu hatujashiriki kwa miaka mingi sana," aliongeza kusema Himid.

Stars iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Uganda, hivyo kufikisha pointi nane na kuungana na Uganda kufuzu kwenye fainali hizo za Afrika wakitokea kwenye Kundi L lililokuwa pia na timu za Lesotho na Cape Verde.

Hiyo ni mara ya kwanza Stars kufuzu fainali hizo tangu mwaka 1980 iliposhiriki michuano hiyo nchini Nigeria.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.Simba | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4.Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.Mbao | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Cecafa yajivunia nne kufuzu Afcon 2019

Na Mwandishi Wetu

BARAZA la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), limezipongeza timu za Taifa za Uganda, Kenya, Burundi na Tanzania kwa kufuzu fainali za Afrika (Afcon) 2019 zitakazofanyika Misri, Juni mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, ilieleza kuwa kwa mara ya kwanza, ukanda huu utakuwa na uwakilishi mkubwa katika michuano hiyo.

Katika taarifa hiyo, Musonye alisema "ni fahari kwa timu nne za ukanda huu kwa juhudi zao na kujitoa katika kufanikisha nafasi hizo. Ni ndoto ya nchi yoyote ya Afrika kucheza Afcon".

Alisema: "Kama kanda tunafurahi kuwa na timu nne kwenye tukio hili na tunaamini kuwa nchi hizo nne zitachomoza kwenye tukio hilo wakati wa michuano sahihi Misri, tunatumai serikali zetu zitasaidia maandalizi yao."

Kwa sasa Tanzania, Uganda, Kenya na Burundi zinasubiri kujua wapinzani wao wakati droo ya michuano hiyo itakapopangwa Aprili 12 jijini Cairo, Misri kuelekea fainali hizo zitakazoanza kutimua vumbi Juni 21 hadi Julai 19, mwaka huu.

Fainali hizo zinafanyika nchini Misri baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuwapokonya uenyeji Cameroon kutokana na kutoridhishwa na maandalizi ya michuano hiyo.

Nichi nyingine zilizofuzu, kutoka Kundi A; ni Senegal na Madagascar zilizozipiku Equatorial Guinea na Sudan. Kundi B; ni Morocco na Cameroon zilizozipiku Malawi na Comoro wakati Kundi C; ni Mali na Burundi zilizozipiku Gabon na Sudan Kusini.

Kwa upande wa Kundi D; ni Algeria na Benin zilizozipiku Gambia na Togo na Kundi E ni Nigeria na Afrika Kusini zilizozipiku Libya na Shelisheli.

Nyingine ni kutoka Kundi F, ambazo ni Ghana na Kenya zilizozipiku Ethiopia na Sierra Leone, wakati kutoka Kundi G; ni Zimbabwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zilizozipiku Liberia na Congo na Kundi H; ni Guinea na Ivory Coast zilizozipiku Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) na Rwanda.

Kundi I; ni Angola na Mauritania zilizozipiku Burkina Faso na Botswana na kutoka Kundi J; ni Tunisia na Misri zilizozipiku Niger na Eswatini, huku Kundi K zikiwa ni Guinea-Bissau na Namibia na Kundi L ni Uganda na Tanzania zilizozipiku Lesotho na Cape Verde.

# Michezo

Jumanne Machi 26, 2019

Nipashe




## Hazard azidi kunoga akipiga ya 100 Ubelgiji

HABARI UK. 30



Rais wa Tanzania, John Magufuli, akiwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Naibu Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, Rais wa TFF Walace Karia (wa pili kushoto), Bondia wa Ngumi za Kulipwa, Hassan Mwakinyo (wa kwanza kutoka kushoto) katika picha ya pamoja na wachezaji wa timu ya Taifa 'Taifa Stars' ambao aliwaalika Ikulu jana baada ya kufanikiwa kufuzu kushiriki fainali za michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 kufuatia kuifunga timu ya Taifa ya Uganda (Cranes) kwa mabao 3-0 Uwanja wa Taifa juzi. **PICHA: IKULU**

# MAGUFULI: VITA AFCON IMEANZA

## ●●● Ainogesha Taifa Stars, bondia Mwakinyo kwa viwanja, amwaga bilioni moja huku akiwataka...

**Na Mwandishi Wetu**

KUFUATIA kuifunga timu ya Taifa ya Uganda (Cranes) na kufanikiwa kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, amekutana na kuwapongeza wachezaji wa timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' Ikulu jijini Dar es Salaam jana na kuwaambia matarajio yake ni kuona wanajiandaa vizuri ili wakafanye vizuri katika michuano hiyo na kwamba "sasa vita imeanza".

Stars juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Uganda katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi kuwania kufuzu Afcon iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, hivyo kuungana na Waganda hao kufuzu michuano hiyo kwa mara ya kwanza tangu 1980, kufuatia Cape Verde na Lesotho zilizokuwa zikiwania nafasi hiyo katika Kundi hilo la L, kutoka sare tasa.

Lesotho ilihitaji ushindi wowote ili kuungana na Uganda kufuzu kutoka Kundi L, lakini sare hiyo iliifanya Stars kukata tiketi hiyo iliyoisotea kwa miaka 39 sasa.

Aidha, mbali na kuwapa neno hilo la matarajio yake, Rais Magufuli alitangaza kutoa zawadi ya kiwanja kimoja cha kujenga nyumba jijini Dodoma kwa kwa kila mchezaji wa Taifa Stars, Bondia Hassan Mwakinyo, mchezaji na nahodha wa zamani wa Taifa Stars, Leodgar Tenga na mchezaji wa zamani na mfungaji wa bao lililoiwezesha Tanzania kucheza robo fainali ya Afcon mwaka 1980, Peter Tino, ambaye pia alizawadiwa Sh. milioni tano.

"Nataka niwahakikishie serikali ipo nanyi na ni matarajio yangu kuwa mtajiandaa vizuri ili mkafanye vizuri katika michuano ya Afcon huko Misri, sasa vita imeanza," alisema Magufuli.

Magufuli alieleza kufurahishwa kwake na matokeo ya mchezo wa juzi na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za wanamichezo wote kwa kuwa mafanikio yao yanaliletea taifa sifa na heshima na pia yanatangaza fursa mbalimbali ikiwamo utalii, biashara na uwekezaji.

Mbali na wachezaji wa Stars, pia Magufuli amewapongeza viongozi wa TFF, Kamati ya Ushindi ya Taifa Stars na Watanzania wote kwa kuungana pamoja kuishangilia timu yao katika mchezo wa jana bila kujali tofauti zao za kidini, itikadi za kisiasa, makabila na kanda wanazotoka.

"Kwa kweli jana nilifurahi sana jinsi mlivyokuwa mnacheza na jinsi mlivyofunga magoli, Watanzania wanataka furaha, sio kufungwafungwa kama mlivyofungwa kule Lesotho, ile iliniuma sana hadi nilipanga kuwa sitaita tena timu kuja hapa Ikulu, lakini sasa safi," alisema.

Aidha, Rais Magufuli ametoa changamoto kwa wadau wote wa michezo kuhakikisha wanasimamia uboreshaji wa miundombinu ya michezo, wanajipanga vizuri kwa michezo mbalimbali ya kuiwakilisha nchi, wanarekebisha dosari zote zilizosababisha kusuasua kwa Tanzania katika michezo ya kimataifa na ameipongeza TFF kwa kufanikiwa kurejesha mgawo wa fedha za maendeleo kutoka Shirikisho la Soka duniani (Fifa).

Magufuli pia ameiagiza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kufuatilia uendeshaji wa uwanja wa Taifa ili kujiridhisha juu ya mapato na matumizi ya fedha za uwanja huo pamoja na kuangalia ubora wake kutokana na kuwapo kwa taarifa kuwa maeneo yanayoharibika hayafanyiwi matengenezo ipasavyo.

Kwa upande wa bondia Mwakinyo, Magufuli amempongeza kwa ushindi alioupata Jumamosi baada ya kumpiga kwa knockout (KO) bondia Sergio Gonzalez wa Argentina katika pambano lisilo la ubingwa lililofanyika jijini Nairobi nchini Kenya, pamoja na mapambano mengine ambayo alishinda na amemtaka kuendelea kufanya vizuri ili kuipatia sifa Tanzania.

"Nafahamu kuwa unazo changamoto nyingi ambazo hukusema hapa, lakini nakupongeza sana, juzi umemtandika yule jamaa mpaka akakaa chini na huwa nakuona unavyofanya mazoezi makali kwa kutumia matairi, wewe ni kijana safi sana," alisema Magufuli huku akiipongeza Kampuni ya Serengeti Breweries Limited ambayo ni wadhamini wa timu ya Taifa Stars na SportPesa ambao ni wadhamini wa Mwakinyo kwa mchango wao mkubwa wa kuendeleza michezo.

Kadhalika, Magufuli alikubali maombi yaliyotolewa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ya kusaidiwa maandalizi ya michuano ya Afcon kwa vijana wa chini ya miaka 17 iliyopangwa kuanza Aprili 14 hadi Aprili 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam huku Tanzania ikiwakilishwa na timu ya Serengeti Boys, ambapo amesema serikali itatoa Sh. bilioni moja kusaidia maandalizi hayo.

Kwa upande wao wachezaji wa Taifa Stars ambao waliongozwa na nahodha Msaidizi Himid Mao na bondia Hassan Mwakinyo, wamemshukuru Rais Magufuli na serikali kwa ushirikiano mkubwa walioupata hadi kufikia mafanikio hayo na wamemuahidi kuendelea kufanya vizuri katika michezo inayofuata.

Naye Rais wa TFF, Wallace Karia na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Tenga wamesema baada ya kufuzu kucheza fainali za Afcon sasa Taifa Stars inaelekeza nguvu zake kujiandaa na michuano hiyo mikubwa barani Afrika na pia wameelezea matumaini makubwa ya Tanzania kufanya vizuri katika michuano hiyo kwa vijana wa chini ya miaka 17 ambapo Tanzania itawakilishwa na timu ya Serengeti Boys, michuano ya Afcon kwa wanawake Tanzania ikiwakilishwa na Twiga Stars na kufanya vizuri kwa timu ya Taifa ya Soka chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heros) ambayo Machi 31, mwaka huu itacheza na Eritrea mjini Asmara.

Katika hafla hiyo ambayo pia ilihudhuriwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, viongozi wa Kamisheni ya Ngumi Tanzania (TPBRC) na Kamati ya Ushindi ya Taifa Stars iliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, wote walijumuika na Rais Magufuli kupata chakula cha mchana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >